# Nipashe

Jumatano Februari 5, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580146

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## Simulizi aliyejifanya mgeni wa gesti alivyotapeli simu, mchele

UKURASA 3




UKURASA 13

# Membe uso kwa uso na Mangula

**AKIRI** kupokea barua ya wito kuhojiwa Kamati ya Maadili CCM, asema yuko tayari, Polepole atoa neno... *Endelea ukurasa wa 2*



Philip Mangula



Benard Membe

# Mwamposa aachiwa kwa dhamana polisi

UKURASA 2



Msemaji wa Jeshi la Polisi, SACP David Misime na Mtume Mwamposa.

## ZITTO ADAI UPOTOSHAJI BARUA BENKI YA DUNIA

UKURASA 3

Scan Hapa



Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

**MICHEZO** KAGERE, TSHISHIMBI WAIPA SERIKALI BIL. 1.7/- UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Membe uso kwa uso na Mangula

**Na Elizabeth Zaya**

ALIYEKUWA Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Benard Membe, anatarajiwa kuhojiwa na Kamati ya Maadili ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mjini Dodoma kesho kutokana na tuhuma zinazomkabili.

Ikiwa ni takriban miezi miwili tangu kutolewa kwa agizo la kumhoji Membe na 'vigogo' wengine ndani ya chama hicho, hatimaye jana Mbunge huyo wa zamani wa Mtama, alithibitisha kupokea barua ya wito wa kuhojiwa na kamati hiyo inayoongozwa na Mwenyekiti Philip Mangula.

Membe (66), aliandika kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Twiter akieleza kwamba ameitwa jijini Dodoma kwa ajili ya kikao cha Kamati Ndogo ya Nidhamu ya CCM.

Katika ukurasa wake huo wa Twitter, Membe alisema ameitwa katika kikao hicho kitakachofanyika Februari 6 mwaka huu, yaani kesho jijini Dodoma, akisisitiza kuwa atatii wito na hatachelewa kufika.

"Hatimaye, jana jioni nimepokea barua ya kuitwa kwenye kikao cha Kamati Ndogo ya Udhibiti na Nidhamu jijini Dodoma. Kikao kitafanyika tarehe 6/02/2020 saa tatu asubuhi kwenye jengo la White House. Nitahudhuria bila kukosa na bila kuchelewa, 'stay tuned'," aliandika.

Msaidizi wa Membe, Allan Kiluvia, alithibitisha kuwa taarifa iliyotolewa kwenye ukurasa huo wa Twitter ilikuwa imetolewa na waziri huyo wa zamani.

**KAULI YA CCM**

Nipashe ilimtafuta Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Hamphrey Polepole, kuzungumzia suala hilo, lakini akasisitiza kuwa taarifa zote za kamati hiyo ni siri.

Kikao cha Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM iliyoketi Desemba 13 mwaka jana jijini Mwanza kiliazimia na kuelekeza Membe pamoja na Makatibu Wakuu wastaafu wa chama hicho, Abdulrahman Kinana na Yusuph Makamba kuhojiwa na Kamati ya Usalama na Maadili ya Taifa ya chama hicho ili kujibu tuhuma za kimaadili zinazowakabili.

Inadaiwa watatu hao sauti zao ziliwahi kusambaa katika mitandao ya kijamii zikizungumzia kupasuka kwa CCM na hata kutupia lawama uongozi wa juu ya chama. Membe alikiri mazungumzo yake ya simu kudukuliwa.

Pia, Kinana na Makamba waliwahi kuandika waraka kwa Baraza la Wazee wa chama hicho, wakilalamika kuhusu kile walichodai kuchafuliwa na mwanaharakati mmoja nchini huku chama chao kikiendelea kukaa kimya.

Mbali na hao, wengine walioonekana kutofautiana na chama hicho ni Mbunge wa Mtama, Nape Nnauye, Mbunge wa Bumbuli, January Makamba na Mbunge wa Sengerema, William Ngereja, ambao baadaye waliomba msamaha na kusamehewa.



Kaimu Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini, James Kaji (kushoto), akiwaonyesha kwa waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, vijana wawili Stanley Ngowi (katikati) na Sultani Ngowi, waliokamatwa kwa tuhuma za kusafirisha dawa za kulevya aina ya Heroin, zenye uzito wa gramu 508.163. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mwamposa aachiwa kwa dhamana

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi nchini limesema limemwachia kwa dhamana kiongozi wa dini, Boniface Mwamposa, na wenzake saba baada ya kuwahoji na kujiridhisha na yale waliyokuwa wanahitaji kutoka kwao.

Kwa mujibu wa taarifa ya jeshi hilo iliyotolewa jana na Msemaji wake, David Misime, uchunguzi bado unaendelea na baada ya kukamilika yatakayobainika yatatolewa na mamlaka husika na kutekelezwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.

"Kila mmoja anatakiwa awe na subira na uchunguzi unaofanywa na wataalamu utakapokamilika mtajulishwa," Misime alieleza katika suala hilo.

Misime alisema waliowaachia ni watu wanane, akiwamo Mwamposa, na wameachiwa kwa mujibu wa sheria ili waendelee kuripoti wakati uchunguzi ukiendelea.

"Baada ya kuhojiwa kwa kina na kujiridhisha na yale yaliyokuwa yanahitajika kutoka kwao, wamepewa dhamana kwa mujibu wa sheria ili waendelee kuripoti wakati uchunguzi ukiendelea," alisema.

Misime alidai amekuwa akipokea simu nyingi kutoka kwa watu mbalimbali wakiuliza maendeleo ya uchunguzi wa tukio hilo.

"Kama ilivyokwisha kuelezwa na viongozi mbalimbali na kwenye taarifa yangu kwenu (waandishi wa habari) ya juzi, hatua mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa.

"Ni kwamba baada ya tukio hilo la watu 20 kupoteza maisha katika mkutano wa Mwamposa, Mkuu wa Jeshi la Polisi, Simon Nyakoro Sirro, alituma timu ya maofisa, wakiwapo wataalamu wa uchunguzi wa sayansi ya jinai kwenda kuungana na timu ya wataalamu kule Kilimanjaro katika uchunguzi," alisema.

Watu 20 walifariki dunia kwa kukanyagana katika viwanja vya Majengo Februari Mosi mwaka huu, wakidaiwa kuelekezwa na kiongozi wa dini kupita kwenye malango ambao kulikuwa kumemwagwa mafuta yanayodaiwa kuwa na upako.

## Mtaalamu aeleza sababu ongezeko maradhi saratani

**Na Romana Mallya**

TIBA mbadala imetajwa kuwa moja ya sababu za wagonjwa wa saratani kufikishwa hospitalini wakiwa hatua ya mwisho ya ugonjwa, hivyo kusababisha vifo.

Wakati hayo yakielezwa, ugonjwa wa saratani, kwa mujibu wa takwimu za dunia, unashika nafasi ya pili kwa kusababisha vifo vingi.

Muuguzi Mtaalamu wa Magonjwa ya Saratani, Nyakaje Mashauri, kutoka hospitali ya Aga Khan aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya Siku ya Saratani Duniani yaliyobebwa na kaulimbiu isemayo, 'I am and I Will' (Mimi na Nitafanya).

Mashauri alisema miongoni mwa wagonjwa wa saratani wanaofikishwa hospitalini, kupelekwa wakiwa katika hatua za mwisho za ugonjwa na moja ya sababu ni baadhi huanzia kwa waganga wa kienyeji.

Alisema baadhi yao wako ambao wanapoanza tiba ya hospitali huzichanganya na za waganga wa tiba asilia.

"Nimekutana na wagonjwa wanaofanya matibabu pande mbili, kwa waganga wa kienyeji na hospitali. Sasa hii inakuwa ngumu kumuhudumia mgonjwa wa aina hii.

"Unamweleza fuata hivi anakwenda kwa waganga atapewa dawa, mara kuchanjwa chale na wakati mwingine anashindwa kuja kufanya vipimo kwa wakati hospitalini na mwisho wa siku wengine wanajikuta wanafika hospitali wakiwa hatua ya mwisho ya ugonjwa," alisema.

Kwa kawaida, alisema hospitali hiyo imekuwa ikipokea wagonjwa 10 hadi 12 kila siku ambao huenda kwa ajili ya matibabu lakini wengi wao huwa katika hatua ya tatu au ya nne ya ugonjwa.

"Wagonjwa wa aina hii tunawapa matibabu ya muda mrefu zaidi tofauti na wale wanaokuja wakiwa hatua ya kwanza na ya pili ya ugonjwa ambao hupewa tiba ya muda mfupi na kupona kabisa.

"Hii linatokana na jamii kutokuwa na elimu ya kutosha namna ya kujikinga na kutibu dhidi ya saratani. Na hawa ni wagonjwa wa kutoka mjini, nina hofu kwa wale walioko vijijini ni kiasi gani watu wanavyoumwa, tunahitaji kuendelea kuielimisha jamii."

Alisema hali ya ugonjwa huo inaongezeka kila siku na imekuwa mbaya zaidi kwa sababu wengi wanafika hospitali wakiwa wamechelewa.

Kuhusu uchangiaji wa damu uliokuwa ukifanywa hospitali hapo kwa ushirikiano wao na Mpango

INAENDELEA UK 8

## HABARI KITAIFA




Meneja wa kiwanda cha uchenjuaji wa madini cha Rendisco (Elution Plant), Amina Hussein, akipandishwa kwenye gari la Polisi, baada ya kudaiwa kuweka steel wire kwenye mashine wakati wa uchenjauji wa madini, kwa lengo la kumwibia mteja aliyefika kiwandani hapo, katika Kata ya Malunga, Halmashauri ya Mji wa Kahama jana, kuchenjua dhahabu. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Simulizi aliyejifanya mgeni alivyotapeli simu na mchele

**Na Steven William, MUHEZA**

MTU anayedaiwa kuwa mkazi wa Kijiji cha Sega, Kata ya Mapapayu wilayani Muheza, Abdi Kosovo, anadaiwa kutapeli simu mbili za thamani na kilo 60 za mchele katika mazingira ya kutatanisha kwa wananchi wa mtaa mmoja.

Tukio hilo lilitokea juzi eneo la Majengo mjini hapa, hivyo wananchi kubaki midomo wazi kutokana na mtuhumiwa huyo kuwaibiwa wananchi simu mbili za gharama ya juu na mchele kilo 60 dukani kwa mazingira ya ajabu.

Mfanyakazi wa nyumba ya kulala wageni ya Upare, eneo la Majengo Nje, Mariam Athumani, alisema mtu huyo ameiba simu za thamani za Asha Mashaka na Beatrice Mhando na kilo 60 za mchele katika duka la Mussa Mpare.

Kwa mujibu wa Mariam, mtu huyo alifika katika nyumba hiyo na hatimaye kuchukua chumba cha kulala.

Mariam alisema baada ya kuchukua chumba na kuweka mizigo yake, alitoka nje na hatimaye kukaa na wafanyakazi wa nyumba hiyo pamoja na Asha Mashaka, anayeishi jirani na nyumba hiyo.

Alisema wote kwa pamoja walikaa katika kivuli cha mwembe na kuanza kuwaagizia vinywaji akawa anawanunulia wafanyakazi hao, hivyo kujenga mazoea nao.

"Ilipofika siku ya pili asubuhi, aliamka katika chumba chake alicholala na kumwita mhudumu na kumuuliza hakuna duka karibu anataka kununua mchele kilo 60, mafuta na unga wa ngano pamoja na sukari kwa wingi," alisema.

"Mara ya kwanza aliondoka mhudumu kwenda katika duka, lakini alikuta limefungwa ndipo aliporudi na kutoa mrejesho kwamba duka limefungwa labda baadaye atakapofungua.

Baada ya muda alipita Asha ambaye walikuwa wamekaa pamoja siku ya kwanza na kuongozana naye kwenda dukani ambalo walikuta duka liko wazi," alisema.

Alisema walipofika, Asha alimwambia mwenye duka ampimie vitu anavyotaka kwa kuwa hana wasiwasi kwa sababu amefikia katika nyumba ya kulala wageni ya Upare na mwenye duka akakubali kufanya hivyo.

Mtu huyo, alisema alipimiwa mchele kilo 60 na kukabidhiwa huku akiendelea kupima unga wa ngano wakati huo Kosovo akiondoka na mchele kwamba anakwenda kwenye nyumba ya wageni alipofikia ili kuchukua fedha na kumalizia vitu vingine baada ya malipo.

Wakati akifanya hivyo, alisema alimwomba Asha ampe simu yake ili akapigie hesabu ya gharama ya vitu alivyoagiza dukani.

Alisema kuwa tapeli huyo aliondokana na simu za Asha na Beatrice pamoja na mchele kilo 60 na kutokomea kusikojulikana.

Mfanyakazi huyo alisema baada ya dakika 10 kupita, mwenye duka alishtuka baada ya kuona mtu huyo harudi kupeleka fedha za mchele na vitu vingine alivyopimiwa, lakini hajachukua pamoja na simu ya Asha aliyoomba kwenda kupigia hesabu.

Kwa mshangao huo, alisema ndipo walipofunguka na kujua kuwa wameibiwa na kuanza kumsaka mtu huyo bila mafanikio.

Kutokana na tukio hilo, alisema wamekwenda kutoa taarifa kituo kikuu cha Polisi Wilaya ya Muheza kuhusu kuibiwa kilo 60 za mchele na simu mbili.

Ofisa mmoja wa Polisi (jina linahifadhiwa) alikiri kuripotiwa kwa tukio hilo na kwamba wanamsaka mtu huyo.

# Zitto adai upotoshaji barua Benki ya Dunia

**Na Enock Charles**

MBUNGE wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe (ACT-Wazalendo), amedai kuna upotoshaji kuhusu barua aliyoiandikia uongozi wa Benki ya Dunia (WB) kuhusu mkopo wa Dola za Marekani milioni 500 ambao Tanzania imeomba kwa benki hiyo.

Akiwa mjini Toronto, Canada juzi, Zitto alidai si lengo lake kuzuia misaada nchini ila anafanya hivyo ili kuwalinda watoto wa kike wanaopata ujauzito wakiwa katika masomo kwa kile alichodai kuwapo ubaguzi katika mfumo rasmi wa elimu nchini.

"Kwanza kuna upotoshaji wa suala hili zima kwa sababu nimeandika barua siyo kuzuia misaada ila kuitaka Benki ya Dunia kabla ya kutoa mkopo kwa Serikali ya Tanzania, izingatie kuwa mkopo ule unakwenda kuwabagua watoto wa kike ambao wamepata ujauzito na kuzuiwa kurudi shuleni," alidai.

Wiki iliyopita baada ya kuibuliwa kwa suala hilo bungeni jijini Dodoma, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alimtaka Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Profesa Adelardus Kilangi, kuchunguza kitendo hicho cha Zitto ili kuona kama kuna jinai au la.

Alisema uchunguzi huo unapaswa kufanyika ili kama kutaonekana kuwapo kwa jinai, mbunge huyo achukuliwe hatua kufuatia hoja binafsi iliyowasilishwa bungeni na Mbunge wa Siha, Dk. Godwin Mollel (CCM), aliyetaka kuchunguzwa kwa jambo hilo.

"Mbunge mwenzetu atakaporudi, labda anaweza akatufafanulia wenzake, Mheshimiwa Zitto Kabwe kuandika barua Word Bank (Benki ya Dunia) kwamba nchi yetu ikose fedha za mkopo ambazo lengo lake ni elimu kwa sababu ya tofauti za sera," Spika Ndugai alisema.

Akijenga hoja yake siku hiyo ili aungwe mkono na wabunge, Dk. Mollel alisema: "Nasimama kwa Kanuni ya 47(1) ili kuomba kuahirisha shughuli za Bunge ili kujadili jambo la dharura. Hapa juzi mwenzetu Zitto ameandika barua kwenye Benki ya Dunia, na alipoandika barua kwenye Benki ya Dunia, alitaka fedha zizuiliwe ambazo zingekuja kusaidia elimu Tanzania.

"Lakini, pesa hizo zingekuja tungejenga shule tano kubwa kwa kila wilaya, tungeweza kuwaweka bwenini watoto zaidi ya 2,000 wa kike ambao mwisho wa siku hata kiwango cha mimba kwa taifa letu kingeshuka sana."

Alisema wabunge waliapa bungeni kwa kutumia Katiba ya Tanzania na katiba hiyo imetaja dhahiri maadui wa taifa ukiwamo umaskini, ujinga na maradhi.

Alisema unapogusa kwenye eneo hilo la elimu ina maana umefuta ujinga, umaskini na maradhi, hivyo akadai Zitto anapaswa kuchukuliwa hatua kwa kuwa amevunja katiba.

World Vision

**SEEKING FOR PROSPECTIVE BOARD MEMBERS**

***"Then Jesus, moved with compassion, stretched out his hand"*** Mark 1:40.

This is a call on the hearts of those with compassion to reaching out to children and communities in need, through the World Vision Tanzania. World Vision is a Christian, Child Focused and Community Empowering Non-Governmental Organization (NGO), operating in 16 Regions in Tanzania. We wish to recruit highly qualified, motivated, very dedicated and results oriented Christian leaders/influencers in their respective fields to serve as Board members **on a voluntary basis.** Collectively, the qualified candidates should represent a relevant diversity in experience, competence, age, gender, church affiliation, ethnicity, and geographic backgrounds. As such, both men and women are encouraged to apply.

The individuals should be able to provide thought leadership to development issues and have a track record as key contributors to poverty reduction and development at a policy level. This may be evidenced by previous participation at the executive or board level in the public, private or non-profit sector where the organizational outcomes are clearly contributing to positive social change

Currently, we are seeking for an individual with demonstrated high-level expertise that contributes to positive social change in Tanzania in one of the following sectors:

1. Development Management especially in the areas of Economic Development, Health, Education and Agriculture
2. Advocacy
3. Church Leadership/Church Relations
4. Fundraising/Resource Mobilisation/Marketing / Public Relations
5. Governance

**Other helpful qualities include:**

- Being a witness to the good news of the Kingdom of God, through selflessly serving the communities
- A heart for the poor and a good steward to the Ministry of World Vision Tanzania.
- English language fluency (written and verbal).
- Good communication skills including public speaking and presentation skills
- Must be a resilient, humble and committed Christian who participates in the worship and life of a local church (a Trinitarian denomination)
- Willing and available during her/his tenure, to participate in the Board and its committees **on a voluntary** basis since serving at World Vision Tanzania Board is a Ministry.

As a child-focused organization which upholds the rights and well-being of children; our recruitment and selection procedures include screening and background checking for child abuse offences. Please send an application letter explaining why you would like to be on the Board and attach a CV with church and professional references to **david_ombeni@wvi.org by 23rd February 2020.**

215616702

# Waziri Kairuki awaeleza wabunge ajenda uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Agellah Kairuki, amewaeleza wabunge kwa undani utekelezaji wa ajenda ya taifa ya uwekezaji na kusema kutokana na uzoefu uliopatikana wa sheria ya mpya za uwekezaji, uboreshaji wa mazingira ya biashara na uvuvi zinaandaliwa na serikali.

Akijibu maswali na michango ya wabunge wa kamati 12 za kudumu za Bunge waliookutana naye jijini Dodoma juzi, waziri huyo alisema sheria mpya zinandaliwa kusawazisha upungufu uliyojitokeza na kuimarisha mafanikio yaliyopatikana.

"Mafanikio yetu katika kutekeleza ajenda ya taifa ya uwekezaji ni makubwa na yako wazi. Lakini tumejifunza mambo mengi; tumekutana na changamoto pia. Tanakuja na sheria mpya ili tuwe na mifumo iliyo bora zaidi. "Miswada hiyo tukiileta mbele yenu tunaomba ushirikiano wenu."

Alizitaja sheria mpya kuwa ni sheria ya uwekezaji na sheria ya kuboresha mazingira ya biashara. Akijibu swali, Kairuki aliwahakikisha wabunge kwamba hakuna taasisi maalumu duniani inayotoa taarifa juu ya uwekezaji katika nchi za dunia, na kufafanua kwamba hata hivyo zipo taasisi zinazofuatilia mienendo ya uwekezaji duniani.

Alisema Tanzania siyo kisiwa, na kwa hiyo inaangalia mifumo, matatizo, changamoto na mafanikio ya nchi nyingine hasa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Alisema ujumbe wa Tanzania umetembelea Rwanda na kubadilishana uzoefu na wajumbe wa Bodi ya Maendeleo ya Rwanda juu ya utalii na uwekezaji.

"Wenzetu wanasema wana mlango mmoja na dirisha moja. Tumegundua kwamba hata sisi tunafanya vizuri sana; tunayo milango mingi inayotatua masuala yote katika jengo moja tu."

Kuhusu diplomasia ya uchumi, Kairuki alisema wizara yake inashirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje ili kuona balozi za Tanzania zinatumika vizuri katika kutafuta wawekezaji.

Amewaeleza wabunge mambo mawili yanayowekewa msisitizo na wizara katika eneo hilo; kwanza ni kuwapo kwa kitengo cha intelijensia juu ya uwekezaji.

Alisema kitengo hicho lengo lake ni kuwasaidia mabalozi kufahamu na kujishughulisha tu na wawekezaji maarufu na mahiri walao 10 katika maeneo yao. Pili; ni kuwatumia watu wenye ushawishi na maarufu, wanaoitwa branding ambassadors, kutangaza fursa za Tanzania za utalii na uwekezaji na

kwamba matumizi ya watu hao yameleta mafanikio China, Uturuki na Italia.

Kairuki ameeleza pia kwamba katika kupambana na urasimu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Mei 18, 2019 alikutana na mawaziri wote wa kisekta na kukubaliana juu ya utekelezaji mzuri wa mwongo (blue print) juu ya uwekezaji na uboreshaji wa mazingira ya kufanya biashara.

Alisema kuwa ni mikutano ya aina hii ndiyo imeibua haja ya kuandaa rasimu ya sheria mpya kuboresha mazingira ya biashara. Kuhusu upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji, alisema kwamba wizara yao inashirikiana na Wizara ya Ardhi kupitia kitengo cha benki ya hifadhi ya ardhi.

Alisema sasa vijiji vinahimizwa kutenga ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa muda mrefu ili wawekezaji watumie muda mfupi kupata ardhi kwa mahitaji yao.

Katika jitihada ya kutatua kero za wawekezaji na wafanyabiashara, alisema wametembelea mikoa minane na baada ya kikao cha bunge watatembelea mikoa ya Mara, Simiyu, Shinyanga na Mwanza.

Pia alieleza wamekutana na wawekezaji wa kigeni kutoka China, Marekani na Uingereza. "Tumewaeleza, tumesikiliza changamoto zao na kuzitafutia ufumbuzi, na ziara hizi zimetuonyesha umuhimu na manufaa ya uwekezaji katika kukuza uchumi wa taifa," alieleza.

Kuhusu uvuvi katika bahari kuu, Kairuki alisema pia sheria mpya nako inakuja, lakini akafafanua kuwa kikwazo kikubwa ni ukosefu wa meli na boti kubwa za kufanya uvuvi katika bahari kuu.

Alisema eneo hilo ni muhimu kwa uchumi na kutoa mfano wa Kampuni ya Alfa ya Mafia na kusema katika kipindi cha mwaka mmoja tu soko lake la nje limeingiza zaidi ya shilingi bilioni 210.

Akijibu hoja ya kwamba uwekezaji unanufaisha mikoa michache yenye miundombinu, Waziri Kairuki aliwahikishia wabunge kwamba sheria mpya ya uwekezaji itaeleza vigezo vya uwekezaji ili mikoa yote inufaike na fursa zilizomo katika maeneo yao bila kukwama kwa sababu ya kukosa vitu kama bandari, barabara, reli na aina nyingine za miundombinu.



Mkuu wa Idara ya Huduma za Kifedha wa Benki ya NMB, Linda Teggisa, akichangia mada wakati wa mkutano na wadau wa maendeleo ya bima kubwa nchini, uliofanyika katika Wizara ya Fedha na Mipango na kuratibiwa na Taasisi ya Africa Trade Insurance (ATI), jijini Dodoma jana. Kulia ni Meneja Uhusiano wa Wateja Wakubwa wa Benki hiyo, Amour Muro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sababu kesi vigogo Nida kukwama

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imeshindwa kuendelea kuisikiliza kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili aliyekuwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), Dickson Maimu na wenzake wanne, baada ya hakimu aliyepangiwa kusiikiliza kuwa na udhuru.

Maimu na wenzake wanakabiliwa na tuhuma za uhujumu uchumi ikiwamo kuisabishia serikali hasara, kutakatisha Sh. bilioni 1.175, kughushi, kuwasilisha nyaraka za uongo ili kumdanganya mwajiri wao, kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu na matumizi mabaya ya madaraka.

Wakili wa Serikali Mkuu, Zacharia Ndaskoi, alidai mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, kuwa kesi ilipangwa kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa, na kwamba upande wa Jamhuri umeita shahidi mmoja, Emmanuel Korosso, lakini kwa bahati mbaya Hakimu Salum Ally anayeisikiliza kesi hiyo amepata udhuru.

Hakimu Shaidi aliahirisha kesi hiyo hadi Februari 17, 2020, na kuagiza Korosso afike mahakamani siku hiyo.

Mbali na Maimu, washtakiwa wengine wanaokabiliwa na kesi hiyo ni Meneja Biashara wa Nida, Aveln Momburi, Ofisa Usafirishaji, George Ntalima, Mkurugenzi wa Sheria, Sabina Raymond na Xavery Kayombo.

Katika kesi hiyo, upande wa Jamhuri unatarajia kuwaita mashahidi 60 na vielelezo 200.

# Nyumba za walimu zageuzwa danguro

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MAJENGO mawili ya nyumba za walimu ambayo ujenzi wake haujakamilika katika Shule ya Sekondari Mwasele, Kata ya Kambarage, Manispaa ya Shinyanga, yamedaiwa kugeuzwa danguro na kusababisha baadhi ya wanafunzi kupewa ujauzito na kuacha masomo.

Diwani wa Kambarage, Hassani Mwendapole, alipaza kilio hicho wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani la manispaa hiyo kilichojadili utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20 ya Sh. bilioni 41.5 kwa kipindi cha nusu mwaka.

Alidai miradi mingi ya maendeleo imeendelea kuwa kiporo, zikiwamo nyumba mbili za walimu zilizoko katika shule hiyo, ambazo kwa sasa zimegeuka kuwa 'guest house' na kusababisha ujauzito kwa wanafunzi shuleni hapo.

"Nyumba hizi za walimu katika Shule ya Sekondari Mwasele zilijengwa tangu mwaka 2011 na sasa kuna mapagale tu, na yameshageuka kuwa kama guest house, zinatumika kwa ngono na kusababisha kuwapo mimba za wanafunzi," alilalamika.

Diwani wa Viti Maalum, Shela Mshandete, alitoa ushuhuda kuwa kwenye majengo hayo ya nyumba za walimu ambayo hayajakamilika kujengwa, kuna wanafunzi walishakamatwa wakifanya ngono.

Pia Diwani wa Mwamalili, Paulo Machela, alisema kuna haja ya kukamilisha miradi ya maendeleo ambayo ni viporo, akieleza kuwa mingi ilijengwa kwa nguvu za wananchi.

Naibu Meya wa Manispaa ya Shinyanga, John Kisandu, aliuagiza uongozi wa manispaa hiyo kuhakikisha hadi kufikia Juni mwaka huu, unakamilisha miradi ambayo ni viporo, na ile ambayo haitakamilika, iingizwe kwenye bajeti ya mwaka ujao wa fedha.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Geofrey Mwangulumbi, alisema tayari alishamwagiza mchumi wa manispaa hiyo, Gwakisa Mwashebya, afuatilie miradi yote ambayo ni viporo ili kupata idadi kamili.

## HABARI KITAIFA



Baadhi ya wafanyakazi wa machinjio ya ng'ombe ya serikali yaliyopo eneo la Kizota jijini Dodoma, wakiwa kazini kuandaa nyama kwa ajili ya kupeleka sokoni, juzi. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Mbaroni kwa tuhuma kutumikisha watoto

**Na Christina Haule, KILOSA**

JESHI la Polisi mkoani Morogoro linamshikilia John Darus, mkazi wa Dumila wilayani Kilosa, kwa tuhuma za kuwatumikisha watoto wadogo watatu wenye umri wa kwenda shule kinyume cha sheria.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, alidai jana kuwa walipata taarifa kutoka kwa wasamalia wema Februari Mosi mwaka huu juu ya utumishwaji huo wa watoto na kuanza kufuatilia na hatimaye kumkamata.

Alidai mtuhumiwa alikuwa akiwatumikisha watoto watatu akiwamo mmoja mwenye miaka mitatu, akiwalipa ujira kidogo.

Kamanda Mutafungwa alidai watoto sasa wako katika mikono salama ya ustawi wa jamii walioshirikiana na jeshi hilo kupitia dawati lake la jinsia la mkoa kumkamata mtuhumiwa.

Alidai wapo kinamama wengi wenye kufanya vitendo kama hivyo vya kuwatumikisha watoto wadogo wanaostahili kwenda shule, akiwatakia kutambua kufanya hivyo ni kuvunja sheria za nchi.

**UKAHABA**

Kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi pia alidai wamewakamata wanawake 11 katika maeneo ya Manzese na Kahumba, Manispaa ya Morogoro kwa tuhuma za kufanya biashara ya ngono.

Kamanda Mutafungwa alidai watuhumiwa hao walikamatwa juzi usiku katika maeneo hayo wakiendesha biashara ya kuuza miili yao.

Alidai wanaamini kukamatwa kwa wanawake hao kutasaidia kupunguza vitendo vingine vya kihalifu, ukiwamo ujambazi, akieleza kuwa kundi hilo wakati mwingine limekuwa likitumiwa na wahalifu.

**Kamanda Mutafungwa alidai watoto sasa wako katika mikono salama ya ustawi wa jamii walioshirikiana na jeshi hilo kupitia dawati lake la jinsia la mkoa kumkamata mtuhumiwa.**

# Mkandarasi aja kutatua shida kubwa ya maji Dar

**Na Frank Monyo**

SERIKALI imesema imemwajiri mkandarasi kutoka kampuni ya Heinan International Ltd ya China baada ya kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa tangi la maji la Changanyikeni ili kuendesha mradi wa kulaza mabomba na kusambaza maji katika maeneo takribani 20 ya Jiji la Dar es Salaam na Bagamoyo ambayo yana tatizo kubwa la maji.

Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo, ndiye aliyetoa taarifa hiyo, alipokuwa akizungumza na Nipashe jana jijini Dar es Salaam, baada ya kukamilika matangi matano yaliyojengwa katika maeneo ya miinuko ya Changanyikeni, Salasala, Wazo, Mabwepande na Bagamoyo pamoja na ujenzi vituo vinne vya kusukuma maji.

Prof. Mkumbo, alisema baada ya kukamilika kwa ujenzi wa tangi la Changanyikeni, hatua inayofuata ni ya usambazaji wa maji kwenye maeneo ambayo ni korofi kwa muda mrefu katika upatikanaji wa maji jijini Dar es Salaam na Bagamoyo.

Alisema gharama za mradi huo ni Sh. bilioni 77 fedha ambazo serikali imekopa kutoka Benki ya Dunia, na kuwa ambapo mradi huo utaendeshwa kwa ushirikiano kati ya kampuni ya Chengdu Industrial equipment installation na Heinan International Ltd kutoka China.

Alitaja maeneo yatakayofikiwa na mradi kuwa ni Changanyikeni, Goba, Madale, Msakuzi, Mabwepande, Kwembe, Mji wa Bagamoyo na maeneo yote ya ukanda wa Dar es Salaam ambayo yanashida ya maji kwa muda mrefu.

"Baada ya mradi huo kukamilika Dar es Salaam, tutakuwa tumekamilisha kutatua shida ya maji, sehemu itakayobaki ni Dar es Salaam ya Kusini kwa maana ya kuanzia eneo la Kigamboni, Gongolamboto, Chanika mpaka Pugu kwa hiyo tunatarajia kutibu tatizo hili kwa mradi wetu mmoja wa Kimbiji na hivi karibuni Dawasa wamekamilisha mradi wao Kisarawe ambao ulifunguliwa na Waziri wa Tamisemi (Suleman Jafo)," alisema Mkumbo.

Aliongeza kuwa changamoto iliyopo hivi sasa ni chanzo cha maji na serikali inafanya kazi kubwa kubaini chanzo cha maji kipya na kuamua kutumia chanzo cha maji cha Mto Rufiji.

Katika hatua nyingine, Prof. Mkumbo aliwapongeza Dawasa kwa juhudi ya kusimamia miradi mikubwa ya maji hadi kukamilika, huku wakiiendesha kwa fedha zao za ndani.

Alisema Dawasa imekuwa wasimamizi wazuri wa miradi ya maji na wamefanikiwa kusimamia mradi wa ujenzi wa matangi na vituo vya kusukumia maji vilivyojengwa na mkandarasi Jain kutoka India na kusimamiwa na kampuni ya WAPCOS.

Akizungumzia mradi mkubwa wa maji Mkoa wa Dar es Salaam, alisema ulikuwa kwa ajili ya kuboresha na kuongeza huduma ya maji kwa maeneo yaliyokuwa na changamoto kubwa ya maji, na kuwa ulihusisha ujenzi wa matangi matano ya maji na vituo vya kusukumia maji (booster station).

"Kulikuwa na awamu mbili, tulianza na kuongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 300 hadi 500 kwa siku, na awamu ya pili ikiwa ni ujenzi wa matenki sambamba na vituo vya kusukumia maji kwenda katika matenki ya kuhifadhia maji yaliojengwa maeneo tofauti," alisema na kuongeza:

"Mradi huu umekamilika, baadhi ya maeneo wananchi wameanza kupata maji kama vile maeneo ya Salasala na kilichobaki ni kwa viongozi kuja."


**BANI INVESTMENT LIMITED**
**DEBT COLLECTORS/ AUCTIONEERS**

**NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA KWA WADAIWA WA NBC BANK MAKAO MAKUU DAR ES SALAAM**

Kwa idhini tuliyopewa na **BENKI YA NBC MAKAO MAKUU** tunatoa notisi ya siku 14 na tangazo la mnada wa hadhara wa mali zilizoorodheshwa hapo chini ambazo ziliwekwa kama dhamana ya mkopo. Hivyo basi utakapopita muda wa siku kumi na nne tangu kutoka kwa gazeti hili,Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada.Mnada utafanyika mahali zilipo mali hizi, siku na saa kama ilivyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:-

| JINA LA AKAUNTI | MMILIKI | MALI ZILIZOWEKWA DHAMANA | MAHALI | TAREHE | MUDA |
|---|---|---|---|---|---|
| Kiokimwe-General Supply And Co | Charles John Mchome | Nyumba yenye C.T NO. 56569, L.O NO. 214770 , PLOT NO 26 | Korogwe-Kibaha | 19.2.2020 | 4:00 asubuhi |
| Mackson s Luganuza | Mackson Luganuza Spratus | Nyumba yenye CT NO.26254-LRMWANZA, L.O. NO.399415, PLOT NO.48 BLOCK 'B' | Kibeta - Bukoba | 19.2.2020 | 4:00 asubuhi |
| Brown J. Simsokwe | Brown John Simsokwe | Nyumba yenye CT NO. 9694-MBYLR, L.O. NO. 176177, Plot NO. 185, BLock 'X' | Mfaranyaki-Songea | 19.2.2020 | 4:00 asubuhi |
| Samora Robert Mandalu | Samora Robert Mandalu | Nyumba yenye CT NO.26834 L.O. NO 194982 PLOT NO.54 BLOCK L | Kidinda-Bariadi | 22.2.2020 | 4:00 asubuhi |
| Kurwaki Supplies And Serv | Shaban James Nyamasagara | Nyumba yenye CT NO. 97377, L.O. NO. 492012, PLOT NO. 167, BLOCK 'H' | Madale-Manispaa ya Kinondoni | 22.2.202 | 4:00 asubuhi |
| Victor L Mgani | Victor Ludandila Mgani | Nyumba yenye CT NO.10295-MBYLR, L.O. NO.149010,PLOT NO.61 BLOCK "L" | Njombe | 22.2.2020 | 4:00 asubuhi |
| Mashaka Sengo Nyadu | Mashaka Sengo Nyandu | Nyumba yenye CT NO.36584-LR MWANZA, L.O NO.223800, PLOT NO.50 BLOCK 'B' | Mwakipugila-Meatu | 26.2.2020 | 4:00 asubuhi |
| Mgaya Oscar | Oscar Mgaya | Nyumba yenye CT NO. 9391-MBYLR, LO NO. 174756, PLOT NO. 55 BLOCK 'Q' | Tukuyu | 26.2.2020 | 4:00 asubuhi |
| Roberth M. Yaseba | Robert Mhangwa Yaseba | Nyumba yenye C.T NO.39257-LR MWANZA, L.O. NO. 389302, PLOT NO. 134, BLOCK 'A' | Kagongwa-Kahama | 29.2.2020 | 4:00 asubuhi |
| Bukumi Inv Limited | Donald Migo Ndaro | Nyumba yenye CT NO.31678-MBYLR, L.O. NO. 582517, PLOT NO. 122 Block 'A' | Isakalilo-Iringa | 29.2.2020 | 4:00 asubuhi |
| Ernest Wilson Loth | Jeremiah Fusso Manyiwa | Nyumba yenye CT.NO. 23629LRMWANZA, LO NO 370493, PLOT.NO. 349, BLOCK 'H' | Kazehill-Tabora | 4.3.2020 | 4:00 asubuhi |
| Makiya | Mashaka Omary Makiya | Nyumba yenye Plot NO.211 Block 'Z' | Kindai-Singida | 7.3.2020 | 4:00 asubuhi |
| Aron P Shaka | Aron Paul Shaka | Nyumba yenye C.T NO.9538- DLR, L.O NO. 115643, PLOT NO. 570 BLOCK 'BB' | Kibaoni - Singida | 10.3.2020 | 4:00 asubuhi |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mali zitauzwa "kama zilivyo " as is where is basis"
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada na kiasi kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki ni juu ya mnunuzi
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wowote isipokuwa usiku.

215616002

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na Ofisi ya:**
Kwa maelezo zaidi wasiliana Na ofisi ya **BANI INVESTMENT LTD** Nkurmah Street, Lida Building, Ghorofa ya 3, Chumba No. 0313 S.L.P 71340 Dar es Salaam au kwa simu na.
**0713 224578, 0713, 295747, 0653 640999.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Maafa Moshi liwe somo kuhudumia mikusanyiko

LILILOTOKEA Moshi na kusababisha vifo vya watu 20 na majeruhi kadhaa katika ibada ya kukanyaga mafuta linatoa funzo kwa kila mmoja kuanzia waumini hadi mamlaka za dola.

Tunawapa pole wafiwa, majeruhi na familia ya Wakristo na waumini ambao msiba huo umegusa maisha yao na wengine imani yao.

Hata hivyo, si wakati wa kulaumiana bali ni muda mwingine wa kufarijiana na kupeana tumaini jipya kuwa kifo ni lazima kitokee na kwa hilo hakuna huruma, mtoto mchanga kama ilivyo kwa mtu mzima au mzee wote hufariki.

Lakini, somo kubwa linalopatikana katika msiba huo ni kujipanga na kujizatiti kikamilifu kuhudumia umati.

Tungependa kuvishauri vyombo vya dola kuzingatia haya wakati panapokuwa na umati au kusanyiko kubwa ambalo panapotokea tatizo ni vigumu kulishughulikia mara moja licha ya watu kupoteza maisha.

Tunashauri kwanza kuhakikisha eneo linalofanyika mkutano linakuwa na nafasi ya kutosha. Mamlaka ziangalie ukubwa wa eneo na kulilinganisha na idadi ya watu watakaoingia ndani ya uwanja au ukumbi.

Tunaona kuwa ni wakati wa kudhibiti uingiaji kiholela na kujazana kupindukia kwenye mikusanyiko. Ikumbukwe zama hizi kuna teknolojia ni vyema kutumia video na kuonyesha tukio linaloendelea kupitia utaratibu huo.

Aidha, jambo muhimu la kuangalia pia ni milango ya kuingilia na kutokea uwanjani au ukumbini. Tunaona kuwa ni lazima iwe mingi ili itoshe kuhudumia watu wengi na kuondoa uwezekano wa msongamano na kuumizana kwa kukanyagana.

Kusanyiko kubwa lina watu wengi wenye shida mbalimbali kama ni mikutano ya maombezi ni vyema kuwa na eneo mahususi kwa ajili ya wasiojiweza kama wagonjwa, wenye ulemavu, wazee, watoto na wajawazito ili kupunguza uwezekano wa kuwaumiza kwa vile wengi hawawezi kujitetea.

Halikadhalika, ni wakati wa kufikiria pia uwezekano wa kuwa na huduma ya kwanza na ya uokoaji kwa kutumia wataalamu, vifaa tiba na vyombo vya kisasa kama helikopta ili kupunguza ukubwa wa maafa.

Tunashauri kuwa ni vyema pia kuhakikisha kuwa iwapo patakuwa na tukio linalofanana na hilo la kukanyaga mafuta ambalo linahusisha pengine watu wengi kuwa na hamasa ya kukimbilia, kuwahi au kuwa wa kwanza kufanya jambo hilo ni lazima kuwe na utaratibu mahususi wa kufanya kitendo hicho ili kuondoa au kuepusha uwezekano wa watu wengi kupoteza maisha.

Usalama wa watu ni jambo la msingi ili kudhibiti uvamizi au kundi kubwa la watu kuvunja utaratibu tunashauri wanyama wanaosaidia kwenye kuchunga usalama na amani kama mbwa na farasi wakatumiwa pale inapobidi kuongeza nguvu.

Wakati mwingine tunaona kuwa kuna haja ya kuingiza suala la wanaoandaa kugharamia baadhi ya vitu kama magari ya uokoaji na kutoa huduma ya kwanza, kuweka vipaza sauti vya kutosha na video ili kusambaza ujumbe wao kwa watu na wafuasi wengi zaidi walio nje na ndani ya ukumbi au uwanja linapofanyika tukio hilo.

Pamoja na jitihada hizo, ni vyema pia kuwa na kikosi kikubwa cha polisi, polisi jamii na wanamgambo ili kusaidiana kuwahakikishia watu usalama wao na kudhibiti nidhamu wakati wote na kuepusha maafa.

Tunaona kuwa kilichotokea Moshi kinaweza kutokea popote, hivyo ni vyema kuchukua tahadhari na kuepusha maafa mengine makubwa yanayotokea kwa wakati mmoja na kukatisha uhai wa watu wengi.

Tunatoa tena pole kwa taifa ambalo limepoteza raia wake na kuwakumbusha kila mmoja kuwa hakuna sababu ya kulaumiana, bali tuviachie vyombo vya dola vifanye kazi yake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




### Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Siasa si uadui, zisitugawe uchaguzi mkuu Oktoba

**MWAKA** huu wa 2020 ni wa uchaguzi mkuu wa madiwani, wabunge na rais. Kama ilivyo kila unapofanyika uchaguzi huo, hamasa za kiasa huwa zinaongezeka kila kona ya nchi.

Hamasa hizo zinalenga kupata wanachama zaidi, kutokana na ukweli kwamba mtaji wa chama cha siasa chenye nguvu ni uimara wa wanachama wake unaounganishwa na umoja, maslahi na malengo yanayofanana.

Pamoja na kuwapo kwa hamasa za kuashiria uchaguzi huo, ipo haja kwa wanasiasa kuhimiza umoja kama taifa na kuepusha kuwagawa Watanzania kwa tofauti za itikadi za kisiasa.

Ninasema hivyo, kwa sababu kwenye mitandao ya kijamii, zimeanza kurushwa video zenye kauli tata za baadhi ya wanasiasa zenye viashiria vya kuwagawa Watanzania kwa misingi ya itikadi za kisiasa.

Watanzania ni vyema watakambua kuwa tofauti zao za itikadi za kisiasa ni sehemu tu ya kuchochea maendeleo ya nchi, wala siyo uadui hadi kufikia kuwaona wengine kama hawafai.

Katika uzoefu wa zaidi ya miaka 20 tangu serikali kuruhusu kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini, unatosha kuwafanya Watanzania kutambua uwapo wa mfumo huo na kuendelea kuwa wamoja.

Ikumbukwe, mfumo wa vyama vingi vya siasa ni hali ya kuwa na chama zaidi ya kimoja, katika nchi moja, lengo la kila kimoja ni kushika dola kwa njia halali kupitia sanduku la kura na pia kuleta ushindani kama chachu ya maendeleo. Hivyo, upinzani wa kisiasa siyo uadui kama ambavyo ndugu yangu Mbunge wetu wa Kigamboni, nakubaliana na wewe kwa asilimia 100 kwa 100. Tatizo ni kwamba siasa zimeingiliwa na maadui, na siyo kwamba siasa ni uadui. Kuna maadui wa kijamii wanapeleka uadui wao hadi ndani ya siasa. "Phenomena" hii iko ndani ya nyanja na fani zote nyingine... imekuwa ikitokea kwenye baadhi ya nchi zinazoendelea, lakini kuwa na vyama vingi vya siasa ni kuongeza wigo wa demokrasia kwa jamii husika.

Wanasiasa epukeni kauli tata bali walinde amani kwa kutambua kuwa siasa siyo uadui, hivyo zisiwagawe Watanzania, badala yake wapambane kwa nguvu ya hoja na kuacha hoja za nguvu, ambazo kimsingi hazifai.

Mwaka huu ni wa uchaguzi mkuu, siasa za visasi, kukomoana zisipewe nafasi bali zitumike kuunganisha Watanzania kwa kutambua kuwa Tanzania ni nchi yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa, ambao upo kisheria.

Wakati nchi inatarajia kufanya uchaguzi mkuu mwishoni mwa mwaka huu, ni vyema kutokuwapo na kauli za wanasiasa zenye lengo la kuwagawa Watanzania bali ni vyema kutambua kuwa wote ni wamoja.

Siasa zenye mwelekeo huu zimewahi kuleta maafa katika nchi mbalimbali barani Afrika, zikiwamo nchi jirani, kutokana na kujikita katika tofauti za itikadi za vyama pamoja na ukabila na ukanda.

Ni wazi kwamba katika nchi yenye mfumo wa siasa ya vyama vingi, huwa kuna tofauti kati ya wanasiasa wake, kwani wale wa upinzani hufanya kila njia kutafuta udhaifu wa chama kilichopo madarakani na kukosoa.

Katika mazingira hayo, hutumia kila kosa na udhaifu wa chama tawala kama njia ya kukishughulikia mbele ya wananchi ili kionekane kimeshindwa kutekeleza mambo kiliyoyaahidi kwenye ilani yake ya uchaguzi kwa wananchi.

Hata hivyo, ukosoaji wa aina hiyo wakati mwingine kusababishe baadhi ya kuanza kujengeana uhasama na kuchukiana.

Hilo linapaswa kuchukuliwa kama njia ya kujisahihisha na kurudi kwenye mstari badala ya wanasiasa kujikita kwenye uhasama, ikiwamo kutoleana kauli tata ambazo kimsingi hazina manufaa kwa maendeleo ya nchi yetu zaidi ya kusababisha migawanyiko.

Wakati vyama vya upinzani vikitumia udhaifu wa chama tawala kujijengea umaarufu kwa wananchi, wafuasi na wanachama wa chama hicho kinatakiwa kujenga hoja katika kujibu mapigo badala ya kutumia njia ambazo zinaweza kuibua vurugu.

Lakini wapo baadhi ya wapambe katika siasa pande hizi mbili, ambao wamekuwa mstari mbele kurushiana maneno makali kana kwamba siasa ni uadui na kumbe tatizo ni wao.

Watu wa aina hii, wanapaswa kukumbushwa kuwa siasa siyo ugomvi wala chuki, bali ni tofauti ya itikadi, mawazo au mtazamo, ingawa suala la utanzania na imoja wa kitaifa linabaki kuwa palepale bila kuvurugwa.

Umefika wakati sasa ionekane ni jambo la kawaida kuwa na itikadi tofauti za kisiasa na kuzingatia zaidi utetezi wa nchi, kwani katika nchi wapo ndugu na jamaa wenye itikadi tofauti za kisiasa.

Vijana wa vyama vya siasa ambao wamekuwa wakilalamikiwa kwamba wanajihusisha na vitendo vya vurugu katika mikutano ya siasa, ni vyema wasipewe nafasi inayoweza kutenganisha Watanzania hususan kipindi hiki kuelekea uchaguzi mkuu.

# Watu 54,554 wakosa vitambulisho wilayani

Na Lilian Lugakingira, MISSENYI

WAKAZI 54,554 wilayani Missenyi mkoani Kagera wameshindwa kusajili laini zao za simu kwa alama za vidole kutokana na kutopata namba au kitambulisho cha Taifa kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), kutokana na taarifa zao kuwa na utata.

Katika taarifa iliyosomwa na Ofisa Mipango wilayani Missenyi, Albert Msemo, kwa niaba ya ofisi ya mkuu wa wilaya wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, ilisema mpaka sasa wananchi waliopata namba za kitambulisho cha taifa ni 18,388, kati ya 79,107 waliosajiliwa.

"Makadirio ya uandikishaji yalikuwa watu 88,889, na waliobaki bila kusajiliwa ni 12,060 tu," alisema.

Alitaja kasoro zilizosababisha wananchi hao wasipewe namba kutoka Nida kuwa baadhi waombaji fomu zao kutokamilika na shaka ya uraia kutokana na wilaya hiyo kuwa mpakani.

Aidha, alitaja changamoto zinazolikabili zoezi hilo ni mwingiliano mkubwa wa watu wakiwamo raia kutoka nchi jirani hasa katika kata za Nsunga, Minziro, Mtukula, Kakunyu na Kashenye, na wananchi wengi kujitokeza siku za mwisho za kusajiliwa na kusababisha msongamano mkubwa.

"Changamoto nyingine ni kutokuwapo kwa mtandao wa Nida katika Wilaya ya Missenyi, hali inayowalazimu kusafiri kwenda Bukoba Manispaa ili kujua maombi ya wananchi husika yamefikia hatua gani hasa wenye uhitaji wa maombi ya haraka, na kutokujibiwa kwa bajeti na mpango kazi wa kushughulikia maombi yenye utata wa uraia," alisema.

Baadhi ya madiwani walihudhuria kikao hicho akiwamo Ibrahimu Kaislanga wa Mabale wameiomba serikali kupitia Mamlaka ya Mawasliano Tanzania (TCRA) kusitisha zoezi la kuzima laini za simu za watu ambao hawajakamilisha usajili, kwani wamekuwa wakishinda kwenye ofisi za Nida kufuatilia taarifa zao bila mafanikio.

"Walikuwa wanakuja kama zimamoto, wanakimbia kimbia mara wakati mwingine saa saba wanafunga, na fomu nyingine walizitupatupa ovyo, kwa kweli hawakutendea wananchi haki," alisema diwani huyo.

# Ajali ya gari, pikipiki yaua sita

Na Romana Mallya

WATU sita wamefariki dunia na watatu kujeruhiwa katika ajali iliyohusisha gari aina ya Toyota RAV4 na pikipiki eneo la JKT Mbuyuni, jijini Dar es Salaam.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kinondoni, Musa Twaibu alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa gari hilo ni lenye namba za usajili T 835 BLP liliigonga pikipiki na kisha kukimbia na kwenda kupata ajali mbele.

Kamanda Twaibu alisema watu hao walifariki jana saa nane usiku baada ya gari hilo lililokuwa na watu saba kupata ajali wakati wakikimbizwa na waendesha pikipiki lilipotokea tukio la mwenzao kugongwa.

"Dereva wa RAV4 alikuwa akitokea Tegeta kwenda Mbuyuni na njiani aligonga pikipiki ambayo ilikuwa na abiria na kuwasababishia majeraha. Baada ya ajali hii, dereva wa gari alikimbia na ndipo madereva wa bodaboda walipoanza kulifukuza gari hadi lilipopata ajali JKT Mbuyuni," alisema.

Kamanda alisema katika ajali hiyo, watu sita walifariki dunia wakiwamo wanne waliokufa papo hapo.

Alisema majeruhi watatu ambao wawili ni wa pikipiki wanaendelea na matibabu.

Twaibu alisema majina ya waliofariki dunia bado hayajafahamika na wote wanakadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 20 hadi 30.



Fundi akiandaa matofali, kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa majengo ya zahanati ya kijiji cha Bukimu, Musoma Vijijini mkoani Mara juzi. Mkakati wa serikali ni kila kijiji kuwa na zahanati, ili kusogeza huduma za afya karibu na wananchi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Bunge laitaka serikali kutoingilia mtaalamu mradi mkubwa miji

Na Godfrey Mushi, DODOMA

BUNGE limeishauri serikali isiingilie majukumu ya kitaalamu ya mtaalamu mshauri atakayeajiriwa kusimamia mradi mkubwa wa miji ya kimkakati Tanzania (TSCP) hasa kwa vitega uchumi vinavyojengwa katika Jiji la Dodoma.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Jasson Rweikiza, alisema kamati yake inalishauri Bunge kuitaka serikali kuhakikisha uongozi wa Jiji la Dodoma unaendesha vitega uchumi hivyo kwa ufanisi na faida.

Rweikiza aliwasilisha pendekezo hilo jana, wakati akisoma Bungeni taarifa ya shughuli za kamati hiyo kwa kipindi cha kuanzia Februari 2019 hadi Januari 2020.

"Kwa kuwa miradi ya vitega uchumi vya soko la kisasa, stendi kuu ya mabasi, kituo cha mapumziko na kituo cha maegesho ya malori, inayotekelezwa kupitia Mpango wa Miji ya Kimkakati (TSCP) katika Jiji la Dodoma imegharimu fedha nyingi ambazo ni mkopo," alieleza.

"Na kwa kuwa miradi hiyo inahitaji kusimamiwa vizuri ili iwe na tija kwa kutoa huduma iliyokusudiwa kwa jamii, kuonyesha thamani halisi ya fedha na kuzalisha fedha ambazo zitachangia kulipa mkopo na kufanya maendeleo mengine.

Aliongeza: "Kamati inalishauri Bunge kuitaka serikali kuhakikisha uongozi wa Jiji la Dodoma unaendesha vitega uchumi hivyo kwa ufanisi na faida kwa kuajiri na kuruhusu mtaalamu mshauri atekeleze majukumu yake ya kitaalamu kwa mujibu wa makubaliano bila kuingiliwa."

Miradi ya ujenzi wa soko, kituo cha mabasi na mtandao wa barabara zinazoingia maeneo hayo na eneo la mapumziko la Chinangali inatekelezwa chini ya Mpango wa Miji ya Kimkakati kwa gharama ya Sh. bilioni 41.5.

Aidha, Rweikiza alisema mbali na Dodoma, miradi mingine ya kimkakati imo ile inayotekelezwa katika Manispaa ya Mtwara-Mikindani ikihusisha uboreshaji wa miundombinu ya huduma za miji na uimarishaji wa mifumo ya halmashauri katika kutoa huduma bora kwa jamii.

Katika mkoa huo wa Mtwara, barabara zenye urefu wa kilomita 15.78 zimejengwa kwa kiwango cha lami kwa gharama ya Sh. bilioni 24.01. Barabara hizo ni Bandari (kilomita 2.75), Zambia (kilomita 3.75), Mikindani (kilomita 1.9), Chuno (kilomita 5.78) na Kunambi (kilomita 1.6).

Aidha, ujenzi wa dampo la kisasa na vizimba 25 vya kukusanyia taka pamoja na ununuzi wa mitambo na vifaa vya kusafirishia taka kutoka kwenye vizimba hadi dampo viligharimu jumla ya Sh. bilioni 4.96.

Kutokana na ufanisi katika utekelezaji wa awamu ya kwanza ya miradi hiyo, Manispaa ya Mtwara Mikindani ilipata nyongeza ya Sh. bilioni 8.8 ili kujenga mifereji ya maji yenye urefu wa kilomita 7.4, maegesho ya magari katika dampo, mizani ya kupimia taka na uwekaji wa taa za nishati ya jua katika barabara ya Chuno.

Kadhalika, Sh. bilioni 21.68 zitatumika kujenga barabara (kilomita 4.1), mfereji wa kupeleka maji baharini (kilomita 3.4), kuboresha maeneo ya wazi, maduka makubwa, stendi ya daladala ya Mikindani, ujenzi wa soko la kisasa la Chuno, kazi zitakazotekele-

# Polisi kuwashughulikia watakaovunja sheria

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imesema Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama limejipanga vizuri kudhibiti vitendo mbalimbali vya uvunjaji wa sheria ikiwamo fujo au aina yoyote ya ukosefu wa amani vitakavyosababisha wananchi kushindwa kushiriki katika shughuli zao za kila siku, ikiwamo michakato ya uchaguzi mbalimbali zinazofanyika nchini.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mtwara Mjini (CUF), Maftaha Nachuma, ambaye alihoji serikali inahakikishaje amani na utulivu katika uchaguzi mbalimbali nchini vinakuwapo.

Akijibu swali hilo, Masauni alisema jukumu la serikali kuhakikisha kuwa amani na utulivu vinatamalaki nchini wakati wote bila kujali nyakati au majira mbalimbali katika mwaka.

"Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama limejipanga vizuri kudhibiti vitendo mbalimbali vya uvunjaji wa sheria ikiwamo fujo au aina yoyote ya ukosefu wa amani vinavyoweza kusababisha wananchi kushindwa kushiriki katika shughuli zao za kila siku, ikiwamo kushiriki michakato ya chaguzi mbalimbali zinazofanyika nchini," alisema.

Alieleza kuwa serikali kupitia Jeshi la Polisi inaendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa askari wake ya ukakamavu, upelelezi na kuongeza vifaa vya kutendea kazi ili kuwajengea uwezo na weledi mkubwa wa kuweza kuzuia na kukabiliana na vitendo kama hivyo vinavyojitokeza nyakati za uchaguzi.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alisema hivi sasa Mtwara Mikindani kumekuwa na baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa wilaya na mkoa wanaratibu vikundi mbalimbali kwa ajili ya uchaguzi na kuhoji kama serikali ipo tayari kwenda kuchukua ushahidi wake.

"Kuna na baadhi ya viongozi wanatumia askari polisi kuwafanyia hujuma upinzani usiku na kuwakamata na kuwakweka ndani ni sababu wananadi vyama vya upinzani, Je, ni lini serikali itaongozana nami kwenda kuwaonyesha ushahidi," alisema.

Akijibu swali hilo, Masauni alisema serikali itafanyia kazi madai hayo.



Wasichana waliokimbia ukeketaji ambao sasa wanalelewa na nyumba salama ya shirika lisilo la kiserikali la Hope for Girls and Women Tanzania la mjini Mugumu, Serengeti mkoani Mara, wakifuatilia uzinduzi wa Wiki ya Sheria mjini humo juzi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

## Serikali yatoa msimamo wabakaji kuhasiwa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

BUNGE limeelezwa kuwa kuruhusu adhabu ya kuhasiwa kwa watuhumiwa wa makosa ya ubakaji na ulawiti kwa watoto na wanawake ni kuvunja Katiba ya nchi.

Serikali imesema sheria zinazotoa adhabu kwa makosa hayo zinajitosheleza.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Mwanasheria Mkuu wa Serikali Prof. Adelardus Kilangi, alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Zainab Katimba.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema kuna tatizo kubwa la ukatili dhidi ya wanawake na watoto hasa vitendo vya ubakaji dhidi ya makundi hayo.

"Sisi tunafahamu kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inataka kuwahakikishia usalama Watanzania wote na kwenye makosa ya ubakaji kama ilivyoainishwa kwenye kifungu cha tano cha Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya mwaka 1998, ambayo imeenda kufanya marekebisho ya kifungu cha 130 cha sheria ya adhabu ya ubakaji," alisema.

Alifafanua kuwa kigezo au masharti ya kuthibitisha kosa la ubakaji ni mpaka aliyebakwa athibitishe kwamba kulikuwa na kuingiliwa na mazingira hayo.

"Ni magumu sana katika utaratibu wa kawaida kuthibitisha kwamba mtu amekuingilia hasa kwa watoto. Je, serikali haioni katika mazingira haya kwamba kufanyike marekebisho ya sheria ili vigezo vya kuthibitisha au kuthibitisha kosa la ubakaji, ipunguzwe kiwango chake ili kusiwe na haja ya kufanya hivyo sababu watoto siyo rahisi kwao kuweza kuthibitisha jambo kama hilo na mazingira yaangaliwe ili kuweza kutoa haki?" Alihoji.

Mbunge huyo pia alihoji serikali haioni kwamba kuna haja ya kuongeza adhabu kwa wale watakaothibitika wamefanya kosa la ubakaji ili adhabu yao iwe kali.

"Kwa mfano, serikali haioni kwenye kosa la ubakaji, mbakaji apewe adhabu ya kuhasiwa ili asije akarudia tena kosa kama hilo ambalo linaleta ukatili mkubwa kwa wanawake na watoto kutokana na kuwaathiri?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema kuruhusu adhabu ya kuhasiwa kwa watuhumiwa wa ubakaji na ulawiti kwa watoto na wanawake ni kuvunja Katiba ya nchi ibara ya 13(6).

Alibainisha ibara hiyo inaeleza kwamba ni marufuku kwa mtu kuteswa, kuadhibiwa kwa kinyama au kupewa adhabu zinazomdhalilisha, hivyo pendekezo hilo likichukuliwa ni kuvunjwa kwa katiba.

Awali, akijibu maswali ya mbunge huyo, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Augustine Mahiga, alisema wameondoa baadhi ya vigezo vilivyokuwapo hasa watoto kutoa ushahidi wenyewe na kuachia mahakama uamuzi wa busara na wa kitaalamu kutoa ushuhuda huo kama kitendo hicho kimetokea.

"Kwa sasa, kuna mfumo wa kutazama na kuboresha mfumo mzima wa kesi za jinai likiwamo suala la ubakaji na kama itatoa mapendekezo yatafuatana na adhabu, lakini niwaambie kweli kwamba kwa makosa haya adhabu ambazo zipo mpaka sasa ni kali na inafika mpaka miaka 30," alisema.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema tatizo ni malezi na hata zikiwapo sheria kali kiasi gani, matatizo ya ubakaji nchini hayataisha.

Aliwataka wazazi, walezi na jamii kutimiza wajibu wa malezi na ulinzi wa watoto huku akitolea mfano kuwa kuna watoto wanabakwa miezi mitatau bila mzazi kujua, hivyo kuwataka wawakague, wawaulize na kuwafuatilia ili waeleze matatizo wanayopata.

## Mtaalamu aeleza sababu ongezeko maradhi saratani

INATOKA UK 2

wa Taifa wa Damu Salama (NBTS), Mashauri aliwaomba Watanzania wajitokeze kuchangia kwa sababu upo uhitaji mkubwa kwa wagonjwa wa saratani.

Alisema ili kuepuka ugonjwa huo watu wanatakiwa kupata chanzo ambazo mara kwa mara serikali imekuwa ikizisisitiza.

"Ninaomba makundi yote katika jamii wajue kuwa hali ya saratani kwa sasa inatisha wagonjwa ni wengi. Vipo visababishi vya aina mbalimbali zikiwamo dawa tunazotumia, vyakula ambavyo siyo vya asili na kutofanya mazoezi," alisema.

Pia Mashauri alisema gharama ya matibabu ya ugonjwa huo ni kubwa ndani na nje ya nchi.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Saratani katika hospitali hiyo, Aleesha Adatia, alisema mtu anapopata saratani si mwisho wa maisha na kwamba atakapopata matibabu mapema, hurudi katika hali yake ya kawaida na kuendelea na shughuli zake za kila siku.

**"Ninaomba makundi yote katika jamii wajue kuwa hali ya saratani kwa sasa inatisha wagonjwa ni wengi. Vipo visababishi vya aina mbalimbali zikiwamo dawa tunazotumia, vyakula ambavyo siyo vya asili...**

HABARI KITAIFA

# Vituo 50 kutoa elimu ya sheria kwa umma Lindi

**Na Said Hamdani, LINDI**

ZAIDI ya vituo 50 vimetengwa mkoani Lindi kwa ajili ya kuelimisha wananchi kuhusiana na masuala mbalimbali yanayohusu sheria kwa umma, ili kuwawezesha kufahamu namna ya kufungua mashauri mahakamani, pale wanapokuwa na tatizo la kisheria kwa lengo la kupata haki zao.

Hayo yameelezwa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Mkoa huo, Elimo Massawe, alipokuwa anazungumza na Nipashe, baada ya kumalizika kwa maandamano kuelekea Wiki ya Sheria nchinbi.

Amesema katika maaadhimisho Wiki ya Sheria nchini, zaidi ya vituo 50 vikiwamo vinavyohamishika vimetengwa mkoani Lindi,huku akieleza wana makundi ya kutosha wakaofanya kazi ya utoaji elimu katika vituo vyote vilivyotengwa.

Hakimu Mkazi huyo Mfawidhi alitaja maeneo yatakayotumika kwa kazi hiyo ni taasisi za umma, vituo vya mabasi na yale yanayotumika kibiashara.

Masawe alisema kazi ya uelimishaji itafanywa na makundi mbalimbali ya watumishi na wasio watumishi, wakiwemo mahakimu, wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria ngazi ya mkoa wa Lindi, watumishi wasaidizi wa Mahakama na Jeshi la Polisi.

Wengine ni Magereza, Uhamiaji, Takukuru, Baraza la Aridhi, TRA, Chama cha Msaada wa Kisheria Mkoa (LIWOPAC), mabaraza ya usuluhishi na chama cha wafanyabiashara.

"Kwa hapa mjini Lindi, elimu hii itatolewa maeneo ya familia za askari Magereza, Polisi, soko kuu na lile la Sabasaba," alisema Hakimu Massawe.

Aidha, aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kwenye vituo hivyo ili kupata elimu itakayowasaidia kupata uwelewa kazi zinazofanywa na mahakama pamoja na jinsi ya kufungua mashtaka wanapokuwa na tatizo.

**Masawe alisema kazi ya uelimishaji itafanywa na makundi mbalimbali ya watumishi na wasio watumishi, wakiwemo mahakimu, wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria ngazi ya mkoa wa Lindi, watumishi wasaidizi wa Mahakama na Jeshi la Polisi.**

# Onyo kuingiza mayai nje kwa kutumia njia za panya

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WAFANYABIASHARA wa mayai wilayani Kahama Mkoa wa Shinyanga, wametakiwa kuacha tabia ya kuendelea kuagiza na kuingiza mayai kutoka nchi za jirani kwa njia za panya ili kudhibiti ugonjwa wa mafua ya ndege ambao unaweza kujitokea wakati wanapoingiza mayai hayo.

Onyo hilo lilitolewa na Ofisa Mifugo wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Dk. Damian Kilyenyi wakati akizungumza na wanahabari, na kueleza kuwa asilimia kubwa ya mayai yanaingizwa kwa njia za panya kutoka Rwanda, Uganda na Burundi.

Aidha, Dk. Kilyenyi alisema mwaka jana walikamata gari likiwa na trei 700 za mayai kutoka (mayai 21,000) yenye thamani ya Sh. milioni 4.9 mali ya Regina Ayinkamiyi, raia wa Rwanda ambaye alitozwa faini ya Sh. 300,000 na mayai hayo kuteketezwa.

Alisema lengo la kuzuia mayai kutoka nje kuingia nchini ni kupambana na ugonjwa wa mafua ya ndege, ambayo yanaweza kujitokeza ikiwamo kuwalisha wateja mayai ambayo asilimia kubwa yanakuwa mabovu.

"Sheria ya Chakula na Dawa ya mwaka 2018 inasema chakula chochote kile kinachosafirishwa kikakosa nyaraka zozote, hakifai kwa matumizi ya binadamu...mayai hayo unakuta yanazaidi ya wiki mmoja, wakati mayai yanayotakiwa kutumiwa ni yale ya ndani ya wiki tangu kutagwa," alisema. Hata hivyo, alisema wafanyabiashara wanaagiza mayai hayo na kuyapitisha kwa njia za panya kutokana na kuuziwa kwa bei ndogo, na kuuza kwa bei kubwa kwa tamaa za kupata faida kubwa, huku wakijua wanahatarisha afya za watumiaji.

Pia aliwataka kuacha tabia ya kuendelea kuingiza mayai hayo kienyeji kwa kushirikiana na wafanyabiashara kutoka nchi za jirani ili kutoendelea kuingia hasara, na badala yake waagize mayai kutoka mikoa inayofunga kuku kwa wingi nchini.



Mtoto akipita eneo lenye maji machafu la Mwananyamala Sokoni, jijini Dar es Salaam, bila kuvaa viatu, kitendo kinachoweza kuhatarisha usalama wa afya yake. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ngariba Tarime wapewa mikopo kuacha kukeketa

**Na Christina Haule, MOROGORO**

JUMLA ya mangariba 10 wilayani Tarime mkoani Mara, wamepatiwa mikopo ya jumla ya Sh. milioni 22 katika kipindi cha mwaka 2018 hadi 2020, ili kufanya ujasiriamali na kuacha vitendo vya ukeketaji kwa wasichana vinayoshika kasi katika maeneo mengi ya Tanzania kwa sasa.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wilayani Tarime, Ocheng Wayoga, alisema wakati wa majadiliano ya bajeti ya mrengo wa kijinsia kuwa vitendo vya ukeketaji wasichana vinavyofanywa na mangariba mara nyingi vimeonekana kuwa vinatokana na umaskini kufuatia ngariba mmoja kupewa Sh. 5,000 kwa kila msichana atayemkeketa.

Wayoga alisema baada ya kuona hivyo, wakaamua kuweka hamasa kwa mangariba hao ili waachane na vitendo hivyo, ambavyo ni ukatili wa kijinsia vinavyoleta athari mbalimbali kwa afya za wanawake ikiwamo kupata ugumu wakati wa kuzaa, kumwaga damu nyingi na pengine kupoteza maisha.

Aidha, Wayoga alisema katika kipindi cha mwaka 2018/19 kupitia bajeti ya halmashauri waliweza kutoa mkopo wa Sh. milioni 4 kwa kikundi kimoja cha mangariba watano ambapo walifanya biashara na kurejesha bila riba.

Alisema mwaka 2019/20 pia walitoa mkopo wa Sh. milioni 10 kwa kikundi cha kwanza na kikundi kipya cha mangariba watano kilipewa mkopo wa jumla ya Sh. milioni 8.

Alisema mafanikio hayo ya kuwapata mangariba ni juhudi za kielimu zilizoletwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) tangu mwaka 2000 na kufanya hata madiwani, viongozi wa dini na viongozi mbalimbali kuelimika na kuweka mikakati ya kupunguza ukatili huo wa kijinsia kwa wanawake.

Wayoga alisema juhudi za TGNP pia zilifanya wadau wa masuala ya kupinga ukatili wa kijinsia kutoa Kenya ambako ni jirani na Mkoa wa Mara kuungana na kuweka mikakati ya kudhibiti ukeketaji Tanzania na Kenya.

"Tarime na Kenya ni jirani, hivyo wapo pia Wakurya Kenya ambao nao wanaendeleza mila na tamaduni zilizopitwa na wakati na sasa wanaona mwisho wao unafika," alisema Wayoga.

Naye Ofisa Programu Mwandamizi kutoka TGNP, Deogratiaus Temba, alisema wanaendelea kutoa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia ikiwamo ukeketaji kwa watoto, wasichana na wanawake katika halmashauri 22 wanazotoa elimu kwa sasa ili kuhakikisha suala la ukeketaji linabaki kuwa historia.

Temba alisema pia wanatoa elimu kwa wanaume na kuwafanya kuwajali wanawake, kuona umuhimu wao kwa kuwathamini nyakati zote kwa kuachana na dhana na mila zilizopitwa na wakati.

Alisema wameanzisha programu ya kuelimisha wazee wa mila, watoto wa kiume wa shule za msingi na sekondari sambamba na kufungua vilabu vya jinsia shuleni na kuhakikisha vyuo vikuu wanajadili masuala ya kijinsia ili kuwafanya wanaume kuelimika na kuacha kuhalalisha vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa kuona lazima kuwaoa wanawake waliokeketwa.

## Majosho 161 kukarabatiwa

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imesema katika mwaka wa fedha 2019/20, imetenga fedha kwa ajili ya kukarabati majosho 161 nchi nzima ili kudhibiti magonjwa yanayoenezwa na kupe, mbung'o na wadudu wengine.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Abdallah Ulega, alisema hayo alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Same Magharibi (CCM), Dk. Mathayo David.

Katika swali lake, Mathayo alisema serikali iliahidi katika bajeti ya Mwaka 2012/13 kujenga malambo, majosho na kisima kirefu kwa ajili ya wananchi wafugaji wa Kata ya Ruvu Jimbo la Same Magharibi, na kuhoji lini ahadi hiyo itakamilishwa.

Akijibu, Ulega alisema wizara hiyo kupitia bajeti yake pamoja na program mbalimbali imeendelea kukarabati na kujenga miundombinu ya maji ya mifugo katika maeneo mengi ya ufugaji hapa nchini ili kupunguza tatizo la maji hasa wakati wa kiangazi kikali.

"Katika Mwaka huu wa Fedha 2019/20, wizara imetenga fedha jumla ya Sh. milioni 700 kwa ajili ya kujenga visima 10 na kukarabati mabwawa 10 katika mikoa Kumi Tanzania Bara," alisema.

Alibainisha kuwa katika utekelezaji wa mpango huo, kisima kimoja kinatarajiwa kuchimbwa katika Wilaya ya Same, hususan Kata ya Ruvu ili wafugaji waweze kupata maji kwa ajili ya mifugo yao.

"Katika mwaka huu wa fedha 2019/20 wizara imetenga fedha kwa ajili ya kukarabati majosho 161 nchi nzima ili kudhibiti magonjwa yanayoenezwa na kupe, mbung'o na wadudu wengine. Mpaka sasa, majosho 46 yamekamilika, majosho 95 ukarabati unaendelea na majosho 20 ukarabati bado haujaanza," alisema.

Hata hivyo, alisema wizara imejenga josho moja la kisasa wilayani Bariadi na pia Halmashauri mbalimbali zinakarabati majosho 288 na zinajenga majosho mapya 84.

"Kwa Halmashauri ya Same, josho moja linakarabatiwa na wizara katika Kata ya Ruvu-Muungano na matatu yanakaribatiwa na halmashauri yaliyopo kwenye vijiji vya Mwembe, Mbangalala na Mkonga," alisema.

Alisema mikakati ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya mifugo inaendelea kadri fedha inavyopatikana.

"Napenda kuchukua fursa hii kutoa rai kwa halmashauri zote nchini ikiwamo Halmashauri ya Same kutenga fedha kwa ajili ya kujenga, kukarabati na kuendeleza miundombinu ya mifugo katika maeneo yao kwa kutumia fedha zinazopatikana kutokana na makusanyo ama tozo za rasilimali za mifugo," alisema.



# Zitto ataka maofisa Uhamiaji wa kutosha kwenye balozi nje



MBUNGE wa Kigoma Mjini (ACT-Wazalendo), Zitto Kabwe, ameitaka serikali kupeleka maofisa uhamiaji wa kutosha kuhudumu kwenye balozi zilizopo nje ili kutoa huduma bora kwa raia wa Tanzania wanaoishi nje ya nchi.

Katika swali lake, ambalo liliulizwa kwa niaba na Mbunge wa Tarime Vijijini (Chadema), John Heche, alisema Watanzania wanaoishi nje ya nchi wanapata changamoto za huduma za uhamiaji kutokana na balozi takribani zote kutokuwa na maofisa uhamiaji.

"Je, ni lini serikali itapeleka maofisa Uhamiaji kuhudumu kwenye balozi zetu ili kuwezesha huduma bora kwa raia wa Tanzania kwenye nchi hizo?" Alihoji.

Akijibu, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuph Masauni, alisema wizara hiyo kupitia Idara ya Uhamiaji inawajibika kuhakikisha Watanzania wanaoishi nje ya nchi wanapata huduma bora za uhamiaji wanapofika kwenye balozi nje ya nchi.

Alifafanua kuwa maofisa hao waliokuwa wanatoa huduma za uhamiaji katika balozi ama wamestaafu au wamemaliza muda wao wa kuhudumu kwenye balozi walizokuwa na wamerejea nchini.

"Ili kuhakikisha huduma bora za uhamiaji zinaendelea kutolewa kwa raia wa Tanzania wanaoishi nje ya nchi, tayari serikali imewateua maofisa watano kutoka Idara ya Uhamiaji ambao wameshapatiwa mafunzo ya kuhudumu katika Balozi," alisema.

Kwa mujibu wa Masauni, Idara ya uhamiaji kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki wako katika hatua za mwisho za kukamilisha taratibu za kuwapeleka maofisa hao kwenda kuhudumu katika balozi walizopangiwa.

Katika swali la nyongeza, Heche alisema licha ya maofisa watano kuteuliwa kwa ajili ya kwenda kuhudumu nje kwenye balozi, inafahamika kuwa katika serikali ya awamu ya tano wengi wamerejeshwa nchini kwa alichodai kuwa ni hofu za Chama Cha Mapinduzi(CCM).

"Sasa maofisa watano tu hamuoni kwamba mnawapa Watanzania matatizo ya kupata huduma za msingi?" Alihoji.

Heche alisema serikali ilisitisha matumizi ya hati za kusafiria za zamani, jambo lililosababisha watu wengi wanaoishia nje ya nchi kuwa una uhitaji.

"Lini serikali itahakikisha Watanzania wanaoishi nje wanapata kwa wakati ili kuondokana na changamoto ya kurudishwa nchini?" Alihoji zaidi.

Akijibu, Masauni alisema serikali ya CCM haina hofu, na kwamba kilichopo ni suala la utaratibu tu, hivyo kwa kutambua upungufu huo ndio maana wengine watano wanapelekewa huko.

"Kutokuwa na maofisa uhamiaji kila balozi haimaanishi kuwa Watanzania walipo nje ya nchi wanakosa huduma, tuna mfumo wa uhamiaji mtandao ambao umarahishia kutoa huduma na haihitaji wananchi kwenda ofisini wanajaza fomu mitandaoni, maafisa wetu wameshapata elimu namna ya kuutumia hivyo wanapata huduma nzuri," alisema.

Masauni alisisitiza kuwa uchache huo hauna madhara.

# Serikali yafafanua usafirishaji mkaa nje



BUNGE limeelezwa kwa sasa serikali haisafirishi mkaa unaotokana na miti kwenda nje ya nchi.

Hayo yalielezwa jana Bungeni na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Ileje (CCM), Janet Mbene.

Katika swali lake, Mbene alisema uchomaji wa mkaa kwa kiasi kikubwa unatumia miti ya asili pamoja na mapori ya akiba, ukataji wa miti hauendi sambamba na upandaji wa miti na hii ina athari kubwa sana kwenye mazingira ikiwamo kupungua kwa mvua na kukauka kwa vyanzo vya maji.

"Je, ni lini serikali itaanza kutoza ada kwa mkaa unaosafirishwa nchi za nje ili iweze kurejesha mazingira katika hali yake?" Alihoji.

Akijibu, Sima alisema biashara ya mkaa inafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Misitu ya Mwaka 2002, Kanuni za mwaka 2004 na miongozo mbalimbali.

Aidha, alisema usafirishaji wa mkaa nje ya nchi umezuiliwa kwa mujibu wa kifungu namba 16 cha sheria inayozuia usafirishaji wa baadhi ya bidhaa nje ya nchi pamoja na makatazo mengine.

"Vilevile, Tangazo la Serikali namba 417 la tarehe 24/05/2019 kifungu Na. 21 - (1) limetoa zuio kwa mtu yeyote kusafirisha mkaa kwenda nje ya nchi isipokuwa mkaa mbadala (charcoal briquettes) na kwa kibali maalumu kutoka kwa waziri mwenye dhamana," alisema.

Alikiri kuwa uchomaji wa mkaa utokanao na miti kwa kiasi kikubwa unatumia miti ya asili pamoja na mapori ya akiba na ni dhahiri, ukataji wa miti hauendi sambamba na upandaji wa miti na ina athari kubwa sana kwenye mazingira ikiwamo kuendelea kupotea kwa bioanuai, kupungua kwa mvua na kukauka kwa vyanzo vya maji.

"Napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa kwa sasa serikali haisafirishi mkaa unaotokana na miti kwenda nje ya nchi kama nilivyotoa ufafanuzi hapo juu," alisema.

Alibainisha kuwa gharama za kurejesha au kuongoa maeneo yaliyoharibika kutokana na shughuli za kibinadamu ukiwamo mkaa, zitatokana na mapato yanayopatikana kwa kupitia tozo mbalimbali zilizoainishwa kwenye Sheria ya Misitu ya Mwaka 2002 ikiwapo asilimia tano ya ushuru wa halmashauri inayotozwa kwa wafanyabiashara wa mazao ya misitu.

Aidha, alisema tozo nyingine zinatokana na tozo za ukaguzi wa biashara ya mkaa unaotokana na mabaki ya miti au mimea ambao unaruhusiwa kwenda nje ya nchi.




Habari na Augusta Njoji

## Sita wajitokeza uenyekiti UWT

**Na Allan Isack, SIMANJIRO**

WANACHAMA sita wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wamejitokeza kuchukua fomu za kugombea nafasi ya uenyekiti wa UWT, wilayani humo.

Uchaguzi huo ni wa kuziba nafasi ya aliyekuwa Mwenyekiti wa umoja huo, Naitapuaki Tukai, baada ya kuteuliwa kuwa Katibu wa UWT wa Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro Agosti Mosi, 2019.

Katibu wa UWT Wilaya ya Simanjiro, Zariha Mwinyi, alisema juzi kuwa wanachama sita wameshajitokeza katika kinyang'anyiro hicho.

Mwinyi aliwataja wanachama waliochukua fomu ni Asha Middle, Scolah Saitabau na Khadija Abraham. Wengine ni Agnes Sanago, Sinyati Letekani na Rehema Alabara.

"Wanachama hawa watajadiliwa na Kamati ya Siasa ya CCM ya Wilaya kisha Halmashauri ya CCM ya Mkoa na yatateuliwa majina matatu yatakayopigiwa kura," alisema.

Alisema wanatarajia uchaguzi huo, utafanyika Mji Mdogo wa Orkesumet Februari mwaka huu, baada ya vikao vya uteuzi kufanyika rasmi.

Mmoja kati ya waliochukua fomu za kugombea nafasi hiyo, Asha Middle alisema ameamua kutimiza haki yake ya kikatiba.

Aidha, alisema amegombea nafasi hiyo, kwa kuwa ana nia na uwezo wa kuwaongoza wanawake hao, kwa sababu ameona kuna umuhimu wa kuitumikia jumuiya hiyo.

**"Wanachama hawa watajadiliwa na Kamati ya Siasa ya CCM ya Wilaya kisha Halmashauri ya CCM ya Mkoa na yatateuliwa majina matatu yatakayopigiwa kura," alisema.**

# Mvua yakosesha makazi kaya 91

**Na Jaliwason Jasson, MANYARA**

KAYA 91 katika vijiji viwili vya Bassotu na Diling'ang' hazina makazi ya kuishi baada ya mvua kujaza Ziwa Bassotu na maji kufurika na kusomba makazi ya wananchi.

Licha ya uharibifu huo, mvua zinazoendelea kunyesha zimekata mawasiliano kati ya Wilaya ya Hanang' na Wilaya ya Mbulu.

Hayo yalisemwa na wananchi wa vijiji hivyo wakati wakizungumza na Nipashe kuhusu athari walizopata, baada ya kunyesha kwa mvua hiyo.

Akizungumzia madhara ya mvua hiyo, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Bassotu Elizabeth Issallo, alisema barabara ya Hanang' kwenda Mbulu ilijaa maji hivyo imekata mawasiliano kati ya wilaya hizo.

Alisema madhara hayo yamesababisha na kuongezeka kwa nauli ya usafiri kuzunguka Hydom kwenda Dareda kiasi cha Sh. 12,000 badala ya Sh. 3,000.

Aidha, alisema kaya 91 hazina makazi ya kuishi na zimehifadhiwa kwa ndugu jamaa na marafiki na zingine zimeamua kutafuta makazi ya kupanga.

Issallo alisema usalama wa watoto siyo mzuri kwa kuwa mazingira ya kwenda shule ni magumu, ingawa wamewalazimisha waende ng'ambo ya pili ya shule.

Aliongeza kuwa kutokana na kukatika kwa mawasiliano hayo, wananchi wameanza kulima kutengeneza mbadala wa mahali pa kupita wakati wakisubiri serikali kufanya marekebisho ya barabara hiyo.

"Miongoni mwa wananchi waliosombewa makazi yao, awali tuliwahi kuliwaambia wahame wakagoma wengine walihama wenyewe kwa kuwa maeneo haya ni hatarishi," alisema Issallo.

Diwani wa Bassotu, Samwel Qawoga, alithibitisha kuwa wananchi hao, wameathirika, na mvua hizo zimekata mawasiliano kati ya Kata ya Katesh na Mkoa wa Singida.

Alisema chanzo cha mafuriko hayo, ni kuungana kwa Ziwa Bassotu na Ziwa la chumvi la Gendabi.

Mmoja wa waathirika, Thomas Sipran, alisema amepata athari ya vyoo kusombwa na mvua na wanakunywa maji yaliyochanganyikana na ya mvua, ziwa na vyoo. Alisema kama serikali haitachukua hatua za haraka, uwezekano wa watu kupata kipindupindu ni mkubwa, hivyo ameiomba iwasaidie.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Paul Kasabago, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara, alisema amefunga barabara hiyo isitumike mpaka serikali itakapojiridhisha kuwa kuna usalama na mawasiliano yamerejea.

Kasabago alisema barabara hiyo, kwa sasa ni hatarishi, hivyo haitakiwi kutumika na amewaagiza viongozi wa kata na Mkuu wa Kituo cha Polisi cha Bassotu kuisimamia barabara hiyo, isitumike mpaka wataalamu wa barabara waifanyie ukarabati.

Aidha, aliwataka wananchi kuwa waangalifu ili watoto wasipate madhara.



Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara wa Madini nchini (Tamida), Sam Mollel, akizungumza baada ya uzinduzi wa soko na mnada wa madini ya vito, uliopo ndani ya ukuta unaozunguka migodi ya madini ya Tanzanite, Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# CCM yalalamika wananchi kukosa huduma ya maji

**Na Zanura Mollel, LONGIDO**

CHAMA Cha Mapinduzi Wilaya ya Longido, kimelalamika wananchi kukosa maji wakati serikali imetoa fedha Sh. bilioni 15.8 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji wa Mto Simba.

Chanzo kikuu cha mradi huo, kimeanzia mkoani Kilimanjaro hadi kufikia Wilaya ya Longido na matarajio ya wananchi yalikuwa ni kupata huduma ya maji ya uhakika baada ya kukamilika kwa mradi.

Hata hivyo, hadi sasa maji hayajafika kama taarifa zilivyotolewa awali na baadhi ya wataalamu wa serikali.

Akizungumza wakati alipotembelea kukagua mradi huo, Mwenyekiti wa CCM, wilayani humo, Joseph Ole Sadira, alisema ni mara ya nne kwake kutembelea mradi huo na amekuta tangi hilo halina maji.

Ziara hiyo ya kukagua tangi la maji lenye ujazo wa lita 800,000 alifanya wakati wa siku ya maadhimisho ya miaka 43 ya CCM.

Amewataka wataalamu wa mradi huo, kujitathmini kwa nini maji hayapatikani kwenye tangi kwa wakati.

"Serikali imetoa Sh. bilioni 15.8 kwa ajili ya mradi wa maji Mto Simba, zimetupatia Sh. milioni 107 kwa ajili ya kujenga Mbauti, pia imeleta Sh. bilioni mbili kwa ajili ya mradi wa maji kwenda Namanga, ni vizuri wananchi wakalinda miundombinu hii," alisema Sadira.

Ameitaka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Arusha (Auwsa), kuwa wakweli kwa serikali kwa taarifa wanazozitoa, ili mradi huo ufikie hatua inayotarajiwa na serikali ya kupeleka huduma ya maji kwa wananchi wake.

Alisema Rais John Magufuli alipokwenda kufungua kituo kimoja cha forodha kati ya nchi ya Tanzania na Kenya, aliagiza mradi wa maji wa mto Simba ufike hadi Mji wa Namanga uliopo mpakani, lakini cha kushangaza wataalamu wanasema mradi huo hautafika huko.

"Rais John Magufuli aliuliza maji yapo yakutosha mlimjibu ndiyo, kwa nini mlimdanganya? Haya maji hata hapa Longido bado hata hayajawafikia wananchi ipasavyao ni kwa nini?" Alihoji Sadira.

Kamati ya siasa ya wilaya hiyo, ilitembelea vituo ambavyo wananchi wanatumia kuchota maji na maji hayakuwapo, huku wananchi wakilalamikia kukosa huduma ya maji.

Waliwataka viongozi hao wa chama kufuatilia jambo hilo, ili kubaini tatizo lililopo kwenye mradi huo.

Sadira alisema Desemba mwaka 2019, mradi huo haukutoa huduma kwa wanachi wa Mamlaka ya Maji Mji wa Longido, haikutoa taarifa kwa wananchi na viongozi kuhusu ukosefu wa maji.

"Nataka kujua ni kweli mradi huu, ulihujumiwa na wananchi kwa maana maji hakuna na hakuna maelezo yanayojitosheleza?" Alihoji Sadira.

Naye Meneja Ufundi kutoka AUWSA, Humphrey Mwiyombela, alisema ili maji hayo yafike katika Mji wa Namanga, ni lazima wataalamu waende tena kwenye chanzo cha maji cha mto Simba kwa ajili ya kuboresha.

Alisema mradi huo, uliibuliwa mwaka 2013, lakini utekelezaji wake ulifanyika mwaka 2017/18, kwa lengo la kupata majisafi na salama katika Mji wa Longido na utahudumia wakazi 16,000.

Akizungumzia uharibifu wa miundombinu, alisema mvua zinazoendelea kunyesha zimesomba mabomba kufuka katika eneo la Engasurai na kusababisha maji kukosekana kwa kuwa wataalamu walilazimika kufanya maboresho na ukarabati.





# Polisi wapewa mbinu za udhibiti madhara gongo

**Na Mary Mosha, ROMBO**

WANANCHI wilayani Rombo, wameliomba Jeshi la Polisi kubadilisha mbinu za kukabiliana na watengenezaji, wauzaji na wanywaji wa gongo ili kunusuru jamii kutokana na madhara yanayotokea kutokana na pombe.

Walisema hayo jana wakati wakizungunza na Nipashe katika Kijiji cha Makiidi ambapo Erinest Massawe, alisema licha ya serikali kujitahidi kutokomeza gongo, lakini bado tatizo ni kubwa katika baadhi ya vijiji wilayani humo hasa vya pembezoni.

Elinasari Makata, alisema ipo haya ya askari Polisi kubadili mbinu za kuwakamata watengenezaji na wauzaji wa gongo, lakini kila mara wanapokuja kwa magari na sare zao wahalifu wanatawanyika kupitia vichochoroni.

"Hali ya unywaji wa gongo katika Wilaya ya Rombo bado ni kubwa na Polisi hawawezi kulifuatilia hili kwa urahisi kutokana na namna yao ya kufika katika eneo la tukio hutumia magari wamevalia sare, hali inayowafanya wahalifu kutoroka mara wanaposikia mingurumo ya gari," alisema na kuongeza:

"Kwa sasa wauzaji wanatumia mbinu ya kumuuzia mtu kisha kwenda mbali na wao kwa ajili ya kunywa... wanaficha kwenye nguo, unaweza ukakutana nae na usione kama wamebeba."


Dismas Mrema, alisema tunashauri Jeshi la Polisi kama watabaini eneo linalotengenezwa gongo wakamate watendaji wa vijiji na vitongoji, lengo likiwa kutoa taarifa kamili ya wauzaji na watumiaji.

"Wako baadhi ya watengenezaji wa gongo wanaodai kuwa wamepewa kibali cha kutengeneza... hatujui, lakini tunaomba mamlaka husika kufuatilia chini ya ulinzi mkali ili kufahamu uhalali wa vibali walivyonavyo," alisema Mrema.

Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Aganes Hokororo, alikiri kuwapo kwa matukio kama hayo, na kusema jitiada za makusudi zimechukuliwa ikiwamo operationi maalumu ya kukamata wauzaji wa gongo na watumiaji ili kuhakikisha tatizo la gongo katika wilaya hiyo linatokomezwa.

"Operesheni hii ni endelevu, tutaendelea kuwakamata watengenezaji wa gongo na wanyaji wote hata wakitumia mbinu mbalimbali bado hatutawaacha na tutahakikisha tatizo la pombe Rombo linabakiwa kuwa historia," alisema Mkuu wa Wilaya.

Aidha, aliwataka wananchi kuacha tabia ya matumizi ya pombe na badala yake kujikita katika kuhakikisha wanafanya kazi kwa ajili ya maendeleo.



Baadhi ya wanawake wa jamii ya wafugaji wa Kimasai wilayani Hai, wakijadiliana kuhusu vitendo vya ukatili wa kijinsia hasa ukeketaji na ndoa za utotoni vinavyoendelea kuwatesa vijijini, wakati wa mradi wa nguvu ya pamoja ya kupambana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto ulioandaliwa na Shirika la Kwieco, juzi. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Hadhari ya utoaji msaada viti mwendo

**Na Mary Mosha, MOSHI**

LICHA ya kuwapo kwa walemavu wa viungo, ambao wana uhitaji mkubwa wa viti mwendo ili kuwasaidia kusogea sehemu moja kwenda nyingine, lakini wataalamu wanashauri kutopewa viti hivyo bila kupimwa kwa afya zao.

Wataalamu hao wanasema lengo la kupima afya ni kiwawezesha kuvitumia kama tiba.

Mtaalamu wa tiba kwa vitendo kutoka CCBRT Moshi, Neofita Lukiringa, aliitaka jamii inapotaka kuwasaidia watu wenye ulemavu hasa wa uti wa mgongo, kuhakikisha wanawataalamu wanafanya vipimo ili kupunguza madhara yanayotokana na matumizi mabaya ya viti mwendo.

"Tunaomba watu wanaotaka kutoa msaada wa viti mwendo ni wema kuwasiliana na wataalamu wa afya na wahusika mwenyewe kwa ajili ya kufanyiwa vipimo kabla ya kununua viti hivyo, kwa kuwa vinaweza kuwaletea madhara zaidi badala ya kuwasaidia kupata matibabu," alisema.

Jennifer Mushi, mlemavu wa uti wa mgongo Wilaya ya Hai, alisema wagonjwa wengi wa ulemavu wa uti wa mgongo na ulemavu mwingine hujikuta wanapata shida zaidi baada ya kusaidiwa viti mwendo kutokana na uhitaji wao.

"Jamii yetu haina uelewa, hata mimi mwenyewe sikuwa na uelewa mpaka nilipoelimishwa katika Hospitali ya Rufani ya KCMC, hivyo tunaiomba serikali kwa kushirikiana na wadau kuhakikisha wanatoa elimu kwa jamii kuwasaidia watu wenye ulemavu," alisema.

Samson Wilson ni mkazi wa Manispaa ya Moshi, alisema licha ya kukosekana kwa elimu ya baadhi ya mambo yanayowahusu walemavu ni kutokana na serikali kutotoa kipaumbele kwa jamii ya watu wenye ulemavu.

Alisema watu wenye ulemavu wamesahaulika na jamii ya baadhi ya Watanzania hasa katika taasisi za serikali hawapewi huduma stahiki, ikiwamo kusikilizwa, ukalimani hasa pale wanapotaka kutoa ushahidi au kutolewa ushahidi, mara nyingi hukosa haki zao za msingi.

"Serikali kupitia mashirika ya siyo ya kiserikali ya kutetea haki za binadamu, ni lazima kuanzisha vipindi maalumu katika vyombo vya habari vinavyotoa elimu mbalimbali na namna ya kumhudumia mlemavu ili kuwasaidia kupata haki zao za msingi," alisema.

Pulcaria Aloyce, katibu wa chama cha walemavu Wilaya ya Hai, alikaririwa na Nipashe katika kongamano la kuwaelimisha wadau na kuiomba serikali kuangalia namna ya kuwasaidia walemavu kujikimu na kuondoa unyanyasaji.

"Mbali na misaada tunayopatiwa ya walemavu kama viti, lakini havina ubora na kusababisha madhara zaidi...lakini pia serikali iangalie namna ya kuwaajiri wakalimani wa lugha, katika vituo maeneo muhimu kama, mahakama, hospitali na polisi," alisema na kuongeza:

"Lakini upo umuhimu wa kuelimisha madereva kuacha tabia ya kuwanyanyasa na kuwadhalilisha walemavu wanapopanda vyombo hivyo."

## Mpango waja kulinda Mlima Kilimanjaro

**Na Mary Mosha, MOSHI**

KATIKA jitihada za kuhakikisha theruji ya Mlima Kilimanjaro inaendelea kuwapo, shirika lisilo la kiserikali ya Kilimanjaro Project limekuja na mpango kabambe wa kufuatilia miti inayooteshwa kwa njia ya mtandao.

Wakizungunza jana wakati wa upandaji wa miti katika Shule ya Sekondari ya Kimochi, mkuu wa kitengo cha usimamizi wa miti kwa njia ya mtandao, Samuel Andrew, alisema mpango huo unaweza zoezi la upandaji na usimamizi wa miti ili kutunza uoto wa asili.

Alisema wameanzisha programu hiyo ili kuhakikisha miti yote inayopandwa haifi hata mmoja kwani inafuatiliwa kwa njia ya mtandao (GPS).

"Hii inapatikana kwenye 'play store', lakini ili kuitumia lazima uje kwetu ili tuweze kukupa maelekezo ya namna ya kutumia, kwani unapapaswa kupiga picha mti mmoja mmoja na sio yote kwa ujumla," alisema Samwel na kuongeza:

"Hii ni fursa kwa wananchi kwani kwa kila atakayeingiza mti wake kwenye mtandao huo na kuufuatilia ipasavyo, atalipwa shilingi 100 kwa kila mti... Hii ni kuhamasisha Watanzania kupanda miti zaidi na kuitunza bila kutoa sababu yoyote."

Ofisa Uhamasishaji kutoka Shirika Mwenza la Nipe Fagio, Wilyhard Shishikaye, alisema katika shule hiyo wameotesha miti 250 ya aina tano tofauti ikiwamo mikuyu na mizambarao kwa ajili ya kulindana na mazingira ya shule hiyo.

Alisema mbali na kuotesha miti hiyo, pia wanatoa elimu juu ya namna ya kuotesha miti na maeneo ya kuotesha ili kulinda uoto wa asili na kutunza mazingira.

Crispin Nyoni, Mkuu wa Shule ya Sekondari Kimochi, aliishukuru taasisi hivyo kufika katika shule hiyo kuotesha miti na kutoa elimu kwa wanafunzi hao.

**"Hii ni fursa kwa wananchi kwani kwa kila atakayeingiza mti wake kwenye mtandao huo na kuufuatilia ipasavyo, atalipwa shilingi 100 kwa kila mti... Hii ni kuhamasisha Watanzania kupanda miti zaidi na kuitunza bila kutoa sababu yoyote."**




Ukurasa 17

**Dondoo za safari ya mageuzi nchini**

## Nchi za Sahel katika mtihani ubia na Ufaransa vita ya uasi



Ukurasa 15



Ukurasa 14

**Katiba safari kuwa ajenda uchaguzi wa Kenya**

siasa
JUMATANO FEBRUARI 5, 2020
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU



Ukurasa 18

**Jenerali Ndayishimiye; mtarajiwa anayerithi kiatu cha Nkurunziza?**

# Mtetezi siasa anapobeba sura mbili kwa hoja moja

• Kila muongo, maana mpya, hoja ileile

**Na Ani Jozeni**

MTAALAMU wa masuala ya Afrika nchini Marekani, aliandika kwa miaka 10 au zaidi baada ya uhuru katika juzuu la siasa za nchi zinazoendelea, alipoingiza insha 'Demokrasia na Ujamaa: Itikadi za nchi za Kiafrika,' hali ambayo miaka 20 baadaye ilipanguliwa kuwa 'demokrasia na maendeleo.'

Kimsingi, vyama vya siasa vya Afrika ni vya 'demokrasia na maendeleo.' Masuala mengine yaliyobaki yanatokana na vyanzo tofauti vya utii kwa utawala uliokuwa madarakani, unaotaka kubatilisha ukweli.

Ni kwa mizania hiyo, mtu anaweza kupima mchango wa

**INAENDELEA UK.16**





Viongozi wa vyama vya upinzani walipokutana. **PICHA: MTANDAO**

**Somo la Ngawaiya, upenyo sahihi kuwanasa viongozi bora Oktoba** Ukurasa 20

UCHAMBUZI

# Katiba safari hii inakuwa ajenda kuu uchaguzi Kenya



Rais Uhuru Kenyatta akiwa na makamu wake, William Ruto. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mashaka Mgeta**

MFUMO wa Uchaguzi Mkuu wa Kenya unaathiriwa na mahitaji ya nyakati yanayopata nguvu kwa kuungwa mkono na mfungamano wa vyama vya siasa, ukirasimishwa na utafutaji mamlaka ya dola nchini humo.

Ndiyo hali iliyokamata Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2007 ambao Rais Mwai Kibaki, alipata ushindi uliotiliwa shaka, dhidi ya aliyekuwa mshindani wa karibu, Raila Odinga.

Wakati huo, ajenda iliyotawala msuguano ni 'Katiba Mpya' iliyowagawa Wakenya katika makundi yaliyojulikana 'chungwa' kutoka timu ya mshindi na mpinzani wakati huo, Odinga - 'ndizi'.

Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2013, mada mpya kwa vyama ikawa 'Kushitakiwa Kwenye Mahakama ya Kimataifa ya Makosa Dhidi ya Ubinadamu (ICC)". Hapo ikawagusa Rais Uhuru Kenyatta, Makamu wake, William Ruto na wengine kadhaa.

Upande wa Raila ulisisitiza sheria kuchukua mkondo wake dhidi ya 'watuhumiwa'na wahusika wa kadhia hiyo, walifikia kila kona ya Kenya kukanusha kuhusika na hilo la mauaji ya baada ya uchaguzi.

Hivi sasa, wakati Kenya ikijiandaa na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2022, hoja inayotawala ni 'mabadiliko ya katiba' yanayotarajiwa kuwa sehemu ya mapendekezo ya kamati maalum iliyoundwa na Rais Kenyatta, kuratibu shughuli za serikali, ili kuongeza ufanisi nchini humo maarufu kama BBI.

Kamati inadaiwa kumuweka kando Ruto na washirika wake, hivyo inatafsiriwa ni hatua ya kumfuta katika siasa za taifa hilo.

> Wanaotuletea matatizo katika chama cha Jubilee ni watu kutoka nje ya chama chetu, tuna chama chetu cha Jubilee kwa hiyo wengine wanapaswa kujipanga kivyao.

**KENYATTA, ODINGA NA BBI**

Upande wa Rais Kenyatta, anayeshirikiana na Raila, wanaounga mkono mabadiliko ya kikatiba inayotoa nafasi nyingi za uongozi kama waziri mkuu na manaibu wawili, washirika wa Ruto wanaliona kuwa gharama kubwa za uendeshaji serikalini na sasa wameanzisha kampuni inayojulikana 'punguza mzigo'.

Odinga, alishafika hadi Kaunti ya Migori hivi karibuni, akiwashawishi wafuasi wa chama chake kupuuzia kampeni ya 'Punguza Mizigo' itakapowasilishwa kwa ajili ya kujadiliwa.

Akiwa kijijini Rinya, katika mji mdogo wa Uriri Ijumaa iliyopita kwenye mazishi ya Askofu Joseph Ogutu wa Kanisa la St John Everlasting, akihimiza makubaliano ya BBI ndiyo yanayopaswa kufuatwa na anafafanua:

"Haya masuala ya 'Punguza Mizigo' hatuyajui, tunawaomba Bunge la Kaunti Migori, kuyakataa pindi muswada utakapowasilishwa kwenye baraza lenu kwa kujadiliwa."

Raila anamtaka Gavana wa Migori, Obado, kuhakikisha kaunti hiyo inafuata mfano wa wenzao wa Siaya (anakotoka Raila) kuukataa muswada wa 'Punguza Mizigo' uliopigiwa upatu.

Gavana Obado, anamthibitishia Odinga, ataunga mkono jitihada za kushikana mkono na Rais Kenyatta, akidai kuwapo mafanikio ya uboreshaji bandari ya Kisumu utakaochochea maendeleo na ustawi wa wananchi wake.

Mbunge wa Uriri, Mark Nyamita, analitahadharisha Bunge la Migori, lisipoukataa muswada wa kinan Odinga ulioko mbioni sasa, watahitajika kujiandaa kurejea kwao kwa kukosa imani kwa wapiga wao.

"Muswada wa 'Punguza Mizigo' hautaeleza masuala ya Wakenya na unakosa baraka za raia wa Kenya," anasema.

Awali, taarifa zilieleza Rais Kenyatta na Raila, watafanya kampeni nchi nzima kuwaelezea raia mapendekezo ya kamati maalum ya BBI itakapokamilisha kazi iliyopewa.

**MABADILIKO KATIBA**

Katibu Mkuu wa Muungano wa Vyama Vinavyotawala Kenya wa Jubilee, Raphael Tuju na Mwenyekiti wa ODM, John Mbadi, wanasema ziara za viongozi zitawawezesha Wakenya kuelewa mwelekeo wa nchi, kadri ya mapendekezo yatakayotolewa.

Tuju akasema waraka wa BBI utakaowekwa kuwa muswada, unaweza kupitishwa na Bunge ama kama ya yatatakiwa maoni ya wananchi, basi kura itapigwa.

Kumbukumbu zinaonyesha, Raila aliwahi kuwataka Wakenya wajiandae kwa kura ya maoni ya mabadiliko ya katiba mwakani.

Hiyo inamaanisha, pindi ripoti ya BBI itakapokamilika, ni wazi ziara ya Rais Kenyatta na Odinga, zitalenga kuipigia kampeni na Rais Kenyatta na Raila, wakapanga ziara ya mikutano yao ya awali ya pamoja, eneo la Mlima Kenya.

**WATAALAMU RIPOTI**

Wakili Paul Mwangi, ni Katibu Mwenza wa BBI, anayesema walikuwa wanaandika ripoti itakayokabidhiwa kwa Rais Kenyatta na Raila.

"Muda tuliopewa kukabidhi ripoti hii ni Oktoba, lakini tutafanya kila linalowezekana kuhakikisha tunaikamilisha kazi hii kabla ya muda huo," anasema Mwangi.

Mwanasheria Mkuu wa zamani wa Kenya na Seneta wa Busia, Amos Wako, ni mjumbe wa timu ya BBI, anasema hawawezi kuanika maudhui ya dondoo walizozipata mpaka wakabidhi ripoti.

Tuju anaeleza imani yake, kwamba itakuwa na mapendekezo yatakayochochea umoja wa kitaifa.

**KENYATTA ANG'ARA**

Licha ya historia wanasiasa Kenya 'kugeukana' kuelekea Uchaguzi Mkuu, upande wa Rais Kenyatta katika Jubilee unadaiwa kuungwa mkono na vyama vya ODM ya Raila, Wiper Democratic Movement ya Kalonzo Musyoka, Amani National Congress ya Musalia-Mudavadi, Ford Kenya ya Moses Wetang'ula na Kanu ya Gideon Moi

Ni muungano unaoonekana kuimarika na huenda ukatoa mwelekeo wa mgombea urais katika ychaguzi wa 2022.

**RUTO AMTESA BOSI**

Ruto hivi sasa kupitia washirika wake, wanapinga kwa wazi jitihada za BBI na hatua inayoendeleza 'kutembea njia tofauti' na bosi wake, Rais Kenyatta na hasimu wake mkubwa zamani, Raila.

Ni muungano wa vyama vinavyounga mkono mabadiliko ya katiba na vinabeba dhana kuu, mfumo uliopo wa Rais kuwa mkuu wa nchi haufai, kwani unachangia ukabila, hivyo uboreshwe.

Kina Rais Kenyatta na Raila, wanataka mabadiliko ya katiba yaruhusu utawala unaozingatia jinsia kwa theluthi mbili na uteuzi wa wabunge, hata kuwa mawaziri.

**RAILA NA URAIS**

Dalili za Raila kuusaka urais katika uchaguzi ujao zimeibua sintofahamu katika muungano wa Nasa, aliyoupitia kuwania kiti hicho katika uchaguzi mwaka juzi, Nasa ilipojumuisha vyama vya Wiper Democratic Movement, Amani National Congress (ANC) na Ford Kenya.

Ingawa Raila hajatamka nia yake, lakini mwenendo wake kisiasa baada ya kushikana mkono na Rais Kenyatta Machi 9, mwaka jana, unaashiria hilo.

Vyama vya Wiper na ANC washirika wa Nasa, vimewahi kutamka kwamba baada ya kuwania urais wa Kenya mara nne bila ya mafanikio, safari hii wanapaswa kumuweka kando Raila.

Mkurugenzi Mtendaji wa Wiper, Jared Siso, alisema chama hicho kinaamini Raila ana dalili zote za kuwania urais safari ijayo.

Anasema, makubaliano ya Nasa bado yapo na hawatakuwa na namna nyingine, zaidi ya kumuunga mkono Kalonzo Musyoka, anayepaswa kuwania kiti hicho.

**RUTO AJIIMARISHA**

Ruto amekuwa akimshutumu Raila kwa kuingilia mambo ndani ya Jubilee, huku akitumia kigezo cha kushikana mkono kwake na Rais Kenyatta.

"Wanaotuletea matatizo katika chama cha Jubilee ni watu kutoka nje ya chama chetu, tuna chama chetu cha Jubilee kwa hiyo wengine wanapaswa kujipanga kivyao," anasema.

Ruto anaamini kwamba walioko nje ya Jubilee ni wajuzi wa kupiga kelele, tofauti na Jubilee inayolenga kuchagiza kasi ya maendeleo ya Kenya na watu wake.

***Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali. Mwandishi wake anapatikana kupitia simu namba +255 754 691540 ama barua pepe:mgeta2000@yahoo.com***

# Nchi za Sahel katika mtihani ubia na Ufaransa vita ya uasi

• Macron aambiwa 'bora magaidi kuliko yanayoendelea...'



Viongozi wa jumuiya ya nchi ukanda wa Sahel, walipokuwa mkutanoni na Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron (wa tatu kutoka kulia), hivi karibuni. **PICHA: MTANADAO**

**Na Anil Kija**

NCHI za Ukanda wa Sahel, zinazopakana na jangwa la Sahara, ziko katika mtihani mgumu wa kuunda umoja wa kimkakati na Ufaransa, kuunganisha majeshi na usimamizi wa mapambano, ili kukabiliana na makundi ya kigaidi yanayozidi kusambaa katika eneo hilo.

Kwanza, kuna makundi ya jadi ya kigaidi kama Boko Haram ya Nigeria, ambayo sasa imesambaza mashambulizi nchi za jirani (kama ilivyo Al Sahaab nchini Somalia na makundi mapya ya kigaidi nchini Msumbiji).

Halafu kuna makundi yanayotokana na athari za kuangushwa utawala wa Kanali Muammar Gaddafi wa Libya mwaka 2011, ambao walishiriki vita nchini humo sasa wanaieneza kute Afrika Magharibi. Ndiyo hasa ambao umoja tarajiwa unawalenga.

Wachunguzi wa habari wanasema, licha ya kuwa tishio la ugaidi na uharamia limekuwa jambo la kawaida katika eneo hilo na hivyo hitaji la kuunganisha nguvu na kungwa mkono na Ufaransa, yenye vifaa na uwezo kusimamia eneo pana la mapambano kama ukanda wote wa Afrika Magharibi, kuanzia Libya hadi Gambia au Niger kwa upande wa Mashariki, zinatafsiriwa ziko katika hisia za kihistoria zinazoweza kukwamisha dhamira hiyo.

Ni hisia kali zilizokuwapo tangu mapema uhuru miaka miaka ya 1960 na kwa vile Ufaransa imekuwa na uhusiano wa karibu na makoloni yake kuliko Uingereza.

Ndiyo maana kulikuwapo mshangao wa kiasi fulani, pale Rais Emmanuel Macron wa Ufaransa, alipowakaribisha marais wa nchi tano za Afrika Magharibi kwa suala hilo, lakini inaelekea alitilia maanani ukinzani huo wa kuhusika kwa Ufaransa kwa karibu eneo hilo.

> Hakuitisha mkutano wenye mbembwe za kidiplomasia na gwaride la heshima jijini Paris, kama ambavyo ingetazamiwa, bali ilikuwa ni kikao cha mashauriano, wala si mkutano wenye hadhi hiyo.

Hakuitisha mkutano wenye mbembwe za kidiplomasia na gwaride la heshima jijini Paris, kama ambavyo ingetazamiwa, bali ilikuwa ni kikao cha mashauriano, wala si mkutano wenye hadhi hiyo.

Kikao hicho kilifanyika mjini Pau, mji mdogo wa kitalii mpakani na Hispania, eneo la Kusini Magharibi.

Wachunguzi wa habari wanasema, wakati viongozi hao wanajumuika mahali hapo, hali ilikuwa mbaya katika hisia na yanayozungumzwa katika vyombo vya habari.

Ufaransa ilikuwa imepata pigo miezi miwili kabla, wakati helikopta zake mbili za kijeshi zilipogongana katika usiku wa giza nchini Mali, ambako vikosi vya Ufaransa vinapambana na makundi ya kigaidi na askari wote 13 waliokuwamo katika helikopta hizo waliuawa.

Badala ya kuonyesha mshikamano na Ufaransa katika ajali hiyo wakati ikisaidia serikali zao kupambana na ugaidi, waandamanaji katika nchi za Mali, Niger na Burkina Faso, walibeba mabango kumtaka Rais Macron na askari wa Ufaransa waondoke.

Kwa kifupi, ulikuwa na ujumbe 'heri ugaidi kuliko kusaidiwa na Ufaransa '" wakati serikali za nchi hizo zimeonyesha wazi hazina ubavu wa kupambana na makundi hayo kikamilifu.

Hali hiyo imefanya vyama vya siasa na vyombo vya habari kuhoji Ufaransa inafanya nini katika eneo hilo na ni kwa mantiki gani inadhani inaweza kushinda vita dhidi ya ugaidi?

Ni hatua iliyopo, wakati Marekani inajaribu na kushindwa, iwe ni Afghanistan, Pakistan, Somalia au jeshi la Kamandi ya Afrika, ambalo limeendesha mashambulizi dhidi ya Al Shabaab, ADF nchini Uganda (ndipo kikundi hicho pamoja na LRA- Lord's Resistance Army - yakajichimbia misitu ya huko DRC? Ni swali ambalo halijajibiwa; Rais Macron anajaribu kujenga taswira ya kukubalika ushirikiano.

### HALI YA MADHARA

Takwimu za madhara ya ugaidi katika eneo hilo zinatisha, kutokana na kuongezeka makundi ya ugaidi na mashambulizi hasa dhidi ya makambi ya jeshi na kuua askari wengi, ambao hawana vifaa na miundombinu ya upelelezi kujua kuwa makundi ya magaidi hayako mbali.

Jumla ya askari 89 wa Niger walikufa katika shambulio mwezi huu na wapo 71 waliokufa katika shambulio mwezi Desemba, kasha raia 41 wa Burkina Faso wakiwamo watoto saba waliokufa katika bomu la kutegwa kando ya barabara.

Taarifa zinazema, idadi ya watu wanaokufa kwa mashambulizi inaongezeka, wakati miaka mitatu iliyopita kuna watu 770 waliokufa katika mashambulizi ya kigaidi katika nchi za Mali, Niger na Burkina Faso na mwaka jana walifikia zaidi ya watu 4,000 waliokuwa katika mashambulizi kama hayo.

Wachambuzi wa habari nchini Ufaransa, wanasema mashambulizi ya kigaidi ya sura kadhaa zinazokanganya, kwani kwa sehemu kubwa yana vianzio ndani ya nchi na siyo tu uvamizi wa makundi kama Boko Haram au yale yanayotokea Libya.

Nchi hiyo ilikuwa na makundi makubwa ya wapiganaji waliokuwa chini ya uangalizi wa Kanali Gaddafi na alipouawa, halafu ikazuka vita ya kuikamata nchi hiyo, halafu maharamia wengine wanarudi kutoka vita ya Dola ya Kiislamu nchini Irak na Syria, eneo hilo limejaa wapiganaji huria.

Hata hivyo, uwepo wa mivutano ya kidini na kupigania rasilimali kwa mfano maeneo ya kilimo au ufugaji inaelezwa kuwa tatizo.

Kwa maana hiyo, Rais Macron haungwi mkono kwa urahisi na vyama vya siasa vya Ufaransa, akijaribu kuziokoa nchi za Afrika zisitumbukie katika shimo la ugaidi na kudidimia vitani, kama ilivyo Nigeria, Somalia, Jamhuri ya Kidemokrasi Congo (DRC) na kwingineko.

### WAONAVYO WATAALAMU

Baadhi ya wachambuzi wanaona, ni jambo jema kwa Ufaransa kuendelea kuzisaidia nchi hizo kupambana na hatari ya ugaidi, lakini kujiingiza kichwa ni kutumbukia katika vita ambayo Ufaransa haiwezi kushinda na kuna mtaalamu aliyeonya kupitia maandiko vitabuni "Vita Iliyoshindwa: Ufaransa katika Sahel."

Mtaalamu mwingine, aliyehojiwa alisema mapambano hayo ni kama mtego, ambako katika mkutano wa Pau ilikubaliwa Ufaransa iongeze askari 220 katika idadi ya 4,500 waliopo katika eneo hilo tayari.

Mwandishi wa habari wa nchini Mali, alimuuliza Rais Macron kuhusu upinzani ulioko kwa uwepo wa askari wa Ufaransa na alijibiwa: "Muda wowote nchi ya Kiafrika ikitaka askari wa Ufaransa waondoke, tutaondoka."

Mtaalamu aliyeandika kitabu, ana maoni kwamba jawabu la wimbi la ugaidi katika Afrika Magharibi, linatakiwa liwe la kisiasa na si kijeshi, wakati huko Pau marais watano walisema wanataka askari wa Ufaransa wabaki.

Pia, kuna msomi mwingine anasema kuwa Ufaransa 'haiwezi kuiacha vita hiyo ikaenda zake' kwani eneo hilo litadidimia) na pia haiwezi kushinda.

# Mtetezi siasa anapobeba sura mbili kupitia hoja moja



Ilivyokuwa harakati za kudai siasa za vyama vingi nchini. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**INATOKA UK.13**

hivi karibuni wa mtendaji mkuu wa asasi muhimu nchini ya kiraia yenye utashi na jamii, anayesema katika jopo la majadiliano kuhusu haki na uhuru wa mtu binafsi nchini.

Anasema kuna umuhimu wa Watanzania kuendelea kupigania haki, upana wa demokrasia na uhuru wa vyombo vya habari.

Kimsingi, inakumbusha alichokisema Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ukumbi wa Nkrumah Agosti mwaka 1978, alipojibu swali la dai kutoka kada ya wasomi 'kuwapo hofu nchini.'

Mtendaji huyo, alikuwa akizungumza na wanahabari na wadau wengine wa tasnia hiyo katika jukwaa kuhusu kujenga taifa la amani, wakati nchi inaelekea uchaguzi mkuu, Oktoba ijayo. Aliongeza 'uhuru hautolewi tu, pia inapiganiwa.'

Ni msimamo pia aliyoutoa Mwalimu Nyerere, katika majibu ya maswali chuoni hapo, ambao baadaye ikawa nukuu ya wanaharakati wasomi katika miaka iliyofuata, kama Profesa Issa Shivji.

Kuna chembe ya maswali katika ya kauli ya mtendaji huyo anayechukua safari mpya. Kama angekuwa anaegemea kambi tofauti kisiasa, pia umri wake si wa siku nyingi katika historia ya siasa ya nchi, huenda mantiki ingeonekana.

> Kwa mantiki ya kawaida, kielelezo sahihi cha mahali alipo ni kusimamia hoja kama 'maendeleo yanahitaji mshikamano' na siyo dhana 'demokrasia inapiganiwa.'

Kwa mantiki ya kawaida, kielelezo sahihi cha mahali alipo ni kusimamia hoja kama 'maendeleo yanahitaji mshikamano' na siyo dhana 'demokrasia inapiganiwa.'

Ni kwanini hivyo? Kimsingi, anayeunga mkono kinachoendelea sasa, hawezi kutanguliza 'kupigania' ila kujenga umoja unaohitajiwa, ili kufanikisha majukumu hayo. Yaani atalenga zaidi 'maendeleo' si 'kusaka demokrasia.'

Ni wastani wa miaka 10 iliyopita, kuna tofauti kuhusu insha zake na ya mwanzoni mwa mwaka huu. Kwa kuziunganisha, zinaanika mabadiliko makubwa. Awali alikuwa na insha muhimu katika maisha ya wanaharakati nchini iitwayo 'Watu: Hoja Kuhusu Watu.'

Iligusia dhana ya Azimio la Arusha kuhusu tunachohitaji tuendelee ni: Watu, Ardhi, Siasa Safi na Uongozi Bora. Watoa rai katika majukwaa tofauti ya ki-CCM kwa miaka mingi, walikuwa wanacheza katika eneo la 'uongozi bora' licha ya kwamba aliwahoji mambo kadhaa.

Mwaka 2009 katika mada au hoja hiyo, kiongozi huyo awa asasi isiyo ya kiserikali, ambaye ana mizizi ya utendaji wa huduma za umma katika historia ya nchi, alihoji dhana 'watu' na kile wanachofanya katika uongozi akidadisi nafasi ya 'umati' wa wazalishaji na 'walaji' katika uchumi.

Mabadiliko hayo ya kihisia kwa baadhi ya wasikilizaji na wanaofuatilia hoja zake, wanaona kuzaliwa mkanganyiko.

### HOJA VS HISTORIA

Hata hivyo, hoja hiyo waliobahatika kupitia taaluma ya historia vyuoni, wanaweza kugusa tofauti hizo kama jambo la kawaida katika maisha ya watu mashuhuri.

Mjerumani George W.F. Hegel, alisema watu hao wanatokea katika historia kana kwamba ni mara mbili, karne tofauti kabisa. Mwingine akaongeza 'kwanza inakuwa kama mkasa, halafu baadaye, kama mzaha.'

Ndiyo hilo kutoka kwa mtoa kauli huyo wa mwaka 2009 alisikitikia mwelekeo wa nchi wa utandawazi (na ubinafsishaji) akililia "utu wetu, Uafrika wetu, uzalendo wetu, Utanzania wetu..." kuwa yote yako shakani kutokana na utandawazi. Sasa amelisahau hilo kidogo na shaka ni kuhusu 'demokrasia.'

Sasa mtu anajiuliza, ni kitu gani kinatawala katika hisia za wanaharakati, kuwa katika miaka ya 2,000 walikuwa wanapigania tunu za uzalendo, hasa 'kumuenzi Mwalimu Nyerere,' lakini hao wanaonekana kupisha kidogo kimatendo, sasa wanaihimiza 'demokrasia' na kuiacha mbali 'tunu za mwalimu.'

Ni dhana inayodhihirisha hata kwa mtoa hoja huyo, amekuwa karibu zaidi na ng'ambo kuliko ukaribu na safu yake ya miaka 'nenda rudi.' Leo hii anakuwa mkosoaji hodari wa kasoro zilizopo chumbani kwake, akililia 'demokrasia'.



Mkutano wa kisiasa wa umoja wa vyama vya upinzani, uliofanyika mjini Dodoma.

### SWALI GUMU

Swali linazuka kutokana na uhalisia huo, kwanini pale 'watu' wanapofuata kinachotajwa 'utandawazi na 'demokrasia' ndio wanalilia uzalendo na utu wa Mwafrika, halafu wakiingia katika utekelezaji, tena kuna kingine cha 'demokrasia'?

Siyo swali linaloweza kujitokezaa kila mahali. Kuna mpangilio wa fikra kama zilivyo chembe za uhai mwilini. Kukiwapo 'pH' ya utandawazi (licha ya kuwa kuna demokrasia) wanakimbilia uzalendo, halafu 'pH' ikibadilika kuwa ya kizalendo (ni pamoja na mapinduzi) wanalilia 'demokrasia.'

Kuna ushuhda wa mambo na tabia zinazojitokeza katika jamii za Kiafrika, watu wanajitokeza na visivyoendana na mapinduzi ya kiuchumi kwao sasa, halafu demokrasia.

Ndiyo hapo inaweza kuingia dhana ya falsafa ya uandishi wa historia (Ulaya) ya 'butterfield sober' yaani makini na 'butterfield drunk' (aliyelewa), kuwa inapokuwepo demokrasia, wanaharakati wanaichukulia 'poa' na kutenda lolote wanalotaka, bila kujua wanahatarisha mfumo unaowalea.

Ndiyo mshtuko uliojikita katika pale waliposhuhudia dhana za ushindani wa kisiasa zilipoanza, zikiwa na kauli nzito majukwaani kutishia uwepo wa uhuru uliozoeleka, kwamba pengine unapaswa kuwekwa kando. Swali linakuja, kwa manufaa ya nani na iweje?

Kikubwa ni watu wafanye kazi za maendeleo kwa miaka mitano, halafu wachague viongozi kupitia taratibu najukwaa yaliyopo, pasipo maandamano na yanayofanna nayo. Pameshashuhudiwa kwingineko, matokeo yake yanazaa kipi.

> Demokrasia ina mipaka. Imebeba ungo wa 'marufuku' katika uhuru wa kutumia visivyo fedha na rasilimali ya umma.

Huyo ndiye 'butterfield drunk' anayechukulia demokrasia kuwa 'si mali kitu,' akitaka pia kuwepo uzalendo halisi katika uendeshaji uchumi, kwa maana ya kimapinduzi 'kudhibiti rasilimali za nchi zisichotwe.'

Mara zote 'kupanga ni kuchagua' na huwezi kuchagua vyote, mapinduzi na demokrasia kwa wakati mmoja. Haijatokea na haiwezekani, pia 'inapowezekana' inazaa janga. Si sahihi, hata kusema 'demokrasia' kwa maana kuwa uchumi uelee kushikwa na soko kwa asilimia zote pasipo kuhitaji mshikamano maalum na udhibiti wake.

Demokrasia ina mipaka. Imebeba ungo wa 'marufuku' katika uhuru wa kutumia visivyo fedha na rasilimali a umma. Usahihi wake unabaki katika maendeleo yaliyoelekezwa, huku uzalendo ukibeba tafsiri ya kubana uhuru uliowekwa.

## Zilivyo dondoo za safari ya mageuzi nchini




Mwalimu Julius Nyerere, alipojumuika na umma kufurahia uhuru wa nchi. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

HISTORIA ya mfumo wa vyama vingi nchini, inaanzia miaka ya 1950, wakati Tanganyika ilipodai uhuru chini ya chama cha Tanganyika African National Union (Tanu).

Vyama vingine vilivyokuwapo ni African National Congress (ANC), All Muslim National Union of Tanganyika (Amnut) na United Tanganyika (UTP).

Uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi uliofanyika 1958 na Tanu ilifanikiwa kupata ushindi mnono wa viti 28 kati ya 30 vilivyoshindaniwa.

Mwaka 1960 ulifanyika uchaguzi wa wabunge na Tanu iliendeleza kupata ushindi wake, viti 70 kati ya viti 71 vilivyokuwapo.

Tanganyika ilipata uhuru wake Desemba 9, 1961 chini ya Tanu iliyokuwa ikiongozwa na Mwalimu Julius Nyerere. Alianzia nafasi ya Waziri Mkuu na uchaguzi wa tatu ulifanyika mwaka 1962.

Ni mwaka uliokuwa na baadhi ya mageuzi, nafasi ya Waziri Mkuu iligeuzwa kuwa Rais, na wakati huo huo, Rais Mwalimu Nyerere alirejea nafasi yake kuongoza serikali, baada ya kujiondoa kwa muda kwenda kuongoza chama cha Tanu.

Tanganyika iliungana na Zanzibar, April 1964 na muda mfupi baadaye, mfumo wa vyama vingi ulifutwa rasmi mwaka 1965 na kuanzia wakati huo, Tanu ikawa chama kilichoshika hatamu za uongozi.

Katika zama za mwaka 1964/1965 una mengi ya kihistoria, kama vile kuundwa kwa Jeshi la Wananchi Tanzania.

Mwaka 1977 Tanu iliungana na ASP ya Zanzibar na kuunda Chama Cha Mapinduzi (CCM), kilichoendeleza mfumo wa chama kimoja hadi mwaka 1992, Tanzania iliporejea rasmi kisheria katika mfumo wa vyama vingi na ndiko kwenye chemchem kuibuka vyama vingi vya kisiasa, kama vile NCCR Mageuzi, TLP, CUF na Chadema,

Harakati za kudai kurejeshwa mfumo wa vyama vingi zilikolea nchi nzima na mwaka 1991, Rais Ali Hassan Mwinyi aliteua Tume iliyoongozwa na Marehemu Jaji Mkuu Francis Nyalali, kukusanya maoni ya wananchi na kutoa mapendekezo kujua kama taifa lilihitaji mfumo wa vyama vingi au kuendelea na mfumo wa chama kimoja.

Harakati hizo zilisababisha kubadilishwa katiba, ili kurejesha mfumo wa vyama vingi, uliositishwa kwa zaidi ya miongo miwili na nusu.

Ni mabadiliko yaliyoendana na kuanzishwa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, ambayo kwa mujibu wa sheria, mbali na kusajili vyama, anapaswa kuhakikisha sheria inafuatwa na vyama vya siasa.

# Jenerali Ndayishimiye; mta anayerithi kiatu cha Nkurur



Wananchi wa Burundi, katika moja ya harakati zao za siasa.

**Na Mashaka Mgeta**

MKUTANO wa dharura wa chama tawala cha nchini Burundi cha CNDD-FDD, kinachoongozwa na Rais Pierre Nkurunziza, umemtangaza kiongozi wa chama hicho, Meja Jenerali Evariste Ndayishimiye (52) kuwa mgombea urais katika Uchaguzi Mkuu wa Mei mwaka huu nchini humo.

Akaunti ya mtandaoni ya 'twita' ya chama hicho ilikuwa na taarifa kutoka katika mkutano wake uliofanyika kwenye jimbo la vijijini la Gitega iliyosomeka, "Jenerali Evariste Ndayishimiye amechaguliwa kuwaikilisha CNDD-FDD katika Uchaguzi Mkuu wa 2020."

Rais Nkurunziza, ameshatangaza azma yake ya kutowania urais baada ya muhula wake wa tatu kwa Uchaguzi Mkuu wa 2015 kuzuia utata na mgogoro wa kisiasa nchini humo.

Maelfu ya Warundi waliongia mitaani kupinga ushiriki wa Rais Nkurunziza katika uchaguzi huo, ambapo watu wengi walidaiwa kufa na wengine kuyakimbia makazi yao.

Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya Jinai (ICC), ilifanya uchunguzi wa vurugu za baada ya Uchaguzi Mkuu huo, ikijielekeza zaidi katika matukio ya mauaji, ubakaji, mateso na kupotea kwa watu.

Kitendo cha Rais Nkurunziza kuongoza mihula mitatu, kiliibua shutuma za kuwapo vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu na ukandamizaji wa kikatili.

> Nkurunziza atarudi tu, hawezi kwenda mbali. Atakuwa anafanya kazi kupitia mlango wa nyuma akijaribu kuilinda familia na utajiri wake.



Evariste Ndayishimiye, katika majukumu.

Miaka miwili iliyopita alishatamka kwamba hatawania tena nafasi hiyo ya juu ya uongozi wa nchi iliyo mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Pia, alikaririwa kwenye mkutano Jumapili iliyopita wa CNDD-FDD uliofanya uteuzi huo, akisema "mwanzo wa ukurasa mpya katika historia ya Burundi na kwa chama cha CNDD-FDD."

Mgombea urais mteule Jenerali Ndayishimiye, anatajwa kwamba si mwanasiasa mgeni nchini humo, kwani alishatumikia nafasi kama Waziri wa Mambo ya Ndani, Waziri wa Usalama na Mkuu wa Baraza la Rais la Raia na Jeshi nchini humo.

Alikuwa mmoja wa watu waliotia saini makubaliano ya kusitisha mapigano ya wenyewe kwa wenyewe mwaka 2003.

Bado haijajulikana kuhusu hatima ya Rais Nkurunziza kisiasa; lakini alikaririwa akipanga kubaki nchini humo kwenye makazi yake yanayodaiwa ya kifahari yanayobatizwa kama 'Luxury Villa' akijinyakulia malipo ya Euro 500,000 sawia na mshahara wake atakaolipwa kipindi chote cha maisha yake, kwa mujibu wa sheria mpya iliyopitishwa nchini humo.

Gazeti la New York Times la

# rajiwa nziza?





Meja Jenerali Evariste Ndayishimiye, katika nyendo zake za kisiasa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Marekani limeripoti tukio hilo kutoka Nairobi nchini Kenya, likimtaja mgombea urais mteule huyo kuwa ni 'Jenerali wa Jeshi'.

Kwa mujibu wa gazeti hilo, hatua hiyo inamaanisha kuwa Rais Nkurunziza atastaafu baada ya kipindi chake cha tatu kilichozua machafuko na kusababisha maelfu kuyakimbia makazi yao.

Ndayishimiye, anayetajwa kuwa rafiki wa karibu wa Rais Nkurunziza, amekuwa akikitumikia chama tawala cha CNDD-FDD katika nafasi ya katibu mkuu. Miaka kadhaa iliyopita, Ndayishimiye alijiondoa kutoka Chuo Kikuu na kuwa mpiganaji wa waasi akiwa pamoja na Nkurunziza.

Mwandishi na mchambuzi wa masuala ya siasa wa Burundi, David Gakunzi, anamtaja Ndayishimiye kuwa ni 'mtu asiyetabirika'.

"Kwa mfano, hivi karibuni alimpinga Nkurunziza katika nia yake ya kuwania urais kwa muhula wa tatu, lakini baadaye akabadilisha fikra zake na kumuunga mkono kiongozi huyo wa nchi," Gakunzi anasema.

Nkurunziza aliingia madarakani mwaka 2005 kutokana na kusainiwa kwa makubaliano ya amani ya Arusha yaliyomaliza vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyodumu kwa miaka 13 vilivyosababisha vifo vya zaidi ya watu 300,000.

Alichaguliwa tena bila kupingwa mwaka 2010 baada ya vyama vya upinzani kususia uchaguzi mkuu wa mwaka huo. Pia, alitangaza kuwa na haki ya kuwania uchaguzi mkuu wa 2015 ikiwa ni mara

> Kwa mfano, hivi karibuni alimpinga Nkurunziza katika nia yake ya kuwania urais kwa muhula wa tatu, lakini baadaye akabadilisha fikra zake na kumuunga mkono kiongozi huyo wa nchi.



Rais Pierre Nkurunziza, anayetarajiwa kuacha kiti mwaka huu, baada ya kutumikia vipindi vitatu.

ya tatu, lakini wanasheria wake wakasema uchaguzi wa kwanza haukujumuisha raia wote bali watunga sheria.

Ushawishi wa Nkurunziza unaweza kuendelea nchini humo hata baada ya uchaguzi mkuu, kwa vile atakuwa kiongozi mkuu baada ya kujiuzulu, kwa mujibu wa muswada ulioidhinishwa na serikali.

Mwaka 2018, chama tawala cha CNDD-FDD kilimtangaza Nkurunziza kuwa 'kiongozi mkuu wa milele', lakini ikakosolewa zaidi na baadhi ya raia wa nchi hiyo.

"Nkurunziza atarudi tu, hawezi kwenda mbali. Atakuwa anafanya kazi kupitia mlango wa nyuma akijaribu kuilinda familia na utajiri wake," anasema Charles Nditije, waziri wa zamani ambaye kwa sasa yupo kamhio ya upinzani.

"Hapatakuwa kamwe na uchaguzi mkuu huru na wa haki, uchaguzi utakaofanyika utatoa fursa tu ya kumpata Rais mpya," anasema, akifafanua kwa kulaumu: "Serikali haiheshimu haki za binadamu na wakala wa usalama wanaua watu huku wakilindwa."

Shutuma za kushamiri vitendo vya ukiukwaji haki za binadamu. vilisababisha Burundi kujitoa katika uanachama wake wa ICC. Serikali ya Burundi imekanusha mara kadhaa shutuma hizo na kwamba zinazowalenga baadhi ya watu.

Burundi, moja ya nchi masikini duniani, bidhaa yake nje ya nchi ni kahawa na inategemea zaidi misaada ya kigeni, iliyopunguzwa kutokana na machafuko ya kisiasa yaliyoikabili nchi hiyo.

Kabla ya uteuzi wa Ndayishimiye, Nkurunziza alisikika akitamka kwamba serikali yake hivi sasa ipo kwenye njia nzuri ya kidemokrasia.

"Tumefanikiwa katika mambo mengi. Mungu yu pamoja nasi," Nkurunziza alisikika akiwaambia wafuasi wa chama chake cha CNDD-FDD.

Ndayishimiye anatajwa na vyombo vya habari, kuwa mmoja wa wanasiasa maarufu nchini humo na rafiki wa karibu wa Nkurunziza.

## HISTORIA YAKE

Aizaliwa mwaka 1968 huko Giheta katika jimbo la Gitega. Tangu Agosti 20, 2016, alikuwa Katibu Mkuu wa CNDD-FDD.

Mwaka 1995, alinusurika machafuko yaliyowalenga wanafunzi wa Kihutu katika Chuo Kikuu cha Burundi kutoka kwa rafiki zao wa kabila la Watutsi.

Kwa haraka zaidi, alijiunga CNDD-FDD iliyochukua 'mkondo wa bunduki' baada ya mauaji ya aliyekuwa Rais wan chi hiyo, Melchior Ndadaye mwaka 1993.

Katika kipindi cha zaidi ya muongo mmoja wa mapigano ya wenyewe kwa wenyewe, Ndayishimiye akiwa Meja Jenerali aliteuliwa kuwa kamanda katika majimbo tofauti na hatimaye kushikawadhifa kwenye ofisi iliyowajibika mipango ya kisiasa kwenye vita.

Mwaka 2003, wakati CNN-FDD iliposaini mkataba wa amani wa kusitisha mapigano, Ndayishimiye akawa Naibu Mkuu wa Utumishi wa Umma.

Kati ya mwaka 2006 na 2007, aliteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Ni baada ya kuwa kiongozi wa baraza la kijeshi la Rais, nafasi aliyoitumikia hadi mwaka 2014 alipochukua nafasi hiyo katika baraza la kiraia.

***Makala hii imeandaliwa kutoka vyanzo mbalimbali vya mtandao.***

DIRA YA UCHAGUZI

# Somo la Ngawaiya, upenyo sahihi kuwanasa viongozi bora Oktoba



Thomas Ngawaiya. **NA MPIGAPICHA WETU**

**Na Sabato Kasika**

TANZANIA mwaka huu imo katika orodha ya nchi za Kiafrika zinazotarajia kufanya uchaguzi mkuu. Nyingine ni majirani Burundi na Ethiopia.

Kwa kurejea nchini, uchaguzi huo utafanyika mwishoni mwa mwaka ukihusisha kupata viongozi wawakilishi wa wananchi katika ngazi za udiwani, ubunge na urais.

Mchakato unaoendelea sasa kabla ya uchaguzi, ni uandikishaji watu katika Daftari la Kudumu la Wapigakura, ukiambatana na mengine kama utoaji elimu ya mpiga kura. Filimbi ya kampeni bado haijapulizwa na wagombea hawajajulikana, zaidi ya minong'ono.

Katika dhana ya utoaji elimu kitaifa, unahusisha wengi, kila mmoja kwa nafasi yake, kuanzia na wadau wa kiserikali, wanazuoni na wanasiasa.

Hapo ndiko kulijitokeza jina la Thomas Ngawaiya, ambaye kisiasa ameshawahi kuwajibika katika kambi ya upinzani, vyama vya TLP na NCCR - Mageuzi, kisha akatua ulingo wa chama tawala - CCM na sasa amejisogeza katika Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (Cegodeta), anayoiendesha kwa miaka kadhaa.

Akitumikia wajibu wake wa sasa na uzoefu, ukiwamo ubunge wa kuchaguliwa, Ngawaiya katika mazungumzo yake na Nipashe wiki hii, anawapa somo la kupata viongozi bora katika uchaguzi huo, kwa kuangalia mambo kadhaa.

> “Hivyo, ni muhimu kuhakikisha kwamba tunawapata bila kujali vyama, ili mradi ana uwezo wa kuongoza, basi wananchi wamshawishi awanie uongozi hata kama utakuwa ni urais.

Kwanza, anasema wapigakura wa Kitanzania na wanaopitisha wagombea, wanatakiwa kuanza kuchunguza namna ya kupata watu wanaofaa kuwaongoza, kisha wawashawishi, ili wakati ukifika uwe wa kuchukua fomu za kuwania uongozi na kujitosa katika kampeni.

Ngawaiya, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Cegodeta, anawataka wahusika wasisubiri hatua za mwisho ndipo wanafanya mchakato unaotakiwa, kwani wanaweza kujikuta wanachagua wasiofaa na kuishia kulalamika.

Mwendelezo wa mazungumzo yao walikuwa ya namna hii, katika mfumo wa maswali ya mwandishi, yaliyojibiwa na Ngawaiya. Fuatilia:

**SWALI: Umeona tatizo gani kwa viongozi waliopo hadi kufikie hatua ya kushauri wananchi kuchunguzana, ili kupata watu sahihi wa kuwashawishi wawanie uongozi katika uchaguzi ujao?**

**JIBU:** Maana yangu ni kwamba, kila unapofanyika uchaguzi, watu wengi huwa wanajitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi, wakiwamo hata wale wasiofaa kuongoza, ili mradi tu wachaguliwe.

Lakini, ninadhani sasa wananchi wanatakiwa kujiongeza kwa kuwaepuka wale wasiofaa. Njia nzuri ni kuchunguzana wenyewe kwa wenyewe mapema, ili kama miongoni wamo wanaofaa, basi wawashawishi kuwania udiwani, ubunge na hata urais.

**SWALI: Unawataka Watanzania waanze kuchunguza watu wanaofaa kuongoza ili hatimaye wawashawishi wachukue fomu kuwania uongozi. Ni njia ipi itakayotumika katika uchunguzi huo?**

**JIBU:** Kila sehemu tunayoishi tunafahamiana. Hivyo, ni rahisi kutambua kwamba mtu fulani anafaa kuwa diwani au mbunge, kwa sababu tunaishi naye au tunamfahamu. Ukiwepo mtu akashawishiwa akakubali, itakuwa ni rahisi kupata kiongozi bora, kutokana na ukweli kwamba maisha yetu yanategemea uongozi bora.

Hivyo, ni muhimu kuhakikisha kwamba tunawapata bila kujali vyama, ili mradi ana uwezo wa kuongoza, basi wananchi wamshawishi awanie uongozi hata kama utakuwa ni urais.

**SWALI: Taasisi yako inashauri Watanzania waanze kuchunguza watu wanaofaa ili wawashawishi wawanie uongozi, lakini kumbuka hata kama wanachukua fomu, ni lazima wapitie kwenye mchakato wa kura za maoni, katika vyama wanavyopitia, inawezekana wakaachwa kwenye mchakato huo. Huoni kwamba bado ushawishi wao unaweza kukwama?**

**JIBU:** Kama ukifuatilia sana, utagundua kwamba Rais John Magufuli, anatambua umuhimu wa watu wanaofaa kuongoza na ndiyo maana anawateua watu kutoka upinzani, bila chama, ili mradi wana uwezo wa kuongoza.

Ninaamini kwamba, kama mtu amependwa na wananchi, halafu ameachwa kwenye kura za maoni, bado anaweza kuteuliwa kushika nafasi nyingine serikalini. Kimsingi, kama nilivyosema, maisha yetu yategemea uongozi bora bila kujali chama, hivyo katika jambo hili, nirudie kusema wananchi waanze uchunguzi au upelelezi ili kupata watu makini, ili wakati ukifika, wawaambie wachukue fomu bila kujali chama.

Nakuhakikishia kwamba Watanzania wakifanyia kazi ushauri huo na ushawishi wao ukazingatiwa, watapata viongozi bora na siyo bora viongozi, kwa kuwa mchakato wa kuwapata utakuwa umeanza mapema kuliko kusubiri hadi mwishoni na kujikuta wakiangukia hata kwa wale wasiofaa.

**SWALI: Wewe umewahi kuwa mbunge kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2000 hadi 2005. Je, ushauri wako huu kwa wananchi hauna uhusiano wowote na kujipigia debe kuwataka wakushawishi, ili mwisho wa siku uchukue fomu kuwania tena nafasi hiyo kwenye uchaguzi mkuu ujao?**

**JIBU:** Ndugu yangu, kila mtu ana haki ya kuwania uongozi ili mradi amekidhi vigezo. Lakini, kwenye suala hili la kuwataka wananchi kuanza kuchunguza watu wanaofaa kuwaongoza au kuwawakilisha kwenye ngazi za uamuzi, ushauri wangu hauna uhusiano wowote na hilo unalouliza.

Ninajua kwamba wananchi wa Moshi Vijijini wamekuwa wakinishauri nirudi kwenye kinyang'anyiro, lakini kwa kweli ninatamani kuona damu changa zikiongoza. Mimi nimefanya mambo mengi kuanzia serikalini na hata kwenye siasa, nimekuwa mbunge kwa miaka mitano, pia Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM Mkoa wa Kilimanjaro.

Ninaona, ipo haja ya kupumzika, ingawa pia siwezi kuzuia wananchi kutoa hisia zao kwangu, kwani wanatambua kuwa siasa haina umri. Lakini kikubwa zaidi kama nilivyosema, suala la kuanza mapema mchakato wa kuchunguza watu wanaoweza kuongoza na kuwashawishi wachukue fomu wakati ukifika, ni la msingi sana.

Hivyo, wito na ushauri wa Cegodeta kwa Watanzania ni kuanza mchakato huo mapema, kwa kutambua kuwa mwaka huu ni wa uchaguzi mkuu na muhimu kupata watu wanaofaa kuongoza, ili wakati wa uchaguzi mkuu wachague watu sahihi.

Taasisi hii ni mdau mkubwa wa utawala bora, ndiyo maana inasema hayo, ili kuwaandaa Watanzania kupata viongozi wanaofaa.



# Bosi TRA anena mifumo mapato

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

KAMISHNA Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Dk. Edwin Mhede, amesema kuimarishwa kwa mifumo ya ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kielektroniki kutaiwezesha serikali kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.

Aliyasema hayo juzi jijini Mbeya wakati wa kikao cha pamoja kati ya wafanyabiashara na maofisa wa TRA, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kwa ajili ya kutoa elimu kwa wafanyabiashara na kujadili matatizo wanayokabiliana nayo katika mifumo ya ulipaji kodi.

Alisema TRA ina mpango wa kuacha kutumia mfumo ghafi katika ukusanyaji wa kodi na kueleza kuwa baadhi ya mifumo ya kielektroniki waliyoanza kutumia imeleta ufanisi na matokeo chanya katika ukusanyaji wa mapato.

Alisema mifumo ya kielektroniki inayotumika sasa ni pamoja na kulipa kodi kwa njia ya simu, mashine ya kielektroniki (EFD), na kufanya mnada kwa njia ya mtandao na kwamba sababu za kuimarisha mifumo hiyo ni kutokana na mifumo ghafi kutokuwa rafiki katika kukusanya mapato.

"Matarajio yetu ni kwenda mbele, kwa sasa tunahitaji kuwa na Mamlaka ya Kiteknolojia huko mbele, hii njia ya kukusanya mapato kwa njia ghafi, na mfumo utasaidia hata kuimarisha ukusanyaji wa mapato katika nchi ambazo tunachangia kwenye ushuru wa forodha," alisema.

Hata hivyo, alisema mamlaka hiyo inatambua mchango mkubwa kutoka kwa wafanyabiashara na kusisitiza kuwa TRA sio adui wa mlipa kodi na kwamba itaendelea kutatua changamoto ambazo ni kikwazo cha kulipa kodi.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema kuna baadhi ya wafanyabiashara ambao wanachafua sifa za wenzao kutokana na vitendo vyao vya kugoma au kuwashawishi wengine kutolipa kodi halali ya serikali.

Alisema katika siku za nyuma kuna baaadhi ya wafanyabiashara kwa makusudi walikuwa wakiwahamasisha wenzao kufunga biashara zao kama njia ya kuishinikiza serikali kupunguza au kufuta tozo mbalimbali na kueleza kuwa watu wa aina hiyo watashughukiliwa kwa mujibu wa sheria.

"Miaka ya nyuma Mkoa wa Mbeya ulikuwa si rafiki kwa biashara kutokana na baadhi yao kugoma kufungua maduka hususani katika eneo la Sido na Mwanjelwa, sasa nakuambia Kamishna (Dk. Mhede) siku wakifunga nitapeleka askari pale, wafunge hata miezi sita, maana huo ni uhuni," alisisitiza.

# Wauza viuatilifu hatarini kupata athari za kiafya

**Na Nebart Msokwa, RUNGWE**

BAADHI ya wauzaji wa maduka ya viuatilifu mkoani Mbeya, wako hatarini kupata matatizo ya kiafya kutokana na kutozingatia kanuni na sheria za uendeshaji wa maduka hayo ambazo wanafundishwa na serikali.

Aidha, kutokana na tatizo hilo baadhi ya maduka hayo yako hatarini kuteketea kwa moto endapo moto utalipuka kutokana na baadhi ya viuatilifu hivyo kuwa na uwezo wa kuchochea moto, lakini wauzaji hao hawana vidhibiti moto.

Hayo yalibainika juzi wakati maofisa wa Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu Tanzania (TPRI) ilipofanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye maduka kwa ajili ya kuona namna wakulima wanavyohudumiwa na wafanyabiashara hao.

Mkaguzi wa TPRI Nyanda za Juu Kusini, Emmanuel Mausa, alisema kwenye ukaguzi huo walibaini ukiukwaji mkubwa wa kanuni za uendeshaji wa maduka hayo ambazo wamekuwa wakifundishwa mara kwa mara.

Alisema walibaini baadhi ya wauzaji wa maduka hayo wana tabia ya kula chakula wakiwa ndani ya maduka hayo hali ambayo ni hatari kwa afya zao kwa madai kuwa viuatilifu hivyo asilimia kubwa ni sumu ambazo ni hatari.

Alisema katika ukaguzi huo pia walibaini kuwa baadhi ya wauzaji wa maduka hayo hawajawahi kuhudhuria mafunzo yanayotolewa na taasisi hiyo na kwamba ndio maana wanafanya kazi bila kuzingatia kanuni.

"Tumewafundisha kuwa na vifaa kinga kwa ajili ya kujikinga na athari za viuatilifu na pia tumewafundisha kuwa na vifaa vya kuyakinga maduka yao dhidi ya moto, lakini hawazingatii kabisa na hii ni hatari kwa wao wenyewe kiafya na maduka yao," alisema Mausa.

Alisema baadhi ya viuatilifu hivyo vina madhara ya taratibu ambayo hawawezi kubaini mapema na hivyo wanaweza wakawa wanadhani wako salama kumbe wanapata madhara.

Baadhi ya wauzaji wa maduka hayo walikiri kuwa vifaa vya kuvaa kwa ajili ya kujikinga na sumu za viuatilifu wanavyouza wanavyo, lakini hawavitumii ipasavyo kwa sababu ya kutojua vizuri madhara wanayoweza kupata.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Tumaini Mwakatwira, alisema wakati mwingine baadhi ya wamiliki wa maduka hayo wanawatumia hata watu ambao hawana mafunzo kutokana na gharama kubwa za mafunzo wanazotozwa na TPRI.

Mwakatwira alisema hivi karibuni walienda kupata mafunzo hayo mkoani Iringa na wakaambiwa gharama za mafunzo hayo zimepanda kutoka Sh. 320,000 mpaka Sh. 400,000, hivyo baadhi wakashindwa kuwapeleka wauzaji wao.

"Mitaji yetu ni midogo sana kwa hiyo ukinyofoa Sh. 400,000 ukampeleka mtu huko inakuwa ni shida tena kwa hiyo tunaomba haya mafunzo watupunguzie gharama," alisema Mwakatwira.

Hata hivyo, alikiri kuwa mafunzo hayo huwa ni muhimu kwao pamoja na wateja wao kwa maelezo kuwa afya ni muhimu kuliko fedha wanazotafuta.

Naye Emmanuel Maganga Maganga, ambaye alikutwa anauza duka bila kuwa na mavazi ya kujikinga alisema mavazi hayo anayo pamoja na vifaa vingine lakini huwa anajisahau kuvitumia.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Majaliwa Mwalembe, alisema wauzaji wa viuatilifu wasiozingatia kanuni za biashara hiyo wanaweza kupata athari kubwa ikiwamo magonjwa ya saratani na mifumo wa kupumua.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Bosco Mwanginde, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Sangambi, wakati wa mkutano wa hadhara uliokuwa umeitishwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Maryprisca Mahundi, kutatua mgogoro wa eneo la kuchimba kati ya wanakijiji na wawekezaji. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Walimu wachangia ujenzi sekondari

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

BAADHI ya walimu wa shule mbalimbali za Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ambao wameunda Jukwaa la Wazalendo, wamechangia mifuko 15 ya saruji katika Shule ya Sekondari ya Usongwe kwa ajili ya kuunga mkono jitihada za wananchi wa Kata ya Utengule-Usongwe kwenye ujenzi wa vyumba tisa vya madarasa.

Aidha, walimu hao walisema wameshatafuta wadhamini wa ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuwaunga mkono ambapo watasaidia tena shule hiyo pamoja na shule zingine za halmashauri hiyo.

Shule ya Sekondari ya Usongwe ambayo ipo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi inakabiliwa na upungufu wa vyumba tisa vya madarasa kwa ajili ya wanafunzi 400 wa kidato cha kwanza ambao wamechaguliwa kuanza katika shule hiyo.

Mmoja wa walimu hao, Benard Kasambala, alisema wananchi wa Kata hiyo ya Utengule-Usongwe wameonyesha jitihada kubwa kwenye ujenzi wa vyumba hivyo na ndio maana hata wao wameguswa kuwasaidia.

Alisema lengo lao ni kuisaidia serikali pia kwenye maeneo ambayo inakwama hasa kwenye ukarabati na ujenzi wa miundombinu mipya kwenye shule mbalimbali.

"Hawa wananchi wana moyo wa ajabu sana, wanafanya mambo ambayo hayakutarajiwa hasa kwa kipindi kama hiki, sisi leo tumeleta mifuko hii ya saruji, lakini tunaahidi kuja tena kuleta vitu vingine na tunataka watoto wasome katika mazingira rafiki," alisema Kasambala.

Alisema wao ndio wanajua ugumu wa kufundisha wanafunzi katika mazingira ambayo sio rafiki na kwamba ndio maana wameamua kushiriki kwenye ujenzi wa vyumba hivyo vya madarasa.

Kwa upande wake, Mwalimu Edson Sanga, alisema kwa kipindi hiki ni lazima yatokee matatizo ya upungufu wa vyumba vya madarasa kutokana na watu wengi kuitikia Sera ya Elimu bila malipo kwa kuwapeleka watoto wao shuleni.

Alisema sera hiyo ni nzuri, lakini uhaba wa vyumba vya madarasa ni tatizo la muda ambalo itafika wakati ambapo vitakuwa vinatosheleza na wengi watafurahia.

Kaimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Usongwe, Mwalimu Tusamile Kyejo, aliwashukuru walimu hao kwa msaada huo na kuomba wadau wengine pia kujitokeza kuwasaidia ili wafanikishe mapema ujenzi wa vyumba hivyo.

Alisema vyumba hivyo vikikamilika mapema hata wanafunzi waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hiyo wataanza masomo mapema.

"Tunawaomba walimu hawa waendelee na moyo huo wa kuiunga mkono serikali kwenye ujenzi wa miundombinu ya elimu, kazi waliyoifanya ni kubwa mno na huwa sio kitu cha kawaida walimu kufanya hivyo," alisema Kyejo.





# W'shara waaswa uvamizi maeneo

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

WAFANYABIASHARA wa masoko ya Jiji la Dodoma, wameshauriwa kuhakikisha wanayatumia maeneo yao yaliyotengwa ipasavyo, ili kuepukana na athari zinazoweza kujitokeza wanapovamia maeneo yasiyo rasmi.

Ushauri huo ulitolewa na ofisa masoko wa jiji hilo, James Yuna, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu masoko yaliyopo kwenye maeneo ya Jiji ambayo wafanyabiashara hawayatumii na badala yake wamekuwa wakipanga bidhaa zao barabarani na maeneo yasiyo rasmi hali ambayo inahatarisha usalama wao, tena na bidhaa zao.

Yuna alisema kuwa Jiji la Dodoma ni moja kati ya halmashauri zenye miundombinu mizuri na ya kisasa hasa kwa upande wa masoko, ambapo karibu kila eneo kuna soko ambalo wafanyabiashara wanaweza kulitumia kujipatia kipato, lakini hali imekuwa tofauti kwani badala ya wateja kufuata mahitaji sokoni wamekuwa wakifuata barabarani .

"Jiji la Dodoma lina Kata 41, mpango wa jiji kila kata inapaswa kuwa na soko na ni kata chache ambazo bado hazina... tayari Halmashauri ilishatenga maeneo hayo, katikati ya mji tuna masoko 12 ambayo yanafanya vizuri, na kuhudumia wateja wengi ikiwemo soko la Bonanza linalohudumia wananchi kwa upande wa matunda, mbogamboga, mahindi mabichi na samaki wabichi."

"Pia tunalo soko la Majengo ambalo ndio kongwe zaidi na mengineyo ambayo yanafanya kazi chini ya usimamizi wa ofisi ya Mkurugenzi, ambapo mfanyabiashara anatakiwa kuandika barua ya kuomba eneo na kisha atapatiwa majibu kama eneo lipo na atapewa," alosema na kuongeza:

"Lakini kumekuwa na changamoto kubwa ya maeneo rasmi ya masoko kutokutumiwa na badala yake wanatumia kupanga biashara zao barabarani na kuathiri utendaji kazi wa maeneo hayo."

"Ukipata eneo la kufanyia biashara fanya wewe mwenyewe na endapo utashindwa toa taarifa kwa mamlaka husika, na libaki kuwa wazi ili mfanyabiashara mwingine anayehitaji kulitumia apatikane na apangishwe," alieleza.

Aliwataka wafanyabiashara pia kuhakikisha wanatoa taarifa sehemu husika endapo wanapobaini kuwapo kwa vitendo vinavyokiuka na sheria na kanuni za Halmashauri ya jiji kama vile kwa wenye tabia ya udalali ambao unaoendelea kwenye masoko na maeneo ambayo wanayofanya biashara ikiwamo barabarani na yasiyo rasmi.

# Walimu, serikali sasa watafuta mwarobaini utoaji mafunzo awali

**Na Godfrey Mushi, DODOMA**

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT) kwa kushirikiana na wataalamu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), wameanza kutafuta mwarobaini wa kudhibiti na kuboresha huduma ya utoaji wa mafunzo ya awali nchini.

Jana, Mkuu wa Idara ya Elimu na Mafunzo wa CWT, Stella Kiyabo, akizungumza katika kikao cha uwasilishaji wa mwongozo wa umahiri wa mwalimu wa elimu ya awali kwa viongozi hao wa wizara, alisema katika utafiti uliofanywa na CWT na Shirikisho la Vyama vya Walimu Duniani, waligundua kuna upungufu kwenye utoaji wa mafunzo ya awali.

"Mpango huu utasaidia kuleta chachu kwa maeneo mengine kupeleka walimu kupata mafunzo haya kote nchini, kupata walimu mahiri wenye taaluma ya elimu ya awali. Tumegundua hakuna mwongozo wa kitaifa wa elimu ya awali unaozungumzia umahiri wa walimu wa awali.

"Kwa maana ya kwamba walimu wengi walikuwa hawana mafunzo ya awali lakini kwa wingi wa shule za awali tulizonazo nchini, shule nyingi zilikuwa zinafundishwa na watu ambao hawana elimu ya awali na kwa sababu hiyo basi, CWT ikatengeneza mradi ambao ni kutoa Diploma ya elimu ya awali na tumejiekeza tutajikita katika wilaya mbili za majaribio ambazo ni Chemba na Mpwapwa."

Kwa mujibu wa Kiyabo, mpaka sasa kuna walimu wanafunzi 436 ambao wanaendelea na mafunzo hayo, na kwamba CWT ilibaini kuwa walimu waliokuwa wanafundisha elimu ya awali, hawakuwa na elimu ya kufundisha elimu ya awali.

"Sisi kama CWT tunaona ni wajibu wetu kuisaidia serikali kwenye kuhakikisha kwamba tunaona nafasi zinazojitokeza katika masuala ya elimu lakini mwisho wa siku tuchukue hatua ni namna gani tunaweza kusaidiana na serikali kuziba zile gapes (nafasi) kwa lengo la kuhakikisha elimu ya nchi hii inakuwa bora zaidi na hasa tukilenga katika elimu ya awali.

Zaidi Kiyabo alieleza: "Tunategemea akiwa na elimu anapoanza basi vizuri ni rahisi kujiendeleza katika madarasa yanayoendelea, lakini niwashukuru ndugu zangu kutoka wizara ya elimu kwa kutupa ushirikiano mkubwa sana."

Aidha, Dk. Theresia Shavega ambaye ni Mkuu wa Kitivo cha Elimu na Mtaalamu wa elimu ya awali wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) alisema wao ndio waendeshaji wa mafunzo hayo kwa sababu ndio waliopewa dhamana ya kuandaa mitaala, kufundisha, mitihani na tathmini yote na wao ndio watakao wahudhurisha na kuwapa stashahada ya elimu ya awali.

Kwa upande wake, Ofisa Usimamizi wa Elimu katika Idara ya Elimu ya Awali na Msingi wa Ofisi ya Rais (Tamisemi), Salvatory Alute, alisema kinachofanyika hivi sasa ni kuandaa miongozo ya kuendeleza au kuinua kiwango cha ufundishaji wa elimu ya awali kwa kuwa na miongozo na mafunzo ya umahiri.



Baadhi ya wananchi wakipata huduma ya msaada wa kisheria kwenye banda la Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), katika maadhimisho ya Wiki ya Sheria kwenye viwanja vya Nyerere Square, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Jaji Mkuu aagiza utoaji elimu ya sheria

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, amewaagiza watendaji kuhakikisha wanatoa elimu ya sheria kwa wananchi kabla ya kuanza kufanya operesheni ya kuwazungukia katika maeneo yao ya biashara au wanayofanyia ili kupunguza kero.

Hayo yalisemwa na Jaji Mkuu wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Sheria uliofanyika hivi karibuni ambayo iliendana na matembezi ya kilomita tano kwa wafanyakazi kutoka idara mbalimbali.

Prof. Juma alisema mtumishi wa umma anayeenda kutekeleza sheria kwa operesheni hatufai kwa sababu anapaswa kutoa elimu ndio aendelee na operesheni kwa mwananchi ambapo hapo asipotekeleza ndio anapaswa kumchukulia hatua za kisheria.

Alisema sheria inapaswa iwekwe katika mizani sawa ili ziweze kufanya kazi katika mizani sawa, hivyo katika wiki hii hivyo vyote vinapaswa kufanyika ili kutoa nafasi kwa wananchi kuelewa nini maana ya sheria.

"Naomba watendaji mjitahidi kutoa elimu kwa wananchi hususani katika wiki hii ya sheria, tunahitaji kuona wananchi wote wanapata mwanga kuhusiana na sheria," alisema Jaji Prof. Juma.

Alisema ni jukumu lao watendaji kuhakikisha wanatoa elimu kwa wananchi jambo ambalo litawasaidia kujua haki zao za msingi pale wanapokuwa wanakesi katika mahakama mbalimbali.

"Wananchi wakijua sheria itakuwa rahisi kuendesha vitu vyao bila kukumbana na vikwazo vya utoaji rushwa, " alisema.

Alisema siku ya uzinduzi wa wiki ya sheria ni muhimu kwa taifa kwa sababu inasaidia kuwakumbusha watu nini maana ya sheria na kila mmoja anapaswa kujua na kuitekeleza.

Prof. Juma alisema sheria ni muhimu ifuate ili watu waweze kuishi kwa amani na utulivu kama ilivyo kawaida ya Taifa letu hivyo ni muhimu kuzingatia.

"Jamii inapaswa kuwa mstari wa mbele kufuata sheria hivyo wiki hii ya sheria wataendelea kutoa elimu ya sheria ikiwemo kujua umuhimu wa sheria na faida Zane, " alisema Prof. Juma.

Alisema sheria lazima ziwe na malengo ya dira ya mwaka 2025 ambayo ni uboreshaji wa hali ya maisha ya wananchi, usalama, amani na umoja pamoja na utawala bora.

Alifafanua zaidi ya kuwa sheria inapaswa kuwawezesha wananchi kupata elimu ya kujua umuhimu wa sheria, kujua elimu ya uchumi ili waweze kushindani na nchi nyingine na kuongeza ni lazima watu waijue.

Jaji Mkuu alisema sheria zinazotungwa lazima ziweke mazingira wezeshi kwa wananchi.

"Siku si zote tujiulize wananchi maskini watarajie nini katika sheria," alisema.

Alisema wakifanya hivyo, sheria watakazotunga zitakuwa na msukumo wa kimapinduzi ambazo zitawawezesha kuwa na uwezo wa kushindana.

# Balozi Iddi ataja zawadi bora CCM

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAKAMU wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, amesema zawadi nzuri ya siku ya kuzaliwa kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ni kuhakikisha inashinda katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu na kuongoza dola.

Balozi Iddi alisema hayo jana alipokabidhi vifaa mbalimbali katika Jimbo la Amani Mkoa wa Mjini Magharibi ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Alisema CCM ilizaliwa Febuari 5, 1977 ikiwa na malengo na madhumuni ya kushika dola kwa kushinda uchaguzi mkuu kila unapofanyika.

Kutokana na ukweli huo, alisema CCM haiwezi kushinda katika uchaguzi kama viongozi waliopewa dhamana, wakiwamo wabunge na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watashindwa kutekeleza ilani na ahadi zao kwa wapigakura.

"Nimefurahishwa na kazi nzuri iliyofanywa na wabunge na wawakilishi katika Jimbo la Amani. Utekelezaji wa ilani umefikia asilimia 90," alisema.

Alisema mwelekeo wa CCM katika uchaguzi mkuu ni kuhakikisha inashinda majimbo yote ya Mkoa wa Mjini Magharibi.

"Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Mjini Magharibi mhakikishe uchaguzi mkuu ujao CCM inashinda katika majimbo yote ya mkoa huu," alisema.

Naye Mbunge wa Amani, Mussa Hassan Mussa, alisema kero zote zilizokuwapo katika jimbo hilo zimepatiwa ufumbuzi ikiwamo suala la majisafi na salama.

"Utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020 umefikiwa kwa asilimia 90 katika maeneo yote muhimu ikiwamo miradi ya jamii na maendeleo," alisema.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Amani, Rashid Ali Juma, alisema katika utekelezaji wa ilani ya uchaguzi wamejikita katika kusimamia miradi ya ujenzi wa shule, vituo vya afya na barabara za ndani kwa kiwango cha kifusi.

Alisema wametumia zaidi ya Sh. milioni 325 kupitia katika Mfuko wa Mbunge na Mwakilishi pamoja na kutumia fedha zao binafsi.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mjini Magharibi, Talib Silima, alisema wameridhishwa na utekelezaji wa ilani kwa viongozi wa Jimbo la Amani ikiwamo kuzipatia changamoto matatizo yanayowakabili wananchi.

"Ushindi wa Chama Cha Mapinduzi uko katika utekelezaji wa ilani ya chama kwa kuzipatia ufumbuzi kero zinazowakabili wananchi ambao ndio wapigakura," alisema.



Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Unguja Ukuu, wakiwa katika harakati za kusafisha samaki ili kupata fedha za kujikimu kimaisha katika soko la mnada wa samaki la kijiji hicho, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ataka sheria zitafsiriwe lugha nyepesi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WIZARA ya Katiba na Sheria imeziagiza taasisi zake kuhakikisha sheria zote zinazowasilishwa katika Baraza la Wawakilishi zinatafsiriwa kwa lugha nyepesi ya Kiswahili ili wananchi kuweza kuzifahamu sheria hizo.

Akizungumza na waandishi wa habari Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, George Kazi, alisema yako malalamiko mengi kutoka kwa jamii kwamba sheria zinazopitishwa katika vyombo vya kutunga sheria na zinazotumika mahakamani hazifahamiki vizuri kwa wananchi.

Kazi alisema sheria hizo hazifahamiki vizuri kwa sababu zinaandikwa kwa lugha ya Kiingereza na miswada yake wakati walengwa wake wanatumia Kiswahili.

"Tumeyapokea malalamiko kutoka kwa wananchi na tumeanza mchakato wa kuzipitia sheria zote muhimu kwa kuzitafsiri kwa lugha ya Kiswahili pamoja na miswada yake," alisema.

Alisema sheria ya kwanza ambayo imetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili ni muswada wa marekebisho ya kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi.

Pia alisema wizara imechukuwa hatua ya kuitafsiri sheria hiyo kutokana na umuhimu wake huku mswada wa Mahakama ya Kadhi ukigusa sehemu kubwa ya jamii.

"Mswada wa Mahakama ya kadhi tumeutafsiri kwa lugha nyepesi ya Kiswahili kwa lengo la kuwawezesha wananchi wengi kuifahamu. Sheria hiyo inagusa sehemu kubwa ya jamii," alisema.

**"Tumeyapokea malalamiko kutoka kwa wananchi na tumeanza mchakato wa kuzipitia sheria zote muhimu kwa kuzitafsiri kwa lugha ya Kiswahili pamoja na miswada yake," alisema.**

# Wahitimu sekondari wapewa ufunuo

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAHITIMU wa kidato cha nne wametakiwa wasitosheke na ufaulu walioupata bali waongeze bidii katika masomo yao ili kufikia malengo yao ya baadaye.

Hayo aliyasema na mdau wa elimu Zanzibar, Dk. Abdalla Ismail Kanduru, katika mahafali ya Shule ya Sunni Madrassa Mkunazini Mjini Unguja wakati akikabidhi vyeti kwa wahitimu waliomaliza masomo yao ya kidato cha nne.

Alisema licha ya matokeo mazuri yaliyopatikana shuleni hapo, wanafunzi wazidishe juhudi katika masomo yao ya kidato cha tano kwa mustakabali wa maisha yao ya baadaye.

Wanafunzi wengi hivi sasa, alisema wanashawishika kuingia vyuoni na kukataa kusoma kidato cha tano na sita jambo ambalo si sahihi kwa kuwa sifa za kuingia chuo kikuu zimekuwa zikibadilika.

"Kila siku mambo yanabadilika, nashauri yule alifanikiwa kuingia kidato cha tano aendelee waache kukimbilia kwenye vyuo jambo ambalo si njia sahihi ya uamuzi," alisema Dk. Kanduru.

Aidha, aliwataka walimu na walezi kuzidisha ushirikiano katika usimamizi wa wanafunzi wao kwa lengo la kuongeza juhudi za ufundishaji na kuimarisha ongezeko la ufaulu wa wanafunzi hao

Naye Mwakilishi wa Rais wa Jamat, Murtaza Turk, alisema juhudi za walimu na walezi wa wanafunzi pamoja na wajumbe wa Bodi ya Shule hiyo zimeweza kusaidia ufaulu mzuri wa shule hiyo.

Alisema katika wanafunzi 70 wa kidato cha nne waliofanya mitihani, 10 wamepata daraja la kwanza, 13 daraja la pili, 22 daraja la tatu na daraja la nne 25.

Aidha, alisema kipindi cha mwaka jana kulikuwa na changamoto kubwa kwa wanafunzi kutofaulu vizuri jambo ambalo lilichafua sifa nzuri ya shule hiyo.

# RC ashauri TRA mapitio ya mkataba mawakala wa EFD

**Na Innocent Ng'oko, MBEYA**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imetakiwa kufanya mapitio ya mkataba na kampuni zilizopewa dhamana ya kusambaza na kuuza mashine za kielektroniki ( EFD) kutokana na ufanisi mbovu wa mawakala hao katika kuwahudumia wateja.

Maagizo hayo yalitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliyekuwa mgeni rasmi katika kikao cha wafanyabiashara mkoa wa Mbeya ambacho kiliitishwa na Kamisha Mkuu wa TRA, Dk. Edwin Mhede, kwa lengo la kutoa elimu kwa wafanyabiashara kuhusiana na aina mbalimbali za kodi.

Alisema wengi wa mawakala hao wamekuwa ni wababaishaji, na kuna uwezekano mkubwa wakawa wanakwamisha jitihada za TRA na serikali kwa ujumla za kuhakikisha wafanyabiashara wanaokidhi vigezo vya kuwa na mashine hizo wanazipata kwa wakati.

Chalamila alisema kwa mkoa wa Mbeya pekee, amekutana na malalamiko ya wafanyabiashara ambao walikuwa wamelipia fedha kwa lengo la kupata mashine za EFD, lakini wamekuwa wakizungushwa na mawakala hao kwa muda mrefu bila ya kupewa mashine hizo.

Alisema mwishoni mwa mwaka jana, aliwatia ndani mawakala watatu wa mashine hizo kutokana na kubainika walikuwa wamechukua fedha za wafanyabiashara bila ya kuwapa mashine za EFD.

"Ndugu kamishna mimi kama mkuu wa mkoa niliwahi kukumbana na changamoto ya mmoja wa mawakala ambaye nilikuwa nimemlipa fedha zangu ili kupewa mashine ya EFDs, lakini jambo la kushangaza hata mimi nilizungushwa kwa muda wa zaidi ya miezi mitatu hadi meneja wa TRA mkoa wa Iringa alipoingilia kati," alisema Chalamila.

Pia alitoa onyo kwa wafanyabiashara hao kuacha ujanja ujanja katika mchakato wa kufanya biashara na kuwa maendeleo ya nchi yoyote duniani yanategemea kodi na kuwa ni lazima kila mwananchi alipe kodi.

Kwa upande wake Dk. Mhede alisema serikali inatambua mchango wa wafanyabiashara wa Mkoa wa Mbeya na mikoa mingine katika suala zima la kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo ya nchi. Alisema TRA kupitia kwa maofisa wake kuanzia ngazi ya juu hadi chini imejiwekea mkakati wa kushuka chini kwa lengo la kukutana na wafanyabiashara ili kusikiliza kero na changamoto zao katika ulipaji wa kodi ndani ya mamlaka hiyo.

Alisema kutokana na umuhimu wa kulipa kodi, ni lazima wafanyabiashara wajitahidi kulipa kodi ya mapato pamoja na kodi ya majengo kwa hiari licha ya kodi hizo kuwepo kwa mjibu wa sheria za nchini.



Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo, akikagua mtambo uliokuwa ukikarabati Mto Salasala jana, alipofanya ziara ya kukagua mito ambayo imeathiriwa na watu waliokuwa wakichimba mchanga. **PICHA: CHRISTINA MWAGALA**

## Ikungi kutumia bilioni 36.8/- kwa 2020/21

**Na Elisante John, IKUNGI**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Ikungi, mkoani Singida imepanga kutumia zaidi ya Sh. bilioni 36.8 kwa mwaka wa fedha 2020/2021, kwa ajili ya miradi ya maendeleo, mishahara na matumizi ya kawaida.

Katika mwaka wa fedha 2019/2020, halmashauri hiyo iliidhinishiwa na bunge zaidi ya Sh. bilioni 25.4 kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo na matumizi mengineyo.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Ikungi, Aika Masawe, akiwasilisha taarifa kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Justice Kijazi, alisema fedha hizo zitatokana na vyanzo vyake mbalimbali ikiwamo mapato ya ndani, ruzuku ya serikali, wafadhili, wahisani na wadau wa maendeleo.

"Katika bajeti hii zaidi ya Sh. 1.9 zitatokana na mapato ya ndani, zaidi ya Sh. bilioni 1.5 zitatokana na mapato halisi, Sh. milioni 426 za mapato na zaidi ya Sh. bilioni 34.8, ni ruzuku kutoka Serikali Kuu na wadau wengine mbalimbali," alifafanua.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Edward Mpogolo, aliwataka madiwani wote kusimamia vema makusanyo ya ushuru wa mazao, masoko na minada katika maeneo yao, ili baadaye yatumike kutekeleza miradi ya maendeleo.

"Pamoja na matatizo mnayokumbana nayo, naamini bajeti hii italeta mabadiliko makubwa ya maendeleo...watendaji, shirikianeni na madiwani ili baadaye wananchi wapate huduma bora, kupitia miradi ya maendeleo," alisema.

Akifungua mkutano huo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Ali Mwanga, alisema bajeti hiyo haitaleta mabadiliko, iwapo hapatakuwa na ushirikiano baina ya watendaji, madiwani, wataalamu na wakusanya ushuru.

Alisema ili kufikia dira ya maendeleo, halmashauri ya wilaya hiyo imejiwekea kipaumbele katika sekta ya elimu ya msingi na sekondari, afya, kilimo, mifugo, ardhi, mapato, maendeleo ya jamii, usafi na mazingira, na maliasili na nyuki.

**"Pamoja na matatizo mnayokumbana nayo, naamini bajeti hii italeta mabadiliko makubwa ya maendeleo...watendaji, shirikianeni na madiwani ili baadaye wananchi wapate huduma bora, kupitia miradi ya maendeleo," alisema.**

# Miradi viporo yawanyima usingizi madiwani

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MADIWANI wa Manispaa ya Shinyanga, wameeleza kusikitishwa uwapo na miradi mingi ya maendeleo viporo ambayo haijakamilishwa kwenye bajeti ya mwaka wa fedha uliopita (2019-20).

Wamesema kuwa hali ambayo wameingiwa hofu ya kukosa imani kwa wapigakura wao.

Madiwani walipaza kilio hicho kwenye kikao cha baraza wakati wa kujadili utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha (2019-20), kuwa kuna miradi mingi ya maendeleo ambayo ni viporo katika bajeti hiyo haijakamilishwa, hali ambayo inawakosesha amani kwa wapigakura wao.

Mmoja wa madiwani hao, Paulo Machela, alisema idadi kubwa ya miradi hiyo viporo yakiwamo maboma ya ujenzi wa shule, na huduma za afya, mingi ilijengwa kwa nguvu za wananchi, na kuwa serikali ilipaswa kuyakamilisha, lakini hakuna kinachoendelea, hivyo linawakosesha amani kwa wananchi.

"Tunaomba katika bajeti ya mwaka wa fedha ujao (2020-21), miradi ya maendeleo ambayo ni viporo hasa iliyojengwa kwa nguvu za wananchi, iingizwe ikamilishwe ili tuwe na imani na wananchi," alisema Machela.

Naye Diwani wa Kata ya Kambarage, Hassani Mwendapole, alisema miradi hiyo viporo imekuwa kero kwa wananchi ukiwamo wa ujenzi wa nyumba za walimu katika Shule ya Sekondari Mwasele, ambazo zimegeuka kuwa nyumba za wanafunzi na kupewa ujauzito.

Naibu Meya wa Manispaa ya Shinyanga, John Kisandu, aliagiza uongozi wa Manispaa kuwa hadi kufikia Juni mwaka huu, wajitahidi kupunguza idadi ya miradi hiyo viporo na ambayo haitakamilika iingizwe kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga Geofley Mwangulumbi, alisema tayari alishamwagiza mchumi wa manispaa hiyo Gwakisa Mwasheba, afuatilie miradi yote ambayo ni viporo yakiwamo maboma ili wawe na idadi yake kamili, na kuanza kufanyiwa kazi ikiwamo kuingizwa pia kwenye bajeti ijayo.

## HABARI KIMATAIFA

# Hong Kong yaripoti kifo cha kwanza corona

**BEIJING,** China

HONG Kong imeripoti kifo cha kwanza kilichotokana na virusi vya corona na Macau imeamuru kufungwa kwa kumbi za kuchezea kamari kwa muda wa wiki mbili.

Kufungwa kwa kumbi hizo ni mkakati wa China kupambana na kuzuwia kusambaa kwa ugonjwa ambao umekwisha ua zaidi ya watu 420 katika China.

Kifo cha kwanza mjini Hong Kong kutokana na virusi hivyo ni cha mtu mwenye umri wa miaka 39 ambaye aliugua ugonjwa huo na alitembelea mji wa Wuhan nchini China.

Chimbuko la kuzuka kwa ugonjwa huo Januari, mwaka huu ni kifo cha pili kutokana na ugonjwa huo wa virusi vya corona nje ya China baada ya mtu mwenye umri wa miaka 44 raia wa China kufariki nchini Ufilipino.

Hali hiyo imesababisha kuchochea kwa baadhi ya maofisa katika mji huo wa kibiashara katika eneo la Asia kufunga mipaka na China.

Idadi kubwa ya wafanyakazi wa hospitali wamekuwa katika mgomo kwa siku ya pili wakimtaka kiongozi wa Hong Kong, Carrie Lam kubadilisha uamuzi kuacha wazi vituo vitatu vya kuingilia nchini humo badala yake wakitaka kufugwa kabisa kwa mpaka na China.

**Wakati huo huo**, miji zaidi nchini China, ikiwa ni pamoja na mji uliokoa kilometa 175 kutoka Shanghai, imewekwa katika hali ya kufungwa jana, wakati athari za virusi vipya vya corona zikisambaa mbali zaidi ya sehemu ulikoanzia. **DW**

# Uchaguzi wa wabunge wapigwa kalenda

**CONAKRY,** Guinea

UCHAGUZI wa wabunge uliopangwa kufanyika Februari 16 nchini Guinea umeahirishwa hadi Machi 1, mwaka huu.

Rais wa nchi hiyo, Alpha Condé alitoa sheria ya kuahirisha uchaguzi wa wabunge, iliyopangwa awali kufanyika Februari 16, 2020, hadi wiki mbili zijazo, sheria ambayo haikuwashangaza wengi.

Sababu zilizotolewa kuahirishwa kwa uchaguzi huo ni vyama vikuu vya upinzani vilitoa wito kwa wafuasi wao kususia uchaguzi huo, ikifuatiwa na kujiondoa kwa maofisa saba wa tume ya uchaguzi (CENI), wakipinga dhidi ya usimamizi mbovu wa mchakato wa uchaguzi.

Sababu nyingine ni viongozi wa dini waliomba watawala wasimamishe maandalizi ya uchaguzi huo hadi wakati ambapo wadau wote katika mchakato huo watakapokutana kwa maandalizi ya uchaguzi wa huru, wazi, haki, wa kuaminika na usiyombagua yeyote. **RFI**

# Mahakama yatoa hati ya kukamatwa Jacob Zuma

**JOHANNESBURG,** Afrika Kusini

MAHAKAMA ya juu ya Pietermaritzburg nchini Afrika Kusini imetoa hati ya kukamatwa kwa aliyekuwa rais wa nchi hiyo, Jacob Zuma baada ya kushindwa kufika mahakamani kukabiliana na mashtaka kuhusu rushwa dhidi yake.

Zuma anakabiliwa na tuhuma za rushwa, ambazo zilimng'oa madarakani.

Zuma mwenye umri wa miaka 77, chama chake cha ANC kilimlazimisha kuachia madaraka Januari 2018. Aliwahi kupigiwa kura ya kutoamaniwa mara tisa katika bunge kabla hajaachia ngazi.

**Mshauri wake wa fedha wakati huo alikutwa na hatia ya kuomba rushwa hizo mwaka 2005 na Zuma alimfukuza kazi yake ya usaidizi wa Rais.**

Zuma anatuhumiwa kuomba rushwa kutoka kwa Thales kwa nia ya kuboresha maisha yake ya kifahari. Mshauri wake wa fedha wakati huo alikutwa na hatia ya kuomba rushwa hizo mwaka 2005 na Zuma alimfukuza kazi yake ya usaidizi wa Rais.



Mashtaka ya awali dhidi ya Zuma yalikuwa yameondolewa muda mfupi kabla ya kuwa Rais. Kwa sasa anakabiliana na shtaka moja la kusababisha ghasia, shtaka moja la rushwa na mashtaka 12 ya udanganyifu.

Urais wa Zuma ulitiliwa mashaka hata kabla ya kuingia madarakani mwaka 2009 kuelekea uchaguzi mkuu mwaka huo tayari Zuma alikuwa akikabiliwa na tuhuma za rushwa na ubakaji.

Zuma aliwahi kutuhumiwa kumbaka rafiki wa familia yake ambaye anaishi na virusi vya Ukimwi mwaka 2006, lakini licha ya ushahidi Zuma aliiambia mahakama kuwa aliogopa ili kujikinga na kupata virusi vya ukimwi ambavyo vingemwandama muda wote wa urais wake. **BBC**



Rais wa zamani wa Kenya, Daniel Arap Moi (kulia), enzi za uhai wake Desemba 28, 2002, muda mfupi kabla ya kuondoka madarakani. **PICHA: REUTERS**

# Rais zamani Kenya afariki na miaka 95

**NAIROBI,** Kenya

RAIS wa zamani wa Kenya, Daniel Arap Moi, amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 95.

Rais Uhuru Kenyatta ametangaza kifo hicho kilichotokea usiku wa kuamkia jana katika Hospitali ya Nairobi alikokuwa anapata matibabu.

Taarifa zinaeleza kuwa Moi alizaliwa Septemba 2, 1924, katika jamii ya wakulima katika eneo la Baringo, magharibi mwa Kenya.

Jina lake la kwanza lilikuwa Toroiticha Arap (mwana wa) Moi lakini baadaye akabatizwa katika Ukristo na kupewa jina la Daniel wakati huo akiwa mwanafunzi

Moi alikuwa Rais wa Kenya kuanzia mwaka 1978 hadi 2002, alikuwa mmoja wa mwanasiasa mashuhuri waliofanikiwa, akitoka jamii ndogo ya Tugen, mojawapo ya makundi yanayounganisha kabila kubwa la Wakalenjin.

Alianza kufanya kazi kama mwalimu mwaka wa 1945 katika shule ya African Government School na mwaka mmoja baadaye akiwa na umri wa miaka 22 akateuliwa kuwa mwalimu mkuu.

Machi 1957 Moi alikuwa mmoja wa watu weusi nane waliochaguliwa kuwa wanachama wa Bunge la ukoloni liitwalo LegCo. **BBC**

# Wanafunzi 15 wafariki dunia kwa kukanyagana

**NAIROBI,** Kenya

IDADI ya wanafunzi waliopoteza maisha baada ya kukanyagana katika Shule ya Msingi Kakamega nchini Kenya imefikia 15.

Mkuu wa kituo cha polisi cha Kakamega, David Kabena alisema kuwa wanafunzi wengine 39 walijeruhiwa na 20 wamepata matibabu.

Zaidi ya wanafunzi 100 wanatibiwa na wengine wako kwenye hali mbaya na kwamba idadi ya vifo inaweza kuongezeka.

Mkanyagano huo ulitokea baada ya kengele ya kumaliza masomo kupigwa na wanafunzi walikuwa wakitoka kuelekea nyumbani.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa wanafunzi hao walikuwa wakitoka katika madarasa yao majira ya saa 11 jioni wakati mkasa huo ulipotokea.

Imedaiwa kwamba baadhi yao walianguka kutoka ghorofa ya tatu ya jengo hilo walipokuwa wakitoka darasani.

# Jaji Mkuu ataka majaji kuandika muhtasari hukumu kwa Kiswahili

**Na Hellen Mwango**

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, ameshauri majaji kuandika muhtasari wa hukumu kwa lugha ya Kiswahili ili kuwasaidia waandishi wa habari kutoa tafsiri iliyosahihi kwenye kesi zenye maslahi kwa jamii.

Rai hiyo aliitoa juzi jijini Dar es Salaam wakati akifungua kongamano la siku mbili lililowahusisha majaji wa Tanzania na wa Uingereza katika wiki ya sheria nchini.

Alisema kongamano hilo limewafungua mambo mengi ikiwamo majaji wenzao kuweka utaratibu wa kuandaa muhtasari kwa kesi zenye maslahi kwa ajili ya waandishi wa habari.

"Mahakama ya Uingereza wameweka utaratibu wa kuandaa muhtasari kwa ajili ya waandishi wa habari tofauti na sisi hapa nchini... tukishasoma hukumu kila mwandishi anakwenda kuandika alichosikia, nashauri majaji wa hapa nchini kuanza utaratibu huo ili tafsiri iwe moja kwa vyombo vyote vya habari," alisema kiongozi huyo wa mahakama nchini na kuongeza:

"Nashauri hapa kwetu kila jaji anapaswa kubadilika kwa kuhakikisha kuwa baada ya kusoma hukumu kwa lugha ya Kiingereza, waandae muhtasari wa hukumu hiyo kwa lugha ya Kiswahili kwa lengo la kuielimisha jamii yote," alisema Prof. Juma.

Akifafanua zaidi alisema mbali na majaji kutoa muhtasari, pia majaji wanaongeza uzoefu wa namna ya kuandika hukumu na kuitoa kwa haraka pamoja na namna ya kuendesha kesi zenye maslahi kwa jamii.

Jaji Mkuu alisema ushirikiano huo utasaidia nchi zinazoendelea na zilizoendelea kufanya kazi pamoja kwa malengo ya kuzijengea uwezo mahakama zake na kwamba majaji wa Tanzania watapata fursa ya kwenda kujifunza Uingereza.

Naye Jaji Kiongozi, Dk. Eliezer Feleshi, alisema mafunzo hayo yataleta manufaa kwa kuipa mahakama uwezo katika utendaji na kufikia malengo waliyojiwekea.

Alisema mfumo wa mahakama nchini unaendana na wa Uingereza kwa sababu walipokuwa watawala walianzisha mahakama, hivyo taratibu mbalimbali zinaendana.



Mkuu wa Wilaya ya Kilolo, mkoani Iringa, Asia Abdallah (katikati), akiagana na timu ya wawekezaji wa kilimo cha mahindi cha Rutuba Farm, baada ya kubadilishana mawazo na kuelezea jinsi watakavyochangia kukuza kilimo nchini, walipomtembelea ofisini kwake jana. **NA MPIGA PICHA WETU**

# Muhimbili yapiga jeki shule ujenzi vyoo

**Na Mary Geofrey**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), Tawi la Mloganzila, imesaidia ujenzi wa choo chenye matundu 10 chenye thamani ya Sh. milioni 15 katika Shule ya Msingi Mloganzila.

Msaada huo ulikabidhiwa juzi na Mkurugezi Mtendaji wa MNH, Prof. Lawrence Museru, katika hafla iliyofanyika shuleni hapo wilayani Kisarawe mkoani Pwani.

Alisema lengo la kutoa msaada huo ni kushirikiana na jamii inayowazunguka katika kudhibiti magonjwa mbalimbali ya kuambukiza yanayoweza kuzuilika.

"Leo (jana) tumekuja kutoa msaada huu wa vyoo katika shule hii. Tumevijenga vya kisasa kwa thamani ya Sh. milioni 15. Hatua hii inamaanisha kuwa licha ya kuwa tunatoa tiba ya magonjwa mbalimbali, tuna wajibu wa kuwa na uhusiano mwema na majirani zetu kwa kuhakikisha wanakuwa salama," alisema Prof. Museru.

Aliwataka wanafunzi hao kuhakikisha wanavitunza vyoo hivyo ili viwasaidie kujikinga na maradhi yatokanayo na kukosa vyoo safi na salama kama kuumwa tumbo na kuhara.

Prof. Museru alisema ni wazi kuwa kukwapo kwa vyoo hivyo kutawasaidia wanafunzi kuongeza umakini katika kuzingatia masomo na kufanya vizuri.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, Zipora Simwanza, aliushukuru uongozi wa Hospitali ya Muhimbili tawi la Mloganzila kwa msaada waliotoa.

Aliwataka kuendelea kushiriki kutoa misaada mingine ya kusaidia jamii yenye mahitaji kama walivyofanya kwa shule hiyo.

Naye Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Geofrey Magembe, mbali na kuishukuru Muhimbili, alisema shule hiyo iliyoongoza kwa kufanya vizuri katika matokeo ya darasa la saba mwaka jana, katika Wilaya ya Kisarawe bado ina mahitaji ya matundu mengine 43 ya vyoo.

Alisema katika shule hiyo kuna uhitaji pia wa vyumba 19 vya madarasa hivyo aliitaka jamii kuendelea kushirikiana na kamati ya shule katika kusaidia kutoa elimu bora.

# Sido, Must wakubaliana teknolojia mpya

**Na Beatrice Philemon**

SHIRIKA la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), limesaini mkataba wa makubaliano ya ushirikiano na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) ili kupata teknolojia mpya ambazo zitaweza kutumika kwa wananchi kulingana na mahitaji yao ya biashara.

Malengo mengine ni kusaidia wanafunzi kupata uzoefu wa vitu walivyosoma darasani pamoja na kuboresha ujuzi wao na kuona vitu gani vinafanyika kwenye vituo hivyo.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mkuu wa SIDO, Prof. Sylvester Mpanduji, baada ya kusaini makubaliano hayo kati ya Sido na Must katika ofisi za makao makuu ya Sido.

Wakati wa utekelezaji, wanafunzi kutoka Chuo cha Must watafanya mafunzo kwa vitendo kwenye vituo vyao vya teknolojia vya Sido na kwenye vituo vya uendelezaji wa teknolojia na katika vituo vya mafunzo na uzalishaji bidhaa vya Sido.

Pia kufanya kwa vitendo mambo waliyosomea na wanafunzi wenye mawazo ya ubunifu na ambao wanataka kuanzisha viwanda kutokana na uzoefu wao, Sido itawachukua na kuwaingiza kwenye vituo vyao atamizi (incubation centres).

"Kwa upande wa teknolojia, teknolojia zote zitakazotengenezwa kwao, sisi tutazichukua teknolojia zao watakazokuwa wanazifanyia utafiti na tukiona kama zinafaa kutumika kwa jamii au wajasiriamali, Sido tutazichukua na kwenda kuzizalisha kwenye vituo vyetu vya teknolojia," alisema.

Pia kama kutakuwa na tatizo kwenye hizo teknolojia ambazo zitakuwa zinatumika kwa wananchi, Sido itazipeleka kwenye Chuo cha Must ili wapate utatuzi wa suala hilo au teknolojia hiyo.

Kadhalika, wahitimu wa chuo hicho watakaotaka kufanya biashara, watapata mikopo midogo midogo kulingana na mahitaji yao.

"Sisi kama Sido tuna kitengo cha mafunzo, tutakuwa pia tunapokea walimu kutoka Chuo cha Mbeya na kama wafanyakazi wangu watahitaji kupata mafunzo maalumu kuhusu teknolojia, watakuja kutufundisha ili kupata teknolojia mpya.

Sido imeamua kusaini mkataba huu baada ya kugundua kuwa wanafunzi wengi wanafanya utafiti na kubuni teknolojia za aina mbalimbali, lakini zinaishia kwenye makabati badala ya kwenda kwa wananchi.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**ANAHITAJIKA MUUGUZI**
Anahitajika muuguzi msaidizi au Nurse Assistant kwa anayehitaji
**Apige: SImu Namba:**
**0786 641903 au 0716 172929**

**MKOPO WA HARAKA NA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL)** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumaliza tenda etc. Kwa maelezo zaidi piga: **0758 112 332. Karibu EFL**


**NIPASHE NI JIBU LAKO**
**NJOO UTANGAZE NASI**
**BIDHAA YAKO**
**KWA BEI NAFUU SANA**


### CHETI KIMEPOTEA



**DATIVA TOMAS MTUI** AMEPOTELEWA NA CHETI CHA ELIMU YA KIDATO CHA NNE,ALICHOSEMEA KTK SHULE YA SECONDARI MLAN'GA. ALICHOMALIZA MWAKA 2012 NA CHENYE **INDEX NO, S.4517-0008.** KWA YEYOTE ATAKAEKIONA ANAOMBWA ATOE TAARIFA KTK KITUO CHOCHOTE CHA POLISI, TAARIFA YA POLISI: **MOR/MVO/RB/95122/2020.**

### KUPOTEA KWA KADI

**Francis Julias Rwebogora** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki aina ya Honda yenye usajili wa namba **MC 405 BBX** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa:
**DAR/KIJ/RB/99440/2020**

115615102

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo
KIMARA

Usimamizi wa mirathi No;18/2020
Ombi la **DICKDANIEL GAUDENCE MGONDA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **GABRIEL GAUDENCE MGUNDA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 6/4/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 03/02/2020.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO KIMARA

215616802

JAMHURI YA MUUNGANO WA MUUNGANO WA TANZANIA

### HATI YA KIAPO

Mimi **JORDAN DAUDI NYUMAYO** wa **S.L.P 2408 TANGA,** mtu mzima, mwenye akili zangu timamu bila kushawishiwa na mtu yeyote kwa hiari yangu mwenyewe ninaapa nakuthibitisha haya yafuatao-

1. Kwamba mimi **JORDAN DAUDI NYUMAYO** ni mmiliki wa nyumba kiwanja **No.5 Plot No.219** eneo la **NGAMIANI** jijini Tanga.
2. Kwamba kwa bahati mbaya Hati ya kumiliki nyumba hiyo imepotea nimefika kituo cha polisi Kongwa na kupewa Loss report Na.**KNG/RB/131/2012** ya tarehe **02/02/2012.**
3. **Kwamba** naiomba ofisi yako itambue kuwa nilikuwa na Hati ya kumiliki Nyumba lakini kwa bahati mbaya imepotea, kwa hiyo ninaomba kupatiwa Hati nyingine kwa jina la **JORDAN DAUDI NYUMAYO.**

**UTHIBITISHO**
Nathibitisha kuwa yote niliyoyatamka ni ya kweli kweli tupu kwa kadri nijuavyo na kuamini kuwa ni kweli na kwa kutia nguvu tamko hili nimefika mbele ya Hakimu Mahakamani na kutia sahihi yangu kuwa ni kweli.

IMETHIBITISHWA HAPA TANGA NA
JORDAN DAUDI NYUMAYO
TAREHE 03 MWEZI 2 2020

JORDAN DAUDI NYUMAYO

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MJINI TANGA

2156162O2

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LUCAS STEVEN JAMES.**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari
Yenye namba ya usajili
**T865CUC**
Chassis **No. 4499952**
Engine **No. 6025786**
Kwa atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu nae.
**ARU/NAM/RB/110768/2020.**

215616302

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;26/2020**

**Ombi la AGNES ALPHONCE MAKINYA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ANTHONY LAWRANCE KIWAMBO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 25/02/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 04/02/2020.

HAKIMU

215615702

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;24/2020**

**Ombi la MWANAHAMIS ISSA FUKU Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ABDUL SEMINDU PAWA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 20/02/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 04/02/2020.

Tarehe 4/2/2020
Sahihi ya Hakimu
HAKIMU

215615402


**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi**

**Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# PIATEK AIGA KWA LEWANDOWSKI



**MUNICH,** Ujerumani

MSHAMBULIAJI wa Hertha Berlin, Krzysztof Piatek, amebainisha kwamba anatumia kila nafasi anayopata kujifunza kutoka kwa mchezaji mwenzake wa timu ya Taifa ya Poland, Robert Lewandowski.

Piatek alijiunga na Hertha kutoka Milan kwa ada iliyoripotiwa kuwa euro milioni 27 Januari mwaka huu, baada ya kutokuwa na wakati mzuri pale kwenye dimba la San Siro.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, alianza kuichezea klabu hiyo kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani akitokea benchi wakati wa sare ya bila kufungana dhidi ya Schalke Ijumaa.

Huku akiwa pamoja na mshambuliaji huyo bora duniani kwa sasa katika timu ya taifa, Piatek amesema anamtazama kwa karibu mno nyota huyo wa klabu ya Bayern Munich kila anapopata nafasi.

"Yeye ni mshambuliaji bora Ujerumani na mmoja wa wachezaji bora duniani," alisema Piatek akiuambia mtandao wa Bundesliga.

"Wakati ninapofanya mazoezi na Robert kwenye timu ya taifa mara zote namtazama yeye. Namwangalia kila kitu anachofanya.

"Nazungumza naye kila wakati kwa sababu nataka kujifunza, na natumaini nitajifunza mengi zaidi kutoka kwake."

Piatek amefunga mabao manne tu katika mechi 18 alizocheza kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, akiwa na Milan msimu huu kabla ya kuhamia Hertha.

# Werner aviita vigogo vya EPL na LaLiga

**MUNICH,** Ujerumani

MSHAMBULIAJI Timo Werner amefungua mlango wa kuhamia kwenye Ligi Kuu ya England au Hispania wakati muda utakapofika wa kuondoka RB Leipzig.

Nyota huyo wa timu ya Taifa ya Ujerumani, Werner alitarajiwa kujiunga na Bayern Munich mwanzoni mwa msimu huu 2019-20 wakati mkataba wake ulipobakiza mwaka mmoja, lakini usajili huo ulishindakana baada ya kusaini miaka minne na Leipzig.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, amekuwa akihusishwa na mpango wa kwenda kwa miamba wa Ligi Kuu ya England, Liverpool, Manchester United na Chelsea, huku pia akitajwa kuwaniwa na Barcelona na Real Madrid.

Werner amefunga mabao 25 katika mechi 28 alizoichezea Leipzig katika mashindano yote msimu huu na anafuraha na namna mambo yanavyokwenda pale katika dimba la Red Bull Arena.

Hata hivyo, mshambuliaji huyo hajaondoa uwezekano wa kuhamia katika moja ya ligi ya England au Hispania kwa siku za usoni.

"Nafikiri kucheza nje ya Ujerumani kwa siku zijazo, lakini kwa uhakika kabisa sijajua wapi nitakwenda. Nipo wazi kwa kila kitu," alisema Werner akinukuliwa na Kicker.

"Wakati nilipokuwa likizo nchini Marekani, klabu za Uingereza zilikuwa zinanifuata kila wakati. Lakini timu kubwa kabisa za Hispania ambako utakuwa wakati mzuri zaidi kwangu kucheza kule, zilinifuata pia."






# *Rakitic abainisha kuondoka Barca*

**BARCELONA,** Hispania

KIUNGO wa Barcelona, Ivan Rakitic anaweza kufanya uhamisho wa kushangaza na kwenda Atletico Madrid msimu ujao.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Croatia ameripotiwa kutokuwa na furaha pale Camp Nou na alikuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka hapo kipindi cha usajili wa dirisha dogo lililopita.

Na sasa amebakia kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, lakini anaweza kuondoka pale Barcelona.

Atletico Madrid tayari wamefanya mazungumzo na Rakitic kuhusu uwezekano wa kuondoka mwishoni mwa msimu na kujiunga nao, kwa mujibu wa Cadena SER.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, mkataba wake na Barcelona unamalizika 2021 na alitua hapo akitokea Sevilla mwaka 2014.

Rakitic alibainisha Jumapili kwamba, alifikiria kuondoka Januari, na sasa anaona uhamisho wake unaweza kufanyika mwishoni mwa msimu huu.

# DEMBELE ASHINDWA KURUDI UWANJANI




**BARCELONA,** Hispania

OUSMANE Dembele ameshindwa kurejea uwanjani wakati akijaribu kurudi kutoka kuuguza majeraha pale Barcelona.

Barca imethibitisha kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 "alijitonesha mguu wake wa kulia" wakati wa mazoezi Jumatatu.

Klabu hiyo ilisema mchezaji huyo ataendelea na matibabu na hawakutoa muda maalumu ambao atarudi uwanjani.

Dembele hajacheza tangu alipotolewa kipindi cha kwanza wakati Barca wakishinda 3-1 nyumbani dhidi ya klabu yake ya zamani ya Borussia Dortmund kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya makundi Novemba 27, mwaka jana.

Awali alikuwa nje ya dimba kwa wiki 10 na alianza katika mechi tatu tu za LaLiga msimu huu, akitumia muda mwingi nchini Qatar ambako alikuwa akitibiwa.

Kocha mpya wa Barcelona, Quique Setien alizungumza na Dembele wiki iliyopita, na kusema hana tatizo kwa klabu kushindwa kusajili mshambuliaji wakati wa dirisha la Januari kwa sababu mshambuliaji huyo atakuwa bora wakati atakaporudi.

Dembele alijiunga na Barca kwa ada ya awali ya euro milioni 105 Agosti 2017, lakini amekuwa akisumbuliwa na majeraha kwa kipindi kirefu cha maisha yake nchini Hispania.

## Son ataka Tottenham kuipiku Chelsea 4-bora




**LONDON,** England

SON Heung-min ameishauri Tottenham kujipanga sawasawa kwenye mbio zake dhidi ya Chelsea kuwania kumaliza kwenye nne bora ya Ligi Kuu ya England.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Korea Kusini, Son alifunga bao wakati Spurs wakiifunga Manchester City 2-0 kwenye Uwanja wa Tottenham Hotspur, Jumapili.

Kikosi hicho cha Jose Mourinho sasa hakijapoteza mchezo wowote kati ya mitatu iliyopita baada ya kupoteza mechi mfululizo.

Pengo lake na Chelsea, ambayo ipo nafasi ya nne, kwa sasa ni pointi nne na timu hizo zitakutana pale kwenye dimba la Stamford Bridge Februari 22.

Son anataka Tottenham kupambana ili kuhakikisha wanashinda mechi zake zote zilizobaki.

"Tuna mechi zaidi ya 10 kwa sasa," alisema. "Tuna mechi nyingi za kucheza, lakini mwisho wa msimu tutaona nini kitakachotokea.

"Tunajaribu kujipanga kwa kila mchezo. Tunatakiwa kuhakikisha tunapata pointi nyingi kadri inavyowezekana.

"Manchester City ni wazuri na walicheza vizuri zaidi kipindi cha kwanza. Tulitakiwa kujilinda, lakini kipindi cha pili tulikuwa imara."

## *Morata aipa pigo safu ya ushambuliaji Atletico*

**MADRID,** Hispania

SAFU ya ushambuliaji ya Atletico Madrid imekuwa kwenye wakati mgumu zaidi baada ya kuumia kwa Alvaro Morata ambapo anaweza asiwapo kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora dhidi ya Liverpool.

Morata alitolewa nje mapema kipindi cha pili wakati Atletico wakifungwa bao 1-0 na vinara wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Real Madrid Jumamosi na ameonekana kuumia misuli kwenye mguu wake wa kulia.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya Hispania, Morata ataukosa mchezo dhidi ya Granada wikendi inayokuja na kuna uwezekano akaikosa Liverpool Februari 18. Atletico, ambayo haijashinda mechi tano zilizopita katika mashindano yote, walicheza bila Joao Felix na Diego Costa wakati wakifungwa pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu.

Majeruhi ya Joao Felix yanaonekana kutokuwa makubwa sana, huku Costa yeye anaweza kurudi kabla ya mchezo huo dhidi ya Liverpool.

Atletico wapo nafasi ya sita kwenye msimamo wa LaLiga, wakipitwa pointi tatu kwenye nne bora.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# FERNANDINHO AIONYA MAN CITY 4-BORA EPL

Kama hatuwezi kuendelea kuzingatia, tunaweza kutolewa nje ya nne bora, hivyo...

**MANCHESTER,** England

FERNANDINHO ameionya Manchester City kuwa inaweza kukabiliwa vita ya kuwania kumaliza nafasi nne za juu kwenye Ligi Kuu kama kuhaha kwao kupata matokeo kunakowakabili kutaendelea.

**Kikosi hicho cha Pep Guardiola kimekuwa karibu zaidi na nafasi ya tano kuliko ya kwanza baada ya kushindwa kuibuka na ushindi katika mechi zake mbili kati ya tatu za Ligi Kuu zilizopita, ikiwa ni pamoja na mchezo wa Jumapili waliopoteza kwa mabao 2-0 dhidi ya Tottenham.**

Mabingwa hao mara mbili watetezi wa Ligi Kuu, wapo pointi 22 nyuma ya vinara wa ligi hiyo, Liverpool na pointi 14 juu ya timu inayoshika nafasi ya tano, Spurs.

Lakini kiungo Fernandinho, anasema City inaweza kukabiliwa na kuingia vitani kuwania kutinga nne bora kama wataendelea kuwa na kiwango kibovu.

"Tunapaswa kuzingatia Ligi Kuu pia, na si mashindano mengine pekee," alisema.

"Kama hatuwezi kuendelea tunaweza kutolewa nje ya nne bora, hivyo tunahitaji kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa msimu ujao. Tutazingatia kuhusu makombe na Ligi ya Mabingwa pia, lakini sisi ni wanataaluma.

"Tunahitaji kuonyesha tabia yetu hadi mwishoni mwa msimu na kumaliza ligi katika njia sahihi inayowezekana."

Wakati wakiwa nyuma katika ligi, City imetinga fainali ya Kombe la EFL na bado imo kwenye Ligi ya Mabingwa na Kombe la FA.

Lakini Fernandinho anahisi kutokuwa na uwezo kwa City kuchukua nafasi yake, kumethibitika kuwagharimu.

"Kipindi cha misimu minne iliyopita, tumekuwa tukicheza namna hii. Katika misimu miwili iliyopita tulishangaza, tumeshinda Kombe la Ligi Kuu mara mbili, tulivuna pointi 198 kwa misimu miwili iliyopita, hatukubadilika sana," alisema.

"Tunaendelea kwa njia hiyo, kutengeneza nafasi, lakini kama hatufungi mabao, huwezi kushinda mechi.

"Tunahitaji kutafuta suluhisho, kuanzia kesho katika mazoezi na kuendelea kwa mechi ijayo dhidi ya West Ham nyumbani.

"Tunapaswa kurekebisha hali hiyo na kuendelea kushinda."

## ZISIKUPITE

### ATAKA KEPA AUZWE

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard yupo katika vita na klabu ya kumuuza kipa Mhsipania Kepa Arrizabalaga, 25. ***(Mirror)***

### MADRID SASA KWA MBAPPE

Real Madrid ipo tayari kwenda kumsajili mshambuliaji wa Paris St-Germain, Mfaransa Kylian Mbappe, 21. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### VAN DIJK, ALISSON KUFUNGWA

LIVERPOOL wana hamu ya kumfunga zaidi beki Mholanzi Virgil van Dijk, 28, na kipa Mbrazil Alisson, 27, kwa mikataba ya muda mrefu zaidi. ***(Independent)***

### POPE KUMRITHI KEPA CHELSEA

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard anataka pengo la Kepa Arrizabalaga endapo akiuzwa lizibwe na kipa wa Burnley na England, Nick Pope, 27. ***(Express)***

### KUJIFUNGA LEICESTER

KIUNGO wa England, James Maddison, 23, yupo karibu kukubali dili la mkataba mpya na Leicester. ***(Telegraph)***

### LINGARD AWANIWA ATLETICO

ATLETICO Madrid na Roma zinaongoza katika nafasi ya kumsajili kiungo wa England, Jesse Lingard, 27, kama ataondoka Manchester United. ***(ESPN)***

### AIZAMISHA UTD, LIVER

LIVERPOOL, Manchester United na Chelsea zinamuwinda Timo Werner, 23, amesema atafungua milango ya kujiunga na klabu sahihi. Straika huyo wa Ujerumani, ana mabao 25 katika mashindano yote akiwa na RB Leipzig msimu huu. ***(Kicker - via Evening Standard)***

### AMULIKA CHINA, MAREKANI

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid na Wales, Gareth Bale, 30, anaweza kujiunga na Ligi Kuu China ama ya Marekani [MLS], kuliko Ligi Kuu England, wakati atakapoondoka katika klabu hiyo ya Hispania. ***(Star)***

### YAKWAMA KWA GABRIEL

ARSENAL na Everton zilishindwa kutoa ofa ya kumsajili beki wa Lille, Mbrazil Gabriel, 22, katika dirisha la Januari. ***(Le10Sport - in French)***

### TUCHEL AMFUNGUKIA MBAPPE

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain, Mfaransa Kylian Mbappe, 21, hatatumia kukwaruzana kwake na kocha Thomas Tuchel wakati akifanyiwa mabadiliko 'sab' kama sababu ya kuondoka klabuni hapo, ameeleza kocha huyo. ***(Goal)***

### SLIMANI KIDUCHU ATUE INTER

INTER Milan walikaribia kukubaliana dili la kumsajili mshambuliaji wa Leicester, Mualgeria Islam Slimani, 31, siku chache kabla ya dirisha la usajili la Januari kufungwa. ***(Calciomercato - in Italian)***

## Malindi yapania 3 za Selem View leo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Malindi imejiandaa kuhakikisha inapata ushindi wa kishindo katika mchezo wake wa leo dhidi ya Selem View kutoka kisiwani Pemba, ambao utakapigwa katika Dimba la Amaan majira ya saa 10 alasiri, kwa mujibu wa Meneja wa timu hiyo, Kau Hojofat.

Malindi wanashuka dimbani wakiwa na alama 10 zinazowafanya kukaa katika nafasi ya 12 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar inayoshirikisha timu 16.

Akizungumza na gazeti hili, Hojofat alisema timu yake imefanya maandalizi ya kutosha kuelekea mchezo huo ambao kwao wanaona ni mgumu, lakini pia wakiwaheshimu wapinzani wao, Selem View.

Alisema kikosi hicho ambacho kimejumuisha wachezaji wapya waliowasajili kipindi cha dirisha dogo, kimezidi kuimarika kutokana na nguvu hiyo mpya na wana uhakika wakufanya vizuri kwenye mzunguko huu wa lala salama.

Aidha, alisema Selem View ni timu isiyotabirika pale inaposhuka dimbani kutoka na uchezaji wao, lakini wamejipanga vya kutosha kuweza kuibuka na pointi tatu.

Mechi nyingine zitakazopigwa leo, Mwenge ya kisiwani Pemba itaikaribisha timu ya Polisi kutoka Unguja katika Dimba la Gombani majira ya saa 8:00 mchana huku saa 10 alasiri Chipukizi ikiikaribisha Jang'ombe Boys katika uwanja huo.

## Kabadi kukabidhi Kalenda BMT

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha mchezo wa Kabadi Tanzania ndani ya wiki hii kinatarajia kukabidhi kalenda ya mwaka huu Baraza la Michezo (BMT), imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa chama hicho, Abdallah Nyoni, alisema awali walipanga waikabidhi kalenda hiyo wiki iliyopita, lakini ilishindikana kutokana na baadhi ya vitu kutokamilika.

"Wiki hii tunatarajia kuipeleka BMT kalenda yetu ya mwaka huu kuna vitu ambavyo tunamalizia kuviweka sawa," alisema.

Mwenyekiti huyo aliendelea kusema, mbali na hilo kwa sasa wanajiandaa na mashindano ya Afrika Mashariki ya kuazimisha Siku ya Kabadi, yatakayofanyika Machi 24-28, mwaka jijini Nairobi, Kenya.



# BABA WA SAMATTA NAYE AWAANGUKIA WATANZANIA

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya juzi nahodha wa Taifa Stars na mchezaji wa Aston Villa, Mbwana Samatta kuwaangukia mashabiki wake na Watanzania kwa ujumla akiwataka kuacha tabia ya kuandika maneno makali au lugha isiyofaa katika akaunti za wachezaji au klabu hiyo kwa sababu hali hiyo inamkera, hatimaye baba yake mzazi, Mzee Samatta naye ametoa raia hiyo.

**Baadhi ya mashabiki wake hususan kutoka Tanzania, wamekuwa wakiandika ujumbe katika mtandao wa Aston Villa, wakimshutumu nahodha wa klabu hiyo, Muingereza Jack Grealish kwa madai ya kuwa mchoyo kwa kutomlisha pasi Samatta.**

Na Samatta juzi kupitia akaunti yake ya Instagram aliandika: "Mashabiki wa soka Tanzania nafahamu kuwa mnanipenda kijana wenu na mnapenda nifanye vizuri katika timu yangu mpya, lakini nawaomba muache kutoa maneno ya kashfa au yenye mlengo mbaya katika akaunti za timu au wachezaji, binafsi sifurahiswi."

Ujumbe huo uliungwa mkono jana na baba yake mzazi, Mzee Samatta ambaye alimwambia mwandishi wetu kuwa hata yeye binafsi, amekasirishwa na mashabiki wa Tanzania kuandika lugha za matusi katika ukurasa wa timu ya Aston Villa.

Mzee Samatta alisema, ni kweli wachezaji wa Aston Villa michezo yote miwili waliyoicheza walionekana kutotoa pasi kwa Samatta, lakini aliwataka Watanzania wavute subira pamoja na kuacha kuandika maneno ya ubaguzi, ambayo yanaweza kumpa wakati Samatta Jr wakati mgumu.

Alisema Samatta Jr ni mpambanaji, hivyo atakuwa kinara tu wa kufunga mabao, jambo ambalo aliwataka Watanzania wenzake kuwa na subira.

"Nimekasirishwa sana kuona maneno yaliyoandikwa kwenye ukurasa wa Aston Villa ambayo yamekandia wachezaji wenzake, si kitu kizuri, tusubiri tuone kwa sababu kocha wake ameliona hilo nafikiri ataliweka sawa, alisema Mzee Samatta.

Alifafanua kuwa hali hiyo pia aliwahi kumkumba Samatta Jr wakati alipojiunga na TP Mazembe na kisha KRC Genk ya Ubelgiji, lakini baadaye alikuwa mchezaji mzuri, hivyo jambo linalohitaji subra tu.

"Hiyo ni moja ya changamoto kwa Samatta anatakiwa akumbuke amevuka vitu vingapi mpaka kufika alipo sasa, naamini yatapita atakaa sawa kwa sababu kipaji anacho," alisema.

Alisema tangu mwanawe aandike ujumbe huo kwenye ukurasa wake, hajazungumza naye kitu chochote zaidi ya kumpongeza jinsi alivyocheza.

"Mimi nilimpongeza tu jinsi alivyocheza, lakini sijazungumza naye chochote juu ya hilo lililojitokeza," alisema huku akimtakia kila la heri katika maisha mapya ya soka, na kumtaka aongeze bidii asikatishwe tamaa na changamoto hizo.




Balozi wa Kampeni ya OMO Ng'arisha Festival, msanii wa muziki wa Singeli, Sholo Mwamba, akitumbuiza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo katika Uwanja wa Zakhem, Mbagala jijini Dar es Salaam hivi karibuni.
**PICHA : JUMANNE JUMA**

# *Hat-trick zafunika za msimu uliopita*

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI wa Kagera Sugar, Kelvin Sabato ameingia katika orodha ya wachezaji waliofunga hat-trick katika raundi hii ya kwanza, hiyo ikiwa ya nne msimu huu kufungwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, hivyo kuzipiku zilizopatikana kipindi kama hiki msimu uliopita.

Msimu uliopita katika raundi ya kwanza, zilifungwa hat-trick mbili tu na msimu ukafungwa zikiwa zimepatikana hat-trick sita, tofauti na sasa ambapo hadi mzunguko huu wa kwanza unaelekea kukamilika tayari zimepatikana nne.

Kwa msimu uliopita, Alex Kitenge wa Stand United alikuwa wa kwanza kuandika hat-trick wakati wakilala kwa mabao 4-3 dhidi ya Yanga, kisha raundi hiyo ya kwanza ikakamilika kwa aliyekuwa mshambuliaji wa Simba [kwa sasa Al Ittihad Alexandria ya Misri], Mganda Emmanuel Okwi kutupia mabao matatu wakati wakiibuka na ushindi wa 5-0 dhidi ya Ruvu Shooting.

Raundi ya pili ya msimu uliopita ilifunguliwa kwa hat-trick ya Salum Aiyee aliyekuwa akichezea Mwadui FC wakati wakishinda 4-0 dhidi ya Kagera Sugar, kisha akapokelewa na Fully Maganga wakati huo Ruvu Shooting ikiichapa Mwadui FC mabao 6-2.

Waliofunga mlango wa hat-trick msimu uliopita walikuwa washambuliaji wa Simba, Okwi na Mnyarwanda Meddie Kagere ambao waliondoka na mipira kwa pamoja kwa kila mmoja kutupia mabao matatu wakati timu yao ikishinda 8-1 dhidi ya Coastal Union ya Tanga.

Kwa msimu huu, Sabato ambaye alisajiliwa na Kagera Sugar akitokea timu ya Gwambina inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza ambayo ilimsajili kutoka Mtibwa Sugar, amefunga hat-trick yake ya kwanza na ya nne kufungwa msimu huu, wakati wakiichapa Singida United 3-0 katika Uwanja wa Kaitaba wiki iliyopita.

Hata hivyo, mlango wa hat-trick msimu huu ulifunguliwa na Ditram Nchimbi wakati akichezea Polisi Tanzania dhidi ya timu yake ya sasa, Yanga, timu hizo zikitoka sare ya mabao 3-3. Ikumbukwe Nchimbi amejiunga na Yanga katika usajili wa dirisha dogo msimu huu.

Obrey Chirwa alifuata kwa kutupia hat-trick ya pili katika Ligi Kuu msimu huu, wakati Azam FC ikiichapa Alliance kwa mabao 5-0, na baada ya hapo akafuata Daruesh Saliboko wa Lipuli aliyecheka na nyavu mara tatu wakishinda 3-0 dhidi ya Singida United.

# Michezo

Jumatano Februari 5, 2020
Nipashe




Fernandinho aionya City 4-bora EPL UKURASA 30




# Kagere, Tshishimbi waipa serikali bil. 1.7/-

## ●●● Aussems, Zahera na mapro wengine wa mwaka 2017/18 pia wahusika katika...

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKATI baadhi ya wadau wa soka wakipiga kelele idadi ya wachezaji wa kigeni wanaosajiliwa na klabu za Ligi Kuu Bara kupunguzwa kutoka 10 wanaoruhusiwa kwa sasa, 'mapro' hao pamoja na makocha wa kigeni wameiingizia serikali jumla ya Sh. bilioni 1.73 kama malipo ya kodi za ajira zao za kufanya kazi nchini, imeelezwa.

> **Baadhi ya wadau wa soka wanaamini uwapo wa wachezaji wengi wa kigeni unafinya nafasi ya wazawa kuonekana jambo ambalo wanadai linadhohofisha hadi timu ya Taifa, Taifa Stars, lakini sasa serikali imetangaza kuingiza kiasi hicho cha fedha kwa kipindi cha mwaka 2017/18.**

Miongoni mwa baadhi ya wachezaji wa kigeni walikuwapo msimu uliopita, ambao kodi hiyo ya kipindi cha 2017/18 makato yao yamehusika ni pamoja na mshambuliaji wa Simba, Mnyarwanda Meddie Kagera na kiungo wa Yanga, Mkongomani Papy Tshishimbi.

Kadhalika, aliyekuwa Kocha wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems na wa Yanga, Mkongomani Mwinyi Zahera nao ni miongoni, hao wakiwa ni baadhi tu kwani wapo wachezaji wengi wa kiegeni na makocha wa kigeni katika klabu hizo, ikiwamo Azam FC, KMC na nyinginezo.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, ndiye aliyeanika pato hilo la serikali lililotokana na kodi ya wachezaji na makocha hao wa kigeni nchini, wakati alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Chemba (CCM), Juma Nkamia.

Katika swali lake, Nkamia alihoji serikali imekusanya kiasi gani cha kodi kutoka kwa makocha na wachezaji wa kigeni wanaofanya kazi nchini kwa mwaka wa fedha 2017/18.

Akijibu swali hilo, Dk. Kijaji alisema kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004, kifungu cha 7, kila mtu anayepata mapato yatokanayo na ajira ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anawajibika kulipa kodi ya mapato kulingana na kipato chake.

"Katika kipindi cha mwaka 2017/2018, jumla ya Sh. bilioni 1.73 zilikusanywa kama malipo ya kodi ya ajira kutoka kwa makocha na wachezaji wa kigeni wanaofanya kazi hapa nchini," alisema.

Aidha, alisema timu zinazoajiri makocha na wachezaji kutoka nje ya nchi, kodi ya mapato lazima mlipaji awe mkazi ndani ya nchi na mgeni akifikishia miezi sita lazima alipe na muajiri atoe taarifa.

Aliwataka waajiriwa wote kulipa kodi kulingana na sheria zinavyoelekeza na kusisitiza kuwa ni jukumu la mwajiri kutoa taarifa ya nani analipwa nini ndani ya taasisi au kampuni ili kodi ya mapato ilipwe kwa mujibu wa sheria.

"Kila mgeni akifikisha miezi sita anahesabika ni mkazi (local resident) na anapaswa kulipa kodi, ni jukumu la mwajiri kutoa taarifa ya nani analipwa nini ili kodi zote stahili ziweze kulipwa kwa mujibu wa sheria," alieleza Dk. Kijaji.

# Kichuya safi Simba Miquissone bado

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kimya cha muda mrefu huku mashabiki wakitaka kuwaona uwanjani wachezaji wao waliosajili katika dirisha dogo lililofungwa Januari 15, mwaka huu, Shiza Kichuya na Luis Miquissone, hatimaye uongozi wa Simba sasa umefunguka.

Kichuya alisajiliwa na Simba baada ya kuachana na klabu ya Daraja la Kwanza, Pharco ya Misri iliyokuwa imemsajili kabla ya kumtoa kwa mkopo klabu ya Enppi inayoshiriki Ligi Kuu ya Misri, wakati Miquissone alitua akitokea UD Songo ya Msumbiji alipokuwa akiichezea kwa mkopo akitokea Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini.



Tangu kusajiliwa kwa wachezaji hao hawajaichezea kwenye mechi za Ligi Kuu, zaidi ya Miquissone kuonekana akitokea benchi katika mechi ya nusu fainali ya Kombe la Mapinduzi dhidi ya Azam FC iliyopigwa Uwanja wa Amaan mjini Zanzibar, lakini sasa Kichuya yupo huru kuanza kukipiga kutokana na Uhamisho wake wa Kimataifa (ITC) kutua.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Simba imeeleza: "Hati ya Uhamisho wa Kimataifa (ITC) ya Shiza Kichuya imefika. Sasa tupo huru kumtumia kwenye mchezo wowote iwapo kocha mkuu atahataji kumtumia."

Kuhusu Miquissone taarifa Simba ilieleza: "Bado ITC ya Luis Miquissone haijatolewa. Jambo hilo linafanyiwa kazi na FIFA. Majibu ya mwanzoni FIFA walihitaji maelezo zaidi na tuliwatumia Jumamosi iliyopita. Kwa sasa yanasubiriwa maamuzi ya Kamati ya Hadhi za Wachezaji ya FIFA."

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >